ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/ Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/ Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/ Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara na Viwanda /Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni,**

			Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati/ Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**

28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chake Chake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 12 Juni, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika Kikao cha Baraza cha tarehe 17 Mei, 2018 Mhe. Rashid Makame Shamsi aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 8. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliahidi kujibu kwa maandishi. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, katika Mkutano wa Kumi wa Baraza la Wawakilishi, Kikao cha Tarehe 17 Mei, 2018. Wizara ya Fedha na Mipango iliulizwa swali la msingi Nam. 8 la Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar kuhusu kuhusu malengo ya Shirika la Bima. Kutokana na majibu ya swali hilo Mhe. Rashid Makame Shamsi aliuliza swali la nyongeza. Mhe. Shamsi alitaka kujua Shirika la Bima kwa mwaka 2016 limepata faida ya kiasi gani.

Mhe. Spika, naomba kujibu swali hilo la nyongeza la Mhe. Rashid Makame Shamsi kwamba Shirika la Bima kwa mwaka 2016 lilipata faida ya Tshs. Mil. 900 baada ya kodi na gawio la Serikali. Naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Hotuba ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/2019. Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 152

Hukumu za Faini katika Kesi za Udhalilishaji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazee ambao watoto wao wamekumbwa na matukio ya udhalilishaji baadhi ya hukumu zinatolewa

mahakamani za faini na fidia, ambapo ile faini inakuwa kubwa na inakwenda serikalini na fidia inakuwa ndogo anayopatiwa muathirika.

(a) Je, kwa utaratibu huu wa hukumu serikali haioni vibaya kujipatia fedha za faini kubwa zinazotokana na kadhia ya mtu kubakwa au kudhalilishwa.

(b) Kwa nini faini isiwe ndogo na fidia ikawa kubwa kwa muathirika ili muathirika apate kugharamia matibabu au hali ya kuathirika kiakili na kimwili.

(c) Vigezo gani vinatumika kuwahukumu wabakaji faini kubwa na fidia ndogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 152 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kawaida mahakama hufanya kazi zake kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwa kutoa adhabu na fidia pindipo mtuhumiwa anapatikana na hatia. Mara nyingi faini inatamkwa na sheria husika na namna gani faini itolewe, lakini fidia kwa kawaida sheria husema tu muathirika wa udhalilishaji alipwe fidia. Lakini suala la fidia kiasi gani imeachiwa mahakama itumie busara zake kupima kiwango cha fidia kufuatana na ukubwa wa udhalilishaji uliofanyika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la msingi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, si vibaya kwa **s**erikali kupata fedha za faini zinazotokana na kesi za udhalilishaji, kwa sababu faini hizi hutamkwa kisheria na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza hili. Kwa hivyo, kama Baraza litaona ipo haja ya kurekebisha kasoro hii, basi sheria inayotoa adhabu kwa makosa haya irekebishwe ikiwa ni pamoja na viwango vya fidia kwa waathirika. Lakini serikali inashauri kuwa ni busara kuiachia mahakama kutumia busara zake katika kiwango cha fidia kufuatana na aina ya udhalilishaji.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali namba 152 (a) kwamba ni suala la Baraza hili la Wawakilishi kuamua kwamba faini kwa makosa haya ya udhalilishaji iwe ndogo na fidia iwe kubwa. Lakini naomba kutahadharisha kuwa, suala la fidia ni la kimadai zaidi na ili fidia iwe kubwa lazima mhanga wa udhalilishaji athibitishe jinsi gani alivyoathirika na udhalilishaji huo. Ndio maana ili kuepuka hayo, mahakama imeachiwa itumie busara zake kupima kiwango cha fidia kutokana na ukubwa wa udhalilishaji uliotendeka.

(c) Mhe. Spika, faini huwa inatamkwa na sheria husika ya Sheria ya Adhabu na Hukumu. Kigezo cha kutathmini fidia imeachiwa mahakama ipime uzito wa udhalilishaji uliofanyika na hatimae kuamua fidia kwa muathirika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mahakama inachukua fidia kubwa kuliko muathirika inatumia busara gani au ndio ule msemo wetu inakuwa maandishi ya kiarabu wakati muathirika kagharamika kiasi kikubwa mtoto yule au vipi.

(b) Kwa nini kesi za udhalilishaji kosa moja mahakama mtu mfano miaka mitatu, mitano, saba hakuna *formula* mahakama zinatumia vigezo gani. Kosa hilo hilo moja, mahakama hiyo hiyo, mtu huyo huyo anaweza kufungwa miaka saba, mwengine mitatu au miaka minne mnatumia vigezo gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi Wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi alitaka kujuwa busara gani ambayo mahakama huwa inatumia katika utoaji wa fidia.

(a) Mhe. Spika naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba mahakimu wetu ni mahakimu ambao wenye elimu, wenye kujua maadili yao na wenye kuipenda kazi yao. Sasa inapotokea wanapotoa maamuzi kwamba fidia kiwango fulani kinatoka pale tujue kwamba wameshaangalia mambo mengi. Miongoni mwa hayo wanachokiangalia kile kiwango kinachotolewa kama nilivyosema awali ni ule ukubwa wa lile kosa lilivyo, lakini kwa kuwa hawa mahakimu wetu ni mahakimu ambao wana ujuzi wanaielewa kazi yao, basi huwa hawayumbishwi yumbishwi na huwa wanaangalia jinsi lile kosa lilivyokuwa udhalilishaji ukubwa wake ulivyo, ndio huwa wanatoa hayo maamuzi ya kutoa hiyo fidia.

Lakini kusema kuna *formula* hii kwamba ukifanya hivi iwe hivi fidia yake ni hii hapana, kubwa zaidi mahakama kama mahakama wanaangalia ule ukubwa wa udhalilishaji uliotendeka. Kwa hivyo, inawezekana kosa la udhalilishaji lakini mmoja akapewa fidia aina nyengine kwa maana kwamba ukubwa unatofautiana kulingana na ule ukubwa wa lile kosa lenyewe. Kwa hivyo, fidia ina-*varies* kutoka ukubwa wa lile kosa lenyewe. Ni busara tu ambayo Mahakama huwa inatumia.

(b) Mhe. Spika, kuhusiana na suala la vifungo sheria yenyewe huwa inaelekeza kwamba kufanya kosa hili adhabu yake ni kuanzia tuseme miaka 10 hadi 12 kwa mfano. Sasa miaka 10 hadi 12 hapa hakimu au jaji amepewa ruhusa na sheria hii kutoa maamuzi baina ya 10 na 12. Kwa hivyo, si dhambi hakimu au jaji kutoa maamuzi hayo, inawezekana sheria

imesema miaka 10 hadi 12, akasema basi namfunga miaka 10, sio kosa. Kwa sababu sheria yenyewe imetoa nafasi kwa hakimu au jaji kutoa maamuzi yale. Kwa hivyo, hii inategemea na sheria yenyewe. Kama miaka 10 hadi 12, kwa hivyo inawezekana hakimu au jaji akatoa miaka 10, akatoa 11 au akatoa miaka 12. Kwa hivyo, inategemea yeye mwenyewe atakavyotoa yale maamuzi kulingana na kesi yenyewe ilivyo. Nashukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na kunipa nafasi asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika kesi zinazosikitikiwa sana na wananchi ni kesi za udhalilishaji na wananchi wengi wao waathirika hupeleka kesi hizi katika vituo vya polisi ili kuona kwamba zitapelekwa mahakamani na kupata haki zao. Lakini Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa kesi hizi katika vituo vya polisi hubadilishwa maana yake na kupewa maana nyengine. Wakati ushahidi ulishapatikana daktari amesha- *prove* kwamba hili ni udhalilishaji, lakini ikifika polisi inaanza kubadilishwa na kupewa jina jengine badala ya udhalilishaji.

Je, Mhe. Naibu Waziri kuna taratibu gani za kisheria ambazo zitatumika ili wananchi wale watakaokumbwa na kadhia hii kuwasaidia kuondokana na tatizo hili. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, sina uhakika na anachokisema Mhe. Mwakilishi kwamba Jeshi la Polisi katika kesi za udhalilishaji basi huwa wanabadilisha pengine kutoka kesi za udhalilishaji kwenda kesi nyengine, hilo sina uhakika kama linafanywa na Jeshi la Polisi. Lakini kama hili lipo na Jeshi la Polisi wanafanya hivi hili ni kosa kwa mujibu wa sheria. Lakini nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi pale ambapo linapotokezea suala kama hili wamepeleka kesi zao katika Jeshi la Polisi na kesi zao zimebadilishwa kutoka kwa mfano udhalilishaji kwenda kesi nyengine, basi wasisite kutoa taarifa katika vyombo mbali mbali vya sheria pamoja hata na Wizara pia kutuarifu tuweze kujua namna gani tunafuatilia suala hilo na sio kuliachilia tu moja kwa moja. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 102

Mkataba wa Matengenezo ya Jumba la Treni

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Pamoja na kwamba kazi za matengenezo makubwa ya Jumba la Treni *(Chawl Building)* zinaendelea vizuri, lakini zimebaki siku chache za mkataba huo kumalizika mwezi wa Mei, 2018. Katika kipindi hichi cha ujenzi lipo tatizo la msongamano wa wafanyabiashara wanaohitaji jengo hilo.

(a) Je, kampuni iliyopewa kazi ya matengenezo hayo itakamilisha na kukabidhi jengo hilo mwezi gani.

(b) Je, hadi sasa kampuni hiyo imeshafikisha asilimia ngapi za ujenzi wa jengo hilo na *guarantee* yake ni ya muda gani.

(c) Je, hadi sasa kampuni hiyo imeshalipwa kiasi gani cha fedha na kiasi gani ambacho kitabakishwa kwa wakati wa uangalizi ili kuhakikisha kwamba jengo hilo linakidhi viwango ambavyo vinakubalika kwa majengo kama hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 102 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kampuni iliyopewa kazi ya matengenezo ya Jumba la Treni wanaendelea vizuri na sasa wanamalizia uwekaji wa *lift* na kazi za nje *(external works*). Ujenzi huo ulitarajiwa kukamilika mwezi huu wa Juni, 2018 na kukabidhi jengo hilo ndani ya mwezi huu. Lakini makubaliano ya sasa Mhe. Spika, ni kwamba jengo hilo litakabidhiwa rasmi si zaidi ya tarehe 12 Julai, 2018.

(b) Mhe. Spika, hadi sasa kampuni hiyo imeshakamilisha asilimia 92 ya ujenzi wa jengo hilo. Kampuni hiyo imeweka *Performance Guarantee* kwa muda wote wa ujenzi. Pia, kuna muda wa mwaka mmoja wa kurekebisha kasoro kwa maana ya *Defect Liability Period* ambapo mkandarasi atahusika na matengenezo hayo au tatizo lolote litakalojitokeza katika ujenzi huo.

(c) Mhe. Spika, hadi sasa kampuni hiyo imeshalipwa TZS. 5,874,755,723.48 ikiwa sawa na asilimia 52 ya gharama yote ya ujenzi. Jumla ya TZS. 562,124,458 sawa na asilimia 5 ya malipo inabakishwa kama *retention* wakati wa uangalizi ili kuhakikisha jengo hilo linakidhi viwango vinavyokubalika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango yenye ufumbuzi na maelezo mazuri ya kina ya mahesabu naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kwanza nilitaka nijue tu hii kampuni yenyewe iliyopewa ni kampuni gani inaitwaje na inatokea wapi.

(b) Pamoja na kuniambia kwamba gharama halisi amenitajia ya Tshs. Mil. Mia Tano na Sitini na Mbili na kwamba kuna nyengine ya asilimia 5 ambayo itakuwa kama Tshs. Mil. Ishirini na Nane Laki Moja na Elfu Sita ambazo zitabakia kwa ajili ya uangalizi. Ningependa tu kujua hizi fedha zimetoka Serikali Kuu au zimetoka kwenye taasisi gani. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kampuni iliyojenga kwa maana Mkandarasi Mkuu *(Main Contractor)* ni Kampuni ya *CRJE East Africa Limited.* Kampuni hiyo ni ya Kichina lakini imesajiliwa hapa nchini. Lakini mbali ya kampuni hiyo kuna kampuni nyengine ambazo tunaziita Kampuni ya Wakandarasi wa Huduma kwa maana *sub-contractors* na hao wapo wanne. Kuna *Engineering Group* ambayo ilihusika na umeme tu pamoja na *ICT*, lakini pia kuna kampuni inaitwa *CITCC* zote Makao Makuu yake Dar-es-Salaam ilihusika na uwekaji wa vipoza joto kwa maana ya *aircondition,* na kuna kampuni iliyohusika na masuala ya *lift* kwa sababu ndani ya jengo lile mtakuwa na *lift* mbili, na kuna kampuni hii inaitwa *Derm Elevator* nayo ya Dar-es-Salaam. Lakini masuala yote ya ujenzi yalihusishwa na kampuni ya *CRJE*.

Lakini jumla Mhe. Mwakilishi alizungumzia *retention* na nilisema katika jibu mama kwamba tumemlipa asilimia 52 ya gharama yote ya ujenzi, na gharama yote ya ujenzi ni karibu Bil. 11.2.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa jengo lile lime-*cost* shilingi bilioni 11 katika ujenzi. Ni kampuni ngapi ambazo zime-*bid* katika ujenzi wa jengo lile na kiasi gani cha fedha ambazo walichosema wataweza kujenga katika *top reel companies* ambazo zilizo-*bid*.

(b) Katika ujenzi wao ambao karibu watakamilisha kama ulivyosema. Ni muda gani wametoa *guarantee* jengo lile litaweza kudumu katika hali iliyokuwa nzuri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Wakandarasi wangapi walio-*bid* hilo nitampa kwa maandishi, walio-*bid* na bei walizo-*bid* wakati huo wazabuni hiyo nitampa kwa maandishi.

Lakini Mhe. Spika, nilisema kwamba ujenzi ule ndani ya mkataba kuna suala la *defect liability period*, ni muda ule wa uangalizi, na muda wa uangalizi ni miezi kumi na mbili na hiyo ni *standard* kwa *contract* zote. Ama jengo lile litadumu kwa miaka mingapi wataalam wa ujenzi wanajua, lakini kwa umadhubuti uliojengwa pale na kuthibitishwa na mamlaka ya Mji Mkongwe na pia tulikuwa na wasimamizi wa ndani, jengo lile linaweza likenda zaidi ya miaka mia moja ijayo kwa sababu limekuwa *reinforced* kwa kiwango na *quality* ya hali ya juu kabisa.

Nam. 93

Ukosefu wa Maji Nchini

Mhe. Mhe. Asha Abdalla Mussa (Kny. Mhe. Bahati Khamis Kombo) - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya jitihada kubwa ili wananchi waondokane na tatizo la maji siku hadi siku na bado tatizo hili lipo Unguja na Pemba.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuweka miundombinu mbadala ya uchimbaji wa visima ili kuondoa tatizo hilo.

(b) Je, serikali haifahamu kuwa kuchimba visima vikubwa tunapata hasara kubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara yangu imekuwa ikifanya jitihada mbali mbali za kutafuta miundombinu mbadala ya uchimbaji wa visima ili wananchi waondokane na tatizo la maji ikiwa ni pamoja na kuandaa *Concept Note* ya uvunaji wa maji ya mvua, kufanya utafiti kwa kujenga matangi ya majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo ya Unguja na Pemba kupitia mradi wa *AfDB.*

Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji, imeshafanya majaribio *(pilot)* ya kuyachuja maji ya chumvi kuwa maji matamu *(desalination process)*, kupitia miradi mbali mbali Unguja na Pemba. Pamoja na jitihada hizo zilizofanywa, jitihada nyengine za karibuni ambazo zinaendelea kufanyika kupitia Kampuni ya *Oversea* ya *Morocco* ambayo kwa sasa ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu kwa kutumia maji bahari kuwa maji matamu kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

(b) Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, serikali haipati hasara kwa kuchimba visima vikubwa, kutokana kwamba visima vinavyochimbwa na Mamlaka ya Maji ni vikubwa na ni kwa ajili ya kuhudumia eneo kubwa, kisima kimoja kinachochimbwa katika eneo moja kinaweza kikahudumia vijiji zaidi ya viwili, au eneo zaidi ya moja. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi napenda nimuulize swali moja la nyongeza.
Kwa kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* imechimba visima vikubwa ambavyo vinaweza kuhudumia katika maeneo mengi ambayo tunatarajia wananchi wetu waweze kupata huduma hiyo ya maji safi na salama, baadhi ya visima hivyo vimekamilika na mmekabidhiwa rasmi *ZAWA.*
Je, visima hivi vitamaliza lini ili wananchi waweze kupata huduma hiyo.
Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilshi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.
Ni dhamira ya Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* kukamilisha visima vyote na ndio maana tuna programu ya kila muda kukamilisha visima vingapi, hii inatokana na nguvu ya uwezo wa fedha ambao tutakuwa tunaupata. Ahsante sana.

Nam. 170

Kampuni Zinazosimamia Mambo ya Utalii Kufanya Udanganyifu Wakati wa Usajili

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa baadhi ya kampuni za utalii (*tour operators)* zimesajiliwa na kupewa leseni lakini kuna baadhi ya kampuni hizo zinakiuka taratibu kwa kudanganya wakati wa usajili wake jambo ambalo ni kwenda kinyume kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utalii.

(a) Je, Kamisheni ya Utalii imefanya utafiti gani kuzibaini kampuni hizo na kuzichukulia hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

(b) Je, pamoja na kampuni za kigeni, kuna kampuni ngapi za wazawa ambazo nazo zimebainika kufanya udanganyifu kwa umiliki wa kampuni sambamba na vibali vya kufanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 170 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, hadi hivi sasa hakuna kampuni za utalii *(tour operators)* waliodanganya wakati wa usajili, hatuna taarifa yoyote ya kampuni kama hizo.

Hakuna kampuni ya ndani ama *National Tour Operator* ambayo imefanya udanganyifu wa aina yoyote, wote wanakuja wanajisajili wanapata *certificate* zao na wana-*operate* kama kawaida. Tutaendelea kuwa makini kwa ushauri wa Mheshimiwa kutazama kampuni ambazo zinafanya udanganyifu na kuwachukulia hatua za kisheria. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambaye najua na yeye yupo kidogo anayaweza mambo haya, lakini mimi nilikuwa na swali la kumuuliza kwa sababu Waswahili wanasema "Lisemwalo lipo na kama halipo linakuja" na sisi tumeyaona.

a) Je, Mheshimiwa nilitaka nijue ni lini hii Kamisheni ya Utalii imefanya uhakiki upya wa kuzibaini kampuni za *Tour Operator* ambazo zimesajiliwa za nje na ndani kwa mwaka huu wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni.

b) Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ambao ndio wanatoa vibali vya kazi. Ni vibali vingapi vimetolewa kwa watu kutoka nje wanaojishughulisha na biashara hii ya utalii kwenye hizi *Tour Operator* za nje wanaofanya kazi hapa ndani Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Nakubaliana na yeye kama jambo likiwa linazungumzwa aidha kama halipo basi linakuja. Kamisheni hii ya Utalii inafanya uhakiki kila mwaka kwa sababu leseni zetu zote zinatolewa mwaka hadi mwaka na zina-*expire* kila mwaka. Kwa hiyo, kuna leseni ya *Tour Operator,* kuna leseni ya *Airport Transfer,* kuna leseni za Minibus zile zinazopeleka wageni kutoka *Airport* kupeleka mahotelini na kadhalika. Zote leseni zao hutolewa kila mwaka, kwa hiyo hupata wasaa mzuri sana wa kufanya uhakiki kila mwaka kwa kila leseni wanazotoa kwa sababu leseni zao humalizika ama ku-*expire* mwaka hadi mwaka.

Kwa hiyo, uhakiki huo huwa unafanyika na kila mwaka tukibaini kwamba kuna kampuni imefungwa, kampuni hiyo haijaja kuomba leseni ripoti yake hutayarishwa na ripoti hiyo huletwa wizarani. Mimi mwenyewe nimebahatika kuona ripoti moja kama hiyo.

b) Kuhusiana na suala la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kupewa vibali. Vibali vipo vya aina nyingi kinachofanyika baada ya *ZIPA* kama ule mradi unaingia kwenye sheria ile ya *ZIPA* unathibitishwa na kupewa kibali cha mwanzo *ZIPA,* halafu *ZIPA* inamhusisha mtu wetu wa Kamisheni ambaye anaingia kwenye ile kamati kubwa kabisa ya *ZIPA.* Kuna mtu wa Idara ya Kazi, kuna mtu wa Idara ya Uhamiaji, kuna watu wa kodi na kuna mtu wetu wa Kamisheni ambaye anaingia moja kwa moja kule *ZIPA,* vibali vile hutolewa kupitia ile *One Stop Centre.*

Lakini kama kuna kampuni ambayo labda ndogo ni *Tour Operator* tu haijaingia kwenye usajili wa *ZIPA* kama mwekezaji mkubwa, basi kampuni ile huja moja kwa moja kuomba kwetu kupitia Kamisheni ya Utalii, na Kamisheni ya Utalii hutoa barua ya kumuombea kampuni ile au mfanyakazi yule anayehusika na kampuni ile vibali vyote vya kazi pamoja na uhamiaji, barua ile hutokea Kamisheni ya Utalii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, naomba kumuuliza maswali ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Kama Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kupitia nafasi yako Mhe. Waziri kuna *Tour Operator* ambao wana uwezo wanaweza kujitangaza wenyewe nchi za nje na kuna *Tour Operator* ndani ya Zanzibar ambao uwezo wao mdogo hawajajulikana.

a) Wizara yako kupitia wewe mwenyewe umejipanga vipi kuweza kuwainua *Tour Operator* hawa waliokuwa wana uwezo wa hali ya chini ndani ya Unguja hasa wazalendo.

b) Kwa kuwa jengo la *Museum Palace* Forodhani lipo katika hali mbaya ambayo linachakaa na haliridhishi. Je, mmejipanga vipi kuweza na jengo lile kulirekebisha kama linavyojengwa sasa hivi la Beit el Ajaib. Tunaomba utupe maelezo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mheshimiwa naomba arudie swali lake la pili sikulisikia kabisa.

Mhe. Spika: Mhe. Nadir rudia swali la pili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, swali langu la (b) nimemuuliza Mhe. Waziri kwamba Beit el Ajaib tumeona sasa hivi limepata wadhamini wanajenga. Je, *Museum Palace* mmejipanga vipi jumba lile ambalo alikuwa akikaa Mfalme mwenyewe kama sehemu yake ya kupumzika na kulala. Katika matengenezo mmejipanga serikali mtatengeneza wenyewe ama kuna wafadhili vile vile wataweza kujenga jengo lile liwe katika hali nzuri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Naomba kwanza nimwambie Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwamba *Tour Operator* katika sheria ile kuu ya *ZIPA* wanaruhusiwa *Tour Operator* wote wa aina mbili, yaani *International Tour Operator* na *Local Tour Operator*. *Tour Operator* anayetoka nje moja kwa moja kuja hapa baada ya kufanyiwa upembuzi na tukaona kwamba kuna soko la kutosha na halitoleta athari kwa *Local Tour Operators* huwa anapewa kibali na *ZIPA* baadae kuja kufuata sheria yetu.

Lakini mara nyingi katika ile sheria ya *ZIPA* wao husisitiza kwamba yule *International Tour Operator* ni muhimu sana awe ana ubia pamoja na *Local Tour Operator* ama *local person* yaani mzalendo awemo katika kampuni hiyo. Hilo ni mojawapo linalofanyika.

Sasa kwa upande wa wale *Local Tour Operators* kitu gani sisi tunafanya kuwashajihisha ama kuwasaidia, wao huwa wanapata baadhi ya mambo kwa unafuu zaidi, hata baadhi ya vibali kwao wao huwa vinakuwa nafuu zaidi. Hata wale *Tour Guides* kuna *local* na kule zile kampuni kama zile za Wataliana wanaleta *Tour Guides* wao, sio kwa kuwatembeza lakini kwa kufanya kazi hotelini, ili kuwa-*entertain* wageni wao nao huingia katika kundi hilo hilo. Kwa hiyo, wale huwa tunawapa kidogo unafuu katika mambo ya ada na mambo mengine kama hayo. Kwa hivyo hilo naomba niliweke wazi Mhe. Spika.

Lakini la pili, kuhusiana na jengo la Beit el Ajaib ni kweli jengo hili tumepata ufadhili wa Serikali ya Oman ambao hivi sasa tayari kazi hiyo ya ujenzi imeshaanza. Kuhusu jengo la *Palace Museum* tunazungumza sasa hivi na wafadhili tumeshawasilisha ripoti yetu serikalini na naamini serikali itatoa taarifa, mara tu mikataba hiyo ya *Palace Museum* itakapokamilika taarifa hiyo itawasilishwa. Ahsante.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, swali langu ni kwamba sekta hii ya utalii inaingiza takriban asilimia 80 ya fedha za kigeni zinazopatikana kupitia sekta hii. Je, katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kiasi gani cha fedha dola zilizopatikana katika kukuza uchumi wa serikali yetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mimi ningemuomba tu Mhe. Nassor Salim Ali asubiri katika ripoti ya Waziri wa Fedha na Mipango atakayokuja ile *overall* na mwelekeo wa uchumi, mle mna taarifa nzuri tu kwamba utalii umechangia kiasi gani. Lakini kwa kweli tupo kwenye asilimia mpaka sasa hivi 48. Lakini *Foreign Direct Investment* kweli maneno yako ipo zaidi ya asilimia thamanini, kama *Foreign Direct Investment* ambayo inaleta fedha za kigeni. Kwa hiyo, ripoti ile itatoa takwimu sahihi ambayo naamini itakuwa inawasilishwa mwisho kabisa katika *session* hii ya bajeti.

Nam. 63
Kufufuliwa Kiwanda cha Nguo *(COTEX)*

Mhe. Ali Saleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub)- Aliuliza:

Mnamo tarehe 5/3/2018 vyombo vya habari nchini vimeripoti mpango wa serikali kufufua upya kiwanda cha nguo cha *COTEX*.

(a) Je, mpango huo ni kweli.

(b) Kwa nini kiwanda kile kilikufa na mikakati gani inafanyika ya kufufua kiwanda hicho ili kudhibiti changamoto zilizosababisha kiwanda hicho kufa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali inaangalia uwezekano wa kutumia rasilimali za Kiwanda cha *COTEX* ili ipatikane tija zaidi kwa serikali na mmiliki wa kiwanda hicho. Mazungumzo yanaendelea kati ya serikali na mmiliki wa kiwanda hicho kuona aina muafaka ya matumizi wa rasilimali hizo kwa kuzingatia kuwa mitambo iliyokuwa ikitumika kiwandani hapo imekaa bila kutumika, imechakaa na teknolojia yenyewe imeshapitwa na wakati. Kiwanda kilisitisha uzalishaji na hatimae kufungwa katika mwaka 1991 kutokana na matatizo ya uendeshaji na kutohimili ushindani wa kibiashara.

(b) Mhe. Spika, mikakati inayoendelea kuhusu kiwanda hiki kama nilivyoeleza katika kifungu (a) cha suala hili, ni kuangalia njia muafaka ya kuzitumia rasilimali za kiwanda kwa kuzingatia mazingira ya sasa. Jambo lililo dhahiri ni kwamba mitambo mikongwe ya kiwanda haiwezi kutumika kwa ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa kama awali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, tulishuhudia hapa Zanzibar viwanda vingi na wawekezaji mbali mbali walikuwepo katika nchi yetu ili kuhakikisha kwamba serikali inapata faida, lakini na wananchi wetu wanapata ajira sehemu mbali mbali. Lakini tatizo kubwa lililofungwa kiwanda cha *COTEX* na vyenginevyo ni suala la kutokuwa na uaminifu kwa baadhi ya

wafanyakazi kujiingiza katika wizi. Tulishuhudia magodoro yanarushwa nje ya ukuta, vitambaa majora kwa majora yanarushwa nje ya ukuta.

a) Je, Mhe. Waziri, atakubalaiana na hili kwamba tatizo kubwa la uharibifu wa kutokujiamini wafanyakazi wetu kwa wizi ndio kuhatarisha viwanda vyetu.

b) Kwa kuwa mwekezaji huyo yupo, yuko wapi ndani ya nchi au nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Yeye anaamini kwamba viwanda vya Zanzibar vilikufa kutokana na wizi. Mimi naomba kumjibu kutokana na maandiko mbali mbali yaliyoandikwa na wataalam mbali mbali sababu zilizopelekea viwanda vya Zanzibar kufa moja ni kwamba malighafi hazitoki Zanzibar, na sera yetu ya Zanzibar sasa hivi kwamba kuanzisha kwa viwanda lazima malighafi ziwe zinatoka Zanzibar.

Suala la wizi inawezekana lipo inawezekana lilikuwa halipo lakini sababu kubwa iliyoandikwa na wataalam katika *reserach* tofauti ni kwamba viwanda vya Zanzibar vilikufa kutokana na malighafi za viwanda vya Zanzibar zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Hiyo ndio sababu walivyoeleza wataalam.

Lakini swali la pili mwekezaji yuko wapi. Mhe. Spika, mwekezaji huyu yuko Tanzania na bado tujue kwamba lile eneo miliki ni yake ingawaje ardhi ni mali ya Serikali, lakini jengo ni lake na bado analipia kwa mujibu wa taratibu za serikali zinavyotaka.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ningeomba kumuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo lakini asinifyatue.

a) Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri katika jibu lake mama kuwa changamoto kubwa lilikosa ushindani wa kibiashara wakati ule wa mwaka 1991 ndio maana kikafungwa. Je, serikali ina mpango gani mkakati wa kuweza kuinua na kuweza kuweka hali bora kwa mwekezaji yule.

b) Kwa kuwa ndugu zetu wa damu kule Bara sehemu za Mabibo *EPZ* wamefanikiwa sana kuweka viwanda vidogo vidogo na kuajiri zaidi ya wananchi elfu nne kufanya kazi za ushoni. Je, serikali ina mpango gani sasa wa kuweza kuleta vitu kama hivi angalau katika zile sekta za viwanda Amani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, swali lake la kwanza kwamba kiwanda kile anasema kilifungwa kunako swali mama kutokana na kilishindwa kutoa ushindani.

   Mheshimiwa ni kweli kiwanda kile kilifungwa kwa mujibu wa maelezo yetu kwamba kilishindwa na hali ya ku-*compete*. Lakini sababu kubwa nimesema kwamba kwa wakati ule viwanda vingi vya Zanzibar malighafi zilikuwa zinaagizwa kutoka nje, sasa ikiwa malighafi inaagizwa kutoka nje uzalishaji unakuwa ghali *cost* inakuwa kubwa. Kwa hivyo, kunako kuuza unakuwa huwezi kushindana kwa sababu kuna watu wengine wanazalisha kwa urahisi, sasa hii ni sababu ya kwanza.

b) Swali lake la pili anauliza Mheshimiwa kwamba wenzetu Bara wameanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vinasaidia katika kutoa ajira. Ni kweli lakini nataka aelewe na afahamu Sera ya CCM inazungumza wazi wazi kwamba kuelekea Tanzania ya Viwanda, kuelekea Zanzibar ya Viwanda.

   Mhe. Spika, naomba kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba serikali tayari imekuja na Sera ya Viwanda, tayari Rais ameshamteua Mkurugenzi Mkuu wa kuwezesha viwanda Zanzibar na sisi tayari tunakwenda katika suala zima la viwanda. Zanzibar ya Viwanda inawezekana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa nia na dhamira ya serikali zetu mbili ni kuanzisha uchumi na viwanda. Na kwa kuwa Zanzibar ilikuwa na kiwanda cha majaribio ya saruji. Je, serikali haioni mpango wa kufufua hichi kiwanda cha saruji hapa Zanzibar, wakati rasilimali kubwa ya jiwe lipo kwa wingi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anauliza kwamba Zanzibar kulikuwa na Kiwanda cha Saruji. Mimi ni mdogo kwa umri lakini sijawahi kukumbuka kuona Kiwanda cha Saruji Zanzibar, yeye ni mkubwa anaweza akakumbuka. Lakini kama kilikuwa kipo au hakipo naomba kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaelekea katika viwanda, tunatekeleza Sera ya Viwanda. Kwa maana hiyo, tunamkaribisha muwekezaji yeyote yule anayetaka kuja kuwekeza katika saruji, chokaa au jambo lolote lile *as longer* aje kuwekeza kwa kheri kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar na kwa manufaa ya uchumi wetu wa Zanzibar. Sisi tupo tayari, tutampa maeneo, tutashirikiana nae kwa sababu ndio sera yetu tunataka kuendelea. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Nashukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba Zanzibar inawezekana kuwa na viwanda na ni kweli. Mhe. Spika, Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar ni kimbilio la wafanyabiashara na wenye viwanda.

Je, Wizara yako ni lini imekaa na jumuiya hii kuwatafuta wawekezaji wa nje na ndani ili kuweka viwanda hapa Zanzibar na kuongeza pato la serikali yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli Wizara ya Biashara na Viwanda jukumu lake moja ni kuhamasishwa kuwekwa viwanda Zanzibar. Lakini jukumu la kuwatafuta wawekezaji wa viwanda ni la *Zanzibar Investment Promotion Authority (ZIPA)*. Sisi tupo tunafanya kazi yetu na tunakaa nao hiyo Jumuiya wa Wafanyabiashara Zanzibar upo chini yetu sisi na tuna Baraza la Biashara (*Business Council)* ambayo ina Katibu mtendaji, hilo ni jukumu letu na tunalifanyia kazi kikamilifu. Kama utakumbuka Zanzibar kuna utaratibu kupitia Wizara ya Biashara serikali kila mwaka kunakuwa kuna Mkutano wa Wafanyabiashara *(Business Council)* ambao unakuwa unafanyika kila mwaka. Yote hayo ni kuhakikisha kwamba Sekta nzima ya Biashara, Sekta nzima ya Viwanda Zanzibar inaendelea kwa tija na manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 236

Ujenzi wa Barabara kutoka Bububu hadi Mkokotoni

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Katika kipindi kisichopungua miezi minane (8) iliyopita, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitiliana saini mkataba wa ujenzi na Kampuni ya Ujenzi kutoka China juu ya ujenzi wa barabara ya Bububu-Mkokotoni, hatua ambayo imefurahiwa sana na wananchi wapenda maendeleo. Hata hivyo, wananchi hao wameanza kuingiwa na hofu juu ya muda wa kuanza kwa ujenzi huo.

(a) Wananchi wapenda maendeleo wangependa kujua ujenzi huo unatarajiwa kuanza lini na utaanzia sehemu gani.

(b) Ni hatua gani zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba nafasi za ajira za kazi za ujenzi wa barabara hiyo zinapewa kipaumbele kwa wananchi wa maeneo husika.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 236 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitiliana saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Bububu-Mahonda-Mkokotoni na Kampuni ya ujenzi ya *China Civil Engineering Construction Co-operation (CCECC)* kutoka nchini China ndio iliyoshinda zabuni ya ujenzi wa barabara hii tarehe 8 Novemba, 2017.

Ni kawaida kwa mikataba ya Kimataifa ya ujenzi wa barabara, baada ya kutiwa saini kuna vipengele vya mikataba lazima vitimizwe kwanza ndipo kazi iweze kuanza. Hii ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba, Muajiri kumhakikishia Mkandarasi ameleta *bank guarantee* inayoonesha kuwepo kwa fedha za kazi na kulipa malipo ya awali *(advance payment).* Baada ya kulipwa kwa malipo hayo ndipo mradi huanza rasmi.

Hivyo napenda kulieleza Baraza lako tukufu Mhe. Spika, baada ya Mkandarasi kupokea fedha za malipo ya mwanzo, kazi rasmi ilianza tarehe 01/03/2018 na kazi zenyewe ni kama zifuatazo:-

1. Kuanza kupima eneo la barabara *(Survey)* ya Bububu- Mahonda-Mkokotoni ambayo kwa mujibu wa mkataba ndio itakayoanza kujengwa.

2. Kuleta vifaa na vimeshawasili nchini.

3. Kuleta Wataalamu wa Ujenzi ambao tayari wamefika.

4. Kujenga kambi yake ambao tayari ujenzi wa kambi hiyo umeshakamilika katika Shehia ya Kandwi Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja na watu wameshakuwepo pale.

5. Mkandarasi pia ameanza kazi ya kufanya ukarabati katika sehemu ngumu zile ambazo haziwezi kupitika hususan kipindi hiki cha mvua zilizoharibika kwenye barabara hiyo ya Bububu - Mahonda - Mkokotoni.

Mhe. Spika, kwa kawaida Mkandarasi huwa anapewa kipindi cha miezi mitatu cha matayarisho wanaita *Mobilization Period* ambacho kimeanza mwezi wa Machi, 2018 na kimemalizika Mei, 2018. Kwa kuhakikisha vifaa, wataalamu, kambi, pamoja na ofisi na nyumba za msimamizi zimejengwa na kukamilika. Kazi rasmi ya ujenzi wa barabara imeshaanza. Tarehe 15/5/2018 kiongozi wa kampuni hiyo kutoka China alifika Zanzibar kuangalia maandalizi ya ujenzi huo yanakwendaje.

Mhe. Spika, kwa kawaida Wizara ikitoa kazi kwa mkataba hua na vikao mbali mbali baina ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi sambamba na kutaka ajira zote kama mtaalamu anapatikana Zanzibar apewe kipaumbele. Pia kwa zile nafasi nyengine ikiwa wapo wenye utaalamu na vigezo vinavyokidhi kazi husika kutoka maeneo ya Mikoa katika barabara ile inapopita watapewa kipaumbele, na wakikosekana watachukuliwa katika maeneo yoyote yale ya Mkoa huo, au Mikoa yoyote ya Zanzibar kwa utaratibu unaokubalika.

Mhe. Spika, hata hivyo kwa kuwa Mkandarasi ndie mwenye dhamana ya ujenzi kwa kuanzia barabara aliyokabidhiwa Bububu-Mahonda-Mkokotoni imebidi kuifanyia matengenezo katika sehemu hizo ili kusiwe na usumbufu wakati wakiwa wanajenga.

Mhe. Spika, Wizara pia itafanya vikao na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa inapopita barabara hiyo na Masheha wa Shehia zote hizo na Mshauri Elekezi wa Mradi huu kwa kutoa nasaha juu ya wananchi kuwepo tayari wanapotakiwa kuajiriwa kwa kufanya kazi hiyo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa. Baada ya pongezi hizo naomba sasa niulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kuwa chanzo cha mradi huu ilikuwa ni barabara ya Kinazini Mjini hadi Mkokotoni Unguja, lakini kwa sababu mbali mbali sasa barabara hii inatarajiwa kuanza Kwa Nyanya hadi Mkokotoni Unguja.

a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wowote angalau wa kukijenga kipande kuanzia Bububu Polisi hadi Kwa Nyanya kwa kutumia nguvu zake, ili kuondoa kero ya barabara mbovu katika eneo lile na kuwapa faraja wananchi wanaopita barabara ile.

b) Hivi sasa kampuni hii inasemekana imeshaanza kuajiri wafanyakazi, lakini baadhi ya wafanyakazi wa kampuni hiyo wanalalamika kwamba wanakatwa makato ya *ZSSF* bila ya utaratibu mzuri au fedha zao kujua kama zinapelekwa kweli kwenye shirika letu la *ZSSF*. Je, Mhe. Waziri anasemaje kuhusiana na jambo hili.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

a) Tunafahamu kwamba kipande cha barabara, barabara inaanzia huko alikoisema yeye kuendelea mpaka Mkokotoni, lakini kwa mradi huu barabara itaanzia Kwa Nyanya na kumalizikia huko. Tunafahamu kwamba baada ya mvua hizi kunyesha kuna matatizo makubwa katika barabara sehemu nyingi zimeathirika ikiwemo hiyo ya kutoka Malindi mpaka kufika Kwa Nyanya. Kazi tunayoifanya sasa hivi baada ya mvua kupungua nilifikiri mimi kwanza mvua imeshapungua lakini naona juzi usiku zimeanza kunyesha tena ni kitu ambacho kinatia wasi wasi. Tumewatuma wafanyakazi wetu wa UUB wanafanya tathmini ya kuangalia barabara zote zilizoharibika kwa mvua ili kuweza kupanga mipango ya kuona jinsi gani tutakavyoweza kuzikarabati. Kwa hivyo, hiyo kazi sio ndogo ni kubwa kwa sababu barabara ni nyingi, huku tutamaliza baadae tutafanya mpango wapi tunaanza na vipi tunamaliza.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa wasaa huu wa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake hasa ile azma ya serikali ya kuanza mradi huu kama alivyosema mwenyewe pamoja na *stretch* ya Kaskazini lakini mradi huu nao una sehemu ya barabara kuanzia Fuoni mpaka Kombeni. Sasa kipande hichi Mheshimiwa kwa kweli kimechafuka sana. Kama alivyosema hata hizo za Kaskazini alikoanza wanaanza kwa ukarabati.

Swali je, huku upande wa Fuoni mpaka Kombeni watapiga angalau ukarabati lini kwa sababu hakupitiki hata kidogo hali ni mbaya sana ya barabara. Kabla ya ule ujenzi maana yake kwa mwaka huu haielekei *contractor* kama atakuja upande ule. Je, Wizara ina mpango gani angalau nayo sehemu ile kupigwa *sop sop* kidogo, ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwanza nilisahau kumjibu Mhe. Machano Othman Said alipoulizia kuhusu *ZSSF*, hilo itabidi nimfanyie kazi na kama kuna tatizo hilo basi tutalishughulikia iwezekanavyo.

Pia napenda kumjibu Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini swali lake la kuhusu barabara ya Fuoni na kumalizikia huku kunako njia ya namba 7 Kombeni. Hii ni moja katika barabara ambazo zitajengwa na programu hii lakini kama tulivyosema kwanza inaanza hii. Kabla ya hawa Wachina kufika mimi nilitembelea barabara zote ambazo zimo katika mradi huu ikiwemo hiyo ya Fuoni-Kombeni. Wakati nilipopita ilikuwa mvua hazijanyesha na barabara ilikuwa inapitika vizuri, sasa kama mvua zimenyesha sitoshangaa kwa sababu barabara yenyewe ni ya udongo. Kama hali iko hivyo katika utathmini wa shughuli zetu tutakazozifanya nitaelekeza watendaji wangu wapite huko kuona maharibiko yako kiasi gani, ili nako tuweze kukurekebisha angalau kwa kupitisha japo *grader* katika hizo sehemu wakati tukisubiri Wachina wamalize sehemu ya huko na waje katika barabara hii.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa mara nyingi sana makampuni hapo nyuma yalikuwa yakija kuwekeza hapa Zanzibar kwa ujenzi yalikuwa yakijenga kambi za muda mfupi na kwa kuwa hapa karibuni zilipojengwa barabara za Pemba Kampuni ya H. Young ilitakiwa kujenga kambi za kudumu kiasi ambacho wakiondoka majengo yale tunayatumia.

Kwa kuwa sasa hivi umeeleza katika majibu yako kwamba kambi zimeanza kujengwa katika Shehia ya Kandwi. Je, kambi hizo ni za muda au ni za kudumu kama zile zilizokuwepo kule Pandani Pemba. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba zinapokuwa zinajengwa barabara huwa kunajengwa kambi, hata ofisi ninayokaa sasa hivi pia ilikuwa ni kambi wakati walipokuwa wanajenga barabara hii iliyotokea *round about* Mombasa kwenda Kombeni. Kambi iliyojengwa Kandwi ni kambi nzuri, nyumba zinakalika, mara nyingi huwa tunajenga kambi za kudumu na ile baada ya hapo itabakia kwa ajili ya shughuli nyengine kwa sababu hatujamaliza shughuli katika upande ule. Kwa hiyo, kipindi kijacho kama inaweza kikatumika kama kambi yetu, lakini kama haikutumika kama kambi, basi hata kwa matumizi mengine inaweza ikafaa ni suala tu la makubaliano na wale katika sehemu na wanaoitaka sehemu ile.

Mhe. Spika: Waheshimiwa kabla sijamwita muuliza swali nitoe maelezo kidogo tu. Jana Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliondosha swali Nam. 73 lakini Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba watangazaji wamekwisha kulitangaza lile swali kwa hiyo wananchi wangependa kupata majibu. Sasa kwa utaratibu Mjumbe akishakuondosha swali serikali haiwezi tena kuja kulijibu hapa, *unless* sasa Mjumbe yule alirudishe lile swali au mzungumze nae ili liweze kuletwa katika ule utaratibu wa kawaida wa kuulizwa maswali. Sasa sitoweza kuruhusu Mhe. Waziri alijibu hapa kwa sababu halikuulizwa na limeondolewa

Baada ya hapo naomba nimwite muulizaji wa swali la mwanzo la Wizara ya Afya Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Nam. 7

Kuimarisha Huduma Zinazotolewa na Wakunga wa Jadi au wa Asili

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa katika nchi yetu kuna wakunga wa jadi au wa asili wengi huko mitaani ambapo Serikali inawatambua kwa kuwapa vibali, pamoja na kuwepo kwa nyumba au vituo binafsi vinavyotambulika kusaidia uzalishaji wa watoto hapa Zanzibar.

Je, Wizara yako iko tayari kuwatafuta na kukaa pamoja na wakunga wa jadi au wa asili kwa lengo la kuwashauri na kufungua vituo hivyo rasmi ili kuendelea kuzalisha kwa usalama wa mama na mtoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Tiba Asili inawatambua Wakunga wa Jadi na iko tayari kuendelea kukaa nao pamoja kwa lengo la kuendelea kuwashauri na kuwataka waendelee kuhamasisha akina mama wajawazito kujifungua katika hospitali na vituo vya afya ili kuwa na uhakika wa kujifungua kwa njia ya usalama.

Katika mkakati wa kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga Wizara yangu haiwashauri Wakunga wa Jadi kutumia nyumba au vituo vya binafsi kutoa huduma za uzazi kwa akinamama, kwani kwa kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha ya mama na mtoto, mtoto ambaye anategemewa kuwa taifa la kesho.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu mkubwa wa suala hili kwa wananchi, hususan akinamama wajawazito. Napenda kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba, Wizara yangu kupitia Kitengo cha Tiba Asili haijasajili nyumba au kituo binafsi kwa ajili ya kutoa huduma za uzazi kwa akinamama wajawazito kupitia Wakunga wa Jadi.

Hivyo basi, tunamuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kama kuna nyumba au vituo wanavyovifahamu ambavyo vinatumika kwa kutoa huduma za uzazi kwa akinamama wajawazito kupitia Wakunga wa Jadi, tunaomba kupatiwa orodha ya nyumba na vituo hivyo, ili tuwafuatilie na tuwapatie ushauri kulingana na miongozo ya Wizara Afya katika kuanzisha huduma hizi. Lengo ni moja tu, kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Mhe. Spika, Wizara yangu inatambua na inathamini mchango mkubwa wa Wakunga wa Jadi kwa jamii na tutaendelea kufanya kazi nao, ila tunaomba wafuate taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa katika majibu yake ya msingi alisema kwamba inawatambua Wakunga wa Jadi na leo anasema anataka apatiwe orodha ya vituo. Kwa nini asitumie fursa hiyo ya kuwatambua na kuwaeleza kwamba waache mara moja kufanya vitu kama hivyo vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, hapa nimekusudia kama kuna vituo au nyumba kwa kawaida tumewafunza kwamba si ruhusa kutumia vituo vyao binafsi au nyumba zao au nyumba zozote nje ya kituo cha afya cha serikali au hospitali kutoa huduma hii.

Mhe. Spika, binaadamu ni binaadamu wanaweza wakapanga nyumba zao huko wakafanya kazi hii. Sasa tumekusudia kukwambia wewe pamoja na wananchi kama mnazifahamu nyumba au vituo wanavitumia hawa wakati sivyo tulivyo wa-*train* basi mtubainishie ili tufuatilie na tuendelee kuwashauri wasiendelee kutumia vituo hivyo kwa kuokoa maisha ya watoto na mzazi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii kuuliza swali na nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kina mama hawa wakunga wa kienyeji ni watu muhimu sana katika jamii na wanafanya kazi kubwa na nzuri.

(a) Ni utaratibu gani ambao mnautumia wa kuwapatia mafunzo ya kitaalam kila mara ili waweze kufanya kazi zao katika usaili ulio mzuri.

(b) Je, kuna vitambulisho vyovyote mnavyowapatia akinamama hawa kwa sababu tunapotoka nao wanapotoka na mgonjwa kule akifika pale hospitali anadhalilika anaonekana kama hana maana yoyote na wakati ametoka na mgonjwa huku amemleta. Je, mnawapatia vitambulisho vyovyote ili ajulikane mkunga huyu rasmi kama anawasaidia akinamama katika vijiji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, wakunga hawa huwa wanapata mafunzo maalum ambazo tunaziita semina za mara kwa mara. Lakini kuhusu vitambulisho hawa wote wana vitambulisho anapodhalilika ni yule ambaye anakwenda pale bila ya kitambulisho na anataka aingie ndani *labour* kushughulika pamoja na manesi kumzalisha mzazi, pale manaesi wetu huwa hawamruhusu. Lakini kama kenda na kitambulisho kinachomdhihirishia kwamba yeye ni mkunga ambaye kapata mafunzo yetu hakuna pingamizi wanamuingiza na wanashirikiana nae katika kumzalisha mzazi yule.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuamka salama usalmini. Mheshimiwa pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba kuna uganga huu wa kienyeji na wakati mwengine unakwenda hospitali baada ya vipimo vyote unaambiwa kwamba rudi nyumbani huonekani maradhi yako. Baada ya kurudi nyumbani ikabidi uende kwa mganga akakutibu, lakini pengine unaweza kufa kwenye uganga. Sasa je, yule anahesabiwa kama ni daktari au anashtakiwa kama kauwa.

Swali (b) ni huu uzazi wetu ambao mtu anazaa sasa tuseme hakufika hospitali lakini kuna mkunga ambaye yupo karibu. Katika uzalishaji aliombwa amzalishe yule mama kutokana na sababu zake, lakini kwa bahati mbaya mzazi pengine ama kafa, kafa mama au wakafa wote. Je, bado sheria inamkamata au nae atakuwa katika suala la kwamba aliokoa maisha kama mganga au kama daktari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa huyu ambaye hakuonekana na maradhi katika vipimo vyote vya hospitali akienda kwa mganga wa kienyeji yule anaitwa ni mganga wa kienyejio, na sisi tunatambua kwa jina la kwamba ni mganga wa kienyeji hahusiani na mambo ya hospitali. Inawezekana kipimo yeye akakiona au vipi.

Lakini kuhusu la pili, mzazi ambaye kazaa kwa bahati mbaya hakuwahi kufika hospitali na kuna mtu ambaye pengine alikuwa anamsindikiza akamsaidia na kwa bahati mtoto au mama akapoteza maisha. Huyu kibinaadamu unachukulia kwamba siku yake imeshafika hatuwezi kumshtaki kwamba kamuua au vipi, lakini zaidi naomba swali hilo ulifanye ni swali la msingi uwapelekee vyombo vya sheria wizara inayohusika nafikiri wanaweza wakalijibu kitaalamu zaidi sheria hapo inasemaje. Lakini kikwetu midhali hakufika mikononi mwetu sisi hatuhusiki nae. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 136

Jengo la Hospitali ya Wete

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Siku za hivi karibuni kumekuwa na harakati za kuwahamisha wagonjwa katika jengo la Hospitali ya Wete.

Je, kuna kitu gani kinafanyika mpaka wagonjwa wanahamishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 136 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya Mhe. Mwakilishi katika swali lake hakusema wagonjwa walihamishwa katika jengo gani la Hospitali ya Wete na kupelekwa wapi. Hivyo, imekuwa ni vigumu kidogo sisi kufuatilia na kuweza kumueleza ni kitu gani kilitokea hadi wagonjwa hao kuhamishwa kutoka sehemu moja hadi nyengine.

Hata hivyo, naomba kumjibu kwamba mara nyingi wagonjwa wenye sababu maalum katika hospitali huhamishwa na kupelekwa eneo ama hospitali nyengine kwa sababu zifuatazo:-

- Mgonjwa anapohitaji huduma za dharura (rufaa).

- Mgonjwa kuwa na maradhi ya kuambukiza ambayo yanahofiwa kuwaambukiza wagonjwa wengine.
- Mgonjwa kutopata huduma stahiki katika wodi/hospitali aliyo kutokana na ugonjwa alionao, pia kuhamishwa na kupelekwa katika hospitali inayostahili. Kwa mfano, mgonjwa ambaye amevunjika kiungo na hospitali ile iwe haina huduma hizo huwa anapewa *first aid* baadae anapelekwa katika hospitali inayohusika.
- Mgonjwa anayehitaji kupewa huduma maalum ya uangalizi wa karibu *(ICU)* pia nae huwa tunampeleka katika hospitali ambayo ina huduma hiyo.

Mhe. Spika, hizi ni baadhi tu ya sababu muhimu ambazo hutufanya kumhamisha mgonjwa kumpeleka katika wodi au hospitali nyengine kwa lengo la kupata huduma bora anazostahili kutokana na tatizo alilonalo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Spika, nimwambie tu Mhe. Naibu Waziri, wagonjwa wapo katika Hospitali ya Wete wamehamishwa mle mle ndani Wete. Wagonjwa katika Hospitali ya Wete, Jimbo la Wete wanalazimika kuhamishwa kutoka na usalama wa jengo na wizara imechukua hatua gani za dharura kukarabati jengo lile ambapo paa lake limekuwa katika hali sio nzuri kabisa na kuhamishwa. Nafikiri Naibu Waziri unatokea Wete, Mwakilishi wa Wete na hospitali iko Wete. Nafikiri utakuwa unafanya ziara.

Lakini la pili, viongozi dhamana kwa kushirikiana na wahisani wamechukua hatua gani kulihami jengo hilo akiwemo Muwakilishi na Mbunge kunusuru hali hiyo ya *drainage system*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa kumbe jawabu Mhe. Mwakilishi tayari alikuwa analo kwamba ni wagonjwa walihamishwa kwa sababu ya usalama. Sasa mimi naomba tu nikudhihirishie kwamba ni kweli inawezekana walihamishwa kwa sababu za kiusalama na sababu ni kwamba jengo lile lilikuwa ni bovu na linataka kufanyiwa ukarabati na wakahamishwa kupitia wodi moja na wodi nyengine. Swali lake angelifafanua basi ningeweza kumjibu majibu mazuri Mheshimiwa.

Lakini la pili, nikueleze kwamba jengo lile wakati wowote kuanzia sasa litajengwa na sio kwa msaada wa Mwakilishi au Mbunge, ni Serikali ndio inagharimia kujenga jengo lile. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mara nyingi sana miaka ya nyuma tulikuwa tukisema gari la wagonjwa lina *full equipment* ambazo za mgonjwa ambaye akitiwa kwenye gari anaweza akafanyiwa *service* mle labda anaingia daktari. Sasa hivi mara nyingi mahospitali yetu tukipeleka magari ya wagonjwa linakuwa ni kama *pick up* tu au ni gari liende tu kwenda kumchukua mgonjwa. Ni sababu zipi zilizofanya kwamba tusirudi tulikotoka kwamba gari la wagonjwa lina *full*

equipment kwa sababu ya mgonjwa na tukaweza kununua magari kama la kwenda kupakia kitu tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.
Mheshimiwa unasemea *ambulance,* kikawaida *ambulance* huwa mna seti mle ya kumhudumia mgonjwa anapoingizwa ili kupelekwa katika hospitali nyengine. Unasema zamani ilikuwa zinabaki mle mle sasa hazibaki mle, lakini muuguzi anapoingia na mgonjwa kumhamisha katika hopitali nyengine, basi anaingia na seti nzima ya vifaa ambavyo vitamsaidia mgonjwa akiwa kwenye *ambulance.*

Hizo *ambulance* ambazo unazikuta hazina kitu nafikiri ni zile ambazo wameleta Wabunge katika majimbo yao sina hakika, lakini nafikiri zile zitakuwa hazina *set* za kuwasaidia. Lakini *ambulance* za serikali mara nyingi huwa hazina ukiingia wewe usaidiwe upelekwe pahala fulani labda na mgonjwa wako ameshatolewa hospitali hutaikuta, lakini muuguzi akiingia na mgonjwa ambaye anamtoa Chake Chake anampeleka Hospitali ya Mkoani, basi anaingia na *kit* yake ya *set* ambayo inamhudumia mgonjwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika nikushukuru kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri yanayozunguka zunguka naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa vijiji vingi au majimbo mengi sasa yamekuwa na *ambulance* hizi lakini hamna vifaa kama ulivyosema vya kuwasaidia au *kit* au *ambu bag* za kuwasaidia wagonjwa. Je, wizara ina mpango gani kuwashajihisha kupata *kit* hizo ili wagonjwa wawe salama wanapopelekwa sehemu husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Wizara ya Afya baada ya Waheshimiwa Wabunge au Wawakilishi kubuni hii njia ya kununua *ambulance* na tunawapongeza sana kwa hatua hii ambayo wamefanya, basi wizara ilitoa elimu kwa jinsi ya kuzitumia *ambulance* zile. Sasa hii kuhusu *kit* pia walielimishwa Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi kwamba *ambulance* ili itimie kuwa ni *ambulance,* basi ni lazima iwe na seti za huduma ya kumhudumia mgonjwa anakotoka hadi afike hopitali.

Sasa kama wapo ambao hawakufanya hivyo au walifanya kwa hatua za mwanzo baadae wakawacha, mimi naomba nichukue nafasi hapa leo ili niwakumbushe tu kwamba zile *ambulance* zinahitaji ziwe na seti za kuwahudumia wagonjwa ambao wanaletwa katika hospitali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa, maswali yamemalizika nina tangazo la mgeni. Mgeni wetu wa leo ni mgeni wa Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini. Mgeni mwenyewe ni Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mbunge Jimbo la Chumbuni. Karibu sana Mheshimiwa, karibu kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Tangazo la kazi hili linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake mara baada ya kipindi cha maswali na majibu waweze kukutana chumba cha Kamati namba 3. Baada ya hapo naomba sasa Mhe. Mohamed Said Mohamed nimekuona.

Mhe. Mohamed Said Mohammed: Mhe. Spika, kwanza nishukuru sana kwa kuniona lakini nimesimama kwa kanuni ya 42 fasili ya 9 (d). Mheshimiwa naomba tu niende moja kwa moja kwa sababu ni kanuni maalum sana na watu wengi wanapenda kuitumia. Nilikuwa sitaki kuchukua muda wako ila nilitaka niombe tu kauli ya serikali.

Katika kipindi kilichopita nilileta ombi la wananchi wa Kisakasaka kuhusu huduma muhimu za pale na Mhe. Waziri wakati ule aliyekuwa akishikilia wizara ile Mhe. Hamad Rashid Mohamed alisema atalirudisha lile, ili kwa kukaa pamoja na kunipa ombi lile kulileta tena Barazani. Lakini mpaka leo sioni hata dalili ya kuletwa ombi lile nilione ili wananchi wa Kisakasaka waweze kujua ombi lao limefikia wapi.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba kauli ya serikali juu ya jambo hili, lini litaletwa au haliletwi tena ili nipate nikawajibu wananchi wale. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, nadhani serikali imelisikia hili, mimi basi niseme walichukue halafu wakishakuwa na majibu watakuja kutujibu hapa kwa faida ya watu wote. Kwa hiyo, serikali imelisikia watalifanyia kazi.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi sana kwa Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa taasisi zote za wizara.

Pili pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake katika kuimairisha Sekta ya Maji, Umeme na Nishati.

Naipongeza *ZURA* kwa utekelezaji wa majukumu. Napongeza sana kipindi cha kuelimisha wananchi changamoto na ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, mafuta ya taa kuadimika mara kwa mara. Baadhi ya makampuni hivi sasa hawaagizii mafuta haya wananchi wanapata usumbufu mkubwa. Naomba hili walizingatie.

Lakini pia, tumeshashuhudia upungufu wa *petrol* na *diesel* katika vipindi tofauti. Mhe. Mwenyekiti, hili ni kero na inarejesha nyumba maendeleo ya uchumi wa wananchi na taifa. Ni vyema *ZURA* iandae mpango maalum.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu naipongeza sana *ZAWA* katika kuleta mapinduzi makubwa ya kudumu ya maji. Nampongeze sana Mkurugenzi Mkuu *ZAWA* kwa weledi, uwajibikaji, ubunifu na usimamizi mzuri. Hivi sasa kero ya maji inapungua kidogo na juhudi tunaziona. Napongeza ubunifu wa kipindi cha *ZAWA* katika *ZBC*. Hongera sana.

Ushauri wangu jitihada iendelee miradi ya maji iliyopangwa ili sisi viongozi wa majimbo tupungukiwe na gharama za maji. Kwa kweli, katika Jimbo langu la Magomeni naomba *ZAWA* kutupia macho sana kisima cha maji alichochimba Mhe. Turki pale kwa Bintiamrani, wapo baadhi ya watendaji wastaafu wa *ZAWA* wanachangia tatizo katika kisima kile. Kitendo hicho kinawakosesha amani wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni hususan katika Shehia ya Meya.

Kwa hiyo, katika eneo hili lina changamoto mbali mbali. Changamoto hizo ni pamoja na kukiukwa taratibu za ukodishwaji linazalisha migogoro kwa wawekezaji na wananchi wa maeneo husika. Vile vile, kuna wawekezaji wengi wazalendo na wageni wamezuiwa na maeneo mengi na makubwa kwa muda mrefu lakini kinachoendelea na serikali inakosa mapato. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri hili lishughulikiwe.

Naipongeza wizara kwa juhudi zake za kupambana na migogoro ya ardhi. Lakini bado kazi pevu ipo mbele yetu. Kuna migogoro mingi ambayo haijapatiwa ufumbuzi. Mfano Mgogoro wa wananchi wa Kajengwa Makunduchi katika eneo la Ras Shungi lililojengwa hoteli na muekezaji mzalendo ambaye na yeye amekwisha liuza kwa wageni na kulihaulisha kinyume na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mgogoro huu unafukuta, naomba waite wananachi wote wake wa Kajengwa Makunduchi ambao tayari wameshaleta barua ya malalamiko.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza tena wajitahidi zaidi, hii ni wizara ngumu na nyeti. Ni wizara yenye kuhitaji uadilifu mkubwa kwani hivi sasa ardhi ndio rasilimali iliyobakia. Kila mtu anataka kujilimbikizia ardhi. Anasahau kuwa iko siku ardhi hiyo itambana. Naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kutekeleza majukumu yake vizuri na kuwa makini sana. Naipongeza programu ndogo ya utawala wa ardhi katika utekelezaji wa utayarishaji wa hati za haki ya matumizi ya ardhi hati 794 ambazo zimeandaliwa kati ya hati 718 za kudumu na hati 76 ni za muda.

Lakini pia niombe watendaji na Mhe. Waziri kuwa makini kwa wale mnaowapatia hati hizo kuwa wengi wao wasiwe wageni ikawa ardhi yetu kuigawa kwa wageni hatimayake ikaja kutuletea matatizo hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, bado serikali inahitajika kuendelea kutoa elimu kwa usajili wa ardhi za mirathi na wakfu kwani elimu ni ndogo sana na hasa ukizingatia matatizo haya huwafika sana wanawake na watoto ndio hukosa haki hizo. Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake walizingatie sana hilo.

Mhe. Naibu Spika, mamlaka hii ina kazi ngumu sana hasa katika utatuzi wa changamoto ya maji safi na salama. Pamoja na jitihada kubwa inazozifanya kuitatua changamoto hii lakini bado imeshindikana na hasa ukizingatia kwenye miji na katika vyanzo vya maji ya kudumu yamekuwa ni makazi ya watu. Tunatakiwa tusaidiane kutoa elimu kwa wananchi wetu. Ahsante sana naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Mohd Mgaza Jecha: Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi Nyumba, Maji Na Nishati, pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana utekelezaji wa wa kazi za wizara kwa niaba ya wananchi wetu wa Zanzibar. Pamoja na pongezi hizi na naomba kuuliza kuhusu tangi la wananchi wa Mtambile hatua gani iliyofikiwa.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia kwa mia moja.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto ya ucheleweshaji wa upatikanaji wa viwanja.

Vile vile, kuhusu sekta ya maji changamoto ni mashine kwenye visima. Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, naiomba wizara iwaongezee vifaa watendaji, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, huo ndio mchango wangu.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, kwanza nashauri tuletewe kwa kufanyiwa semina Barazani. Suala la Sera ya Ardhi, pawepo na *Land Use Plan* ya nchi nzima, ili kutenga maeneo maalum ya ujenzi, kilimo ufugaji na maeneo ya hifadhi.

Ufafanuzi wa matumizi ya ardhi uwe imara kwa kusimamia sheria.

Programu Kuu PNO105 Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati. Hii programu ni kubwa sana kuwekwa pamoja huduma za maji na nishati.

Mhe. Spika, ushauri wangu kuwe na programu pekee kwa maji na nyengine kwa ajili ya nishati.

Vile vile, kuhusu suala la maji Dimani kilio kikubwa cha watu wa Dimani ni ubovu wa tangi la maji Dimani. Nashauri ahadi iliyotolewa na *ZAWA* ya kulikarabati tangi la Dimani wiki mbili itatekelezwa.

Pia turejeshewe *pump* iliyoibiwa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati pamoja na Naibu Waziri kwa kuendelea na jitihada yao kubwa ya kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutatua matatizo ya wananchi wa Zanzibar pamoja na mambo katika sekta ya jamii.

Pia nawapongeza kwa kuteuliwa kwao tena kwa kuongoza wizara hiyo kwa mara nyengine tena. Hali hii inaonesha namna gani Mhe. Rais alivyothamini utendaji wao wa kazi kabla ya kuapishwa kwa mara ya pili kuiongoza wizara hiyo.

Programu Ndogo ya Utatuzi wa Migogoro ya ardhi:-

Jambo la kwanza elimu kwa jamii inayohusiana na shughuli za mahakama ya ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi ni vyema elimu hiyo ikatolewa mara kwa mara kwa wananchi, ili migogoro ya ardhi ikaweza kupungua au kumalizika kabisa. Elimu kupitia programu ya semina ni vyema pia ikaweza kutumika mjini hadi vijijini, elimu hiyo pia ijumuishe matumizi sahihi ya ardhi.

Vile vile, kuhusu kupitia na kuifanyia marekebisho Sheria namba 4/2010 hili ni jambo jema. Ni vyema wizara ikaharakisha zoezi hilo ili Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe iweze kuwa na sheria nzuri zaidi na yenye kwenda na wakati.

Naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi na kuweza kusema niliyonayo au niliyoyaona.

Vile vile, nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano ya kukaa pamoja na kuyaandaa haya mliotuletea ndani ya hotuba, ninakushukuru sana.

Mhe. Spika, naanza na habari ya mafuta ndani ya sheli za hapa mjini kumejitokeza changamoto zinazotokea wakati pale tu mafuta yanapoadimika ndani ya hizo sheli. Lakini chakushangaza mafuta hayo wanapewa watu pale pembeni kwa bei ya juu, ukienda pale unaitwa mafuta ninayo. Kutokana na hali hiyo, wizara inachukuwa hatua gani dhidi ya watu wanaofanya hivyo kuwapa shida wananchi kwa kuwalanguwa bei zisizo kuwa za kisheria.

Mhe. Spika, hayo mashirika yanayoleta mafuta tatizo hilo naomba wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi kwa nini wanafanya hivyo kuipaka serikali hii matope linauma sana wanyonge hawana uwezo wa kupata, naomba majibu.

Kwa kweli, Mhe. Waziri nimesema sana kuhusu masuala ya maji ndani ya Mkoa wa mjini ni kweli visima vipo vingi lakini maji ndani ya shehia zetu hatuna inafika hata miaka mitatu hayatoki. Nakuomba sana Mhe. Waziri watendaji wako hawapiti kuangalia baazi ya mitaa wananchi walio wengi wanasaidiwa na visima vilivyochimbwa na Waheshimiwa wetu wa Majimbo siyo ya *ZAWA*. Nakuomba sana ulifanyie kazi wanawake wanateseka sana wewe ndio wanawake unajua shida na umuhimu wa maji.

Mhe. Spika, tunaomba msaada na ninashukuru sana sina haja ya kuzuia fungu bali naomba majibu ya kutosheleza, ili wanawake wa Mkoa wa Mjini waondokane na shida hii ya miaka mingi.

Kwa hiyo, namshukuru sana Mhe. Waziri naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Naomba majibu ili wanawake waridhike na majibu utakayonipa.

Mwisho, pongezi kwa Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi wote ndani ya wizara hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza naomba nizungumzie kuhusu suala la ucheleweshwaji wa hatimiliki baada ya watu wanapouziana nyumba. Kwa kweli, jambo hili ni vyema tukalitolea ufafanuzi, kwa sababu yapo manunguniko mengi mitaani ambayo zaidi ya mwaka mmoja, miwili na na kadhalika. Mhe. Spika, naomba kama ikiwa ni utaratibu basi ni vyema tutoe elimu wananchi wetu wawe na uwelewa ili kusudi wasiipake matope serikali.

Vile vile, kuhusu Shirika la Nyumba kuweka nyumba za vijiji zilizojengwa na Mzee wetu Abeid Aman Karume baada ya Mapinduzi. Nyumba zilizo vijijini mpaka sasa kuna baadhi ya nyumba hakuna fedha inayopatikana kwa ukodishwaji na ulikuwepo mpango wa serikali kwa kuuza nyumba zile kwa sasa nyumba zimechakaa sana chafu, maji, umeme na zinavuja, wanaoishi wamekuwa wakiishi hawana vya kufanya tu.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kama Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilivyoeleza kuhusu kuuza nyumba kwa bei nafuu wananchi waweze kuwasaidia. Ili kuepuka migongano na ukaribu na uharakwishaji wa utapitakanaji wa huduma. Kwa hivyo, ni vyema sasa wawepo watendaji Afisi ya Wilaya akiwemo Afisa wa *ZECO* ngazi hii na awe na Afisi katika Wilaya wananchi wamekuwa wakisumbuka kwa kutafuta huduma za umeme masafa marefu.

Suala la upatikanaji huduma za umeme, ukweli watendaji wamekuwa wakijitahidi sawa ila naomba miradi ya upelekaji wa huduma za umeme vijijini, Micheweni takribani shehia zote zimeshafikiwa na huduma ya umeme.

Lakini kutokana na mafanikio ya upatikanaji wa huduma hii sasa ongezeko la watu wanaohitaji katika vijiji vipya kumekuwa na mahitaji zaidi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tuendelee kushirikiana pamoja na kunipatia fursa ya kusambaza umeme katika jimbo langu la Micheweni.

Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba hii, hotuba imekidhi mahitaji yote.

Nawapongeza wafanyakazi wa wizara hii kwa mashirikiano mazuri waliyonayo baina yao na wananchi ambao ndio watumiaji wakuu wa ardhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwa wananchi wasimamiwe wanapohitaji kujenga nyumba za kuishi ili wajenge kwa kufuata *plan* za mipango ya miji, ili iwe rahisi kupitisha gari baina ya nyumba na nyumba au mtaa kwa mtaa, kwa kweli jambo hili ni hadhari ya kujikinga na majanga yanapotokea ikiwemo janga la mto ili kuruhusu miundombinu ya kupitisha gari la *fire*, gari za wagonjwa na kadhalika.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Mhe. Spika, je vipi kuhusu tangi la maji Mtambile.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu Idara ya Nyumba kuna nyumba iliyoanguka huko Pemba nitahitaji maelezo kwa bei kubwa iliyopo aliyopewa ya kuuziwa shilingi 88,000/= nyumba iko chini na yeye ndio mwenyewe na nyumba yenyewe imeshaanguka nina ghofu nahitaji maelezo.

Mhe. Spika, nazuia fungu PN0103.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote. Naomba nichangie kwa ufupi.

Mhe. Spika, iko haja ya kubadilisha miundombinu ya maji kwa kuchimba visima ambavyo havina gharama kubwa kama wanaochimba wananchi wenyewe.

Vile vile, nakumbusha visima vya Ras-al-Khaimah Ukutini Ngwachani. Nashukuru sana kinaendelea kufanyiwa matengenezo.

Mwisho, nimalizie kuhusu umeme Mtengombe nakumbusha na pia hali itakaporuhusu basi naomba katika kijiji cha Shangani, Chambani basi na wao wapatiwe huduma hii.

Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi wanazozichukuwa katika kutatua changamoto za wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Shirika la Umeme *ZECO*, namuomba Mhe. Waziri katika jimbo langu la Fuoni kipo kijiji cha Fuoni Birikani hakuna umeme hadi leo hii. Kwa hivyo, katika bajeti ya mwaka 2018/19 naomba afanye juhudi ili kijiji hicho kipate umeme na sisi viongozi wa jimbo tupo tayari kusaidiana ili kufanikisha lengo hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Maji *ZAWA* kwa wananchi wengi wa Jimbo la Fuoni hawapati maji, na kwa kuwa vipo visima vya Ras-al-Khaimah ambavyo havijamaliza. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri afanye maarifa yale ili tupatiwe kumaliziwe kisima japo kimoja kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *ZURA* kwa kuwa utafiti wa mafuta na gesi umefanyika kwa kipindi sasa ni yepi matokeo ya utafiti huo.

Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa utendaji wake pamoja na Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wote. Nimpongeze zaidi Mkurugenzi Mkuu *ZAWA* muda mfupi aliochaguliwa tunaona utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kwenye suala la maji naomba kutoa ushauri kwa juhudi zilizochukuliwa na wizara baada ya kilio kikubwa cha visima vya Ras-al-Khaimah vilivyomo katika jimbo langu sasa limepatiwa ufumbuzi kibanda tayari kimeshajengwa, umeme tayari naamini zoezi hili litakamilika. Mhe. Waziri kwa kazi kubwa anayofanya Mkurugenzi huyu naamini na kisima kilichobaki kitatengenezwa na wananchi kuondokana na tatizo la maji.

Vile vile, kuna wafanyakazi wanaojitolea kulinda na kufungua maji hawana mishahara, naiomba serikali iwaone wafanyakazi hawa ili waweze kujitegemea na familia zao. Kwa kweli, naipongeza wizara kwa kusambaza umeme maeneo ya vijijini, lakini bado tatizo la umeme lipo. Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara pahala panapohitaji nguzo 3 na kuendelea Waheshimiwa Wawakilishi wachangie nguzo 1 huduma zilizobakia wizara imalize.

Kuhusu suala la ujenzi holela Idara ya Mipango Miji ipo haja ya kutenga maeneo maalum ya kujenga wananchi, ili kuondokana na tatizo hili la ujenzi holela. Kwa mfano, kuna ujenzi mbele ya Skuli ya Nyuki hizo mita zinazotakiwa na watu wa barabara hazikufikiwa. Je, *DCU* iko wapi. Hawaoni au tunasubiri ujenzi umalizike tuwaambie wavunje.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie.

Mwisho nawapongeza tena nyote naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Juma Ali Khatib: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, naunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja. Lakini naomba kutoa ushauri tuongezee bidii kubwa kwenye kuweka miundombinu ya maji ili kuondoa tatizo la maji. Pia naomba tuongeze umakini wakati wa kununua *pump* za maji tuchaguwe zenye ubora ili zidumu muda mrefu. Ahsante naunga mkono.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwepo leo. Napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hekima na busara katika kupanga safu yake ya uongozi, ili kutekeleza kikamilifu maendeleo ya nchi za Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati na Katibu Mkuu Ali Khalil Miraz na watendaji wenzake wote wa wizara. Mhe. Naibu Spika, nikupongeze wewe na afisi zenu zote kwa ushirikiano wanaotupa siku hadi siku.

Baada ya shukurani hizo zote na mimi naomba nichangie yafuatayo:

Kuendelea kutambua juhudi kubwa zinazofanywa na wizara hii katika maeneo yote ya ardhi. Hivi sasa watu wanaendelea kujenga kufuata utaratibu wa majenzi baada ya maendeleo mazuri ya wizara hasa katika makaazi mapya.

Elimu ya wafanyakazi inaendelea kuongezwa katika ukurasa wa 21.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza suala hili la maji linagusa wanawake na watoto kwa kweli kupitia wizara hii nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuhakikisha kuwa miradi yote ya maji inasimamiwa vizuri, ili watu wote wafaidi maisha bora. *ZAWA* na *ZECO* kwani maji na umeme viko sambamba.

Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo ni muhimu kwetu sisi pale ambapo tunaona vitu vinahisabiwa na watu wachache wasiopenda maendeleo, uharibifu unapotokea tukemee, mali ya serikali yetu sote.

Aidha, ni pongezi juhudi za utafiti wa mafuta na gesi kila mtu anajua neema hiyo ikipatikana basi tutaongea lugha nyingine na maendeleo ya kisasa. Mhe. Naibu Spika, haya mengi mazuri yamechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe walio tangulia.

Kwa hivyo, napenda niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kuunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri, ili bajeti ipite bila mabuti na kama alivyoomba apewe kwa asilimia mia.

Mhe. Naibu Spika, asilimia mia ahsante na ubarikiwe. Naendelea kuwatakia afya katika ibada zinazoendelea za kufunga.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa, naomba sasa kwa heshima na taadhima nianze kumwita mchangiaji wetu wa mwisho Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ili aweze kuchangia. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia uhai na uzima kwa kuweza kuendelea na majukumu yetu katika Baraza lako Tukufu.

Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe walitoa hoja nyingi nitajaribu katika mchango wangu kutoa baadhi ya maelezo na baadhi ya hoja hizo na kwanza nianze na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira.

Mhe. Mohamed Said Mohamed alitaka kujua mapato ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka 2018/2019 yamepelekwa wapi kwani kwenye kitabu kikubwa cha Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati hakuna kitu ambapo yanaonekana.

Mhe. Spika, ni kwamba kama inavyofahamika kuwa shughuli ya usimamizi wa mazingira zimehamishiwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hivyo mapato ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kwa mwaka 2018/2019 yamehamishiwa ofisi hiyo ambapo jumla ya shilingi 81,000,000/- za Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka 2018/2019 imepangiwa kukusanya.

Mhe. Spika, niende sasa kwa upande wa Mahakama ya Ardhi, nianze na Mhe. Khamis Juma Maalim alishauri kwamba Mahakama ya Ardhi ni vyema kutoa elimu kwa wananchi mara kwa mara ili kuweza kupunguza au kumaliza kabisa kwa migogoro ya ardhi.

Mhe. Spika, ni kwamba Mahakama ya Ardhi itaendelea kutoa elimu kuhusu migogoro ya ardhi kupitia mikutano mbali mbali ya masheha, semina na kupitia vyombo vya habari. Lakini pia alikuwepo Mhe. Suleiman Makame Ali, alihoji inakuwaje Mahakama ya Ardhi inatoa nyaraka mbili katika ardhi moja.

Mhe. Spika, ni kwamba kazi kubwa ya Mahakama ya Ardhi ni kutatua migogoro ya ardhi inayowasilishwa Mahakamani na haihusiki kabisa na utoaji wa hati yoyote ya umiliki wa ardhi, isipokuwa kwa kesi hii ambayo Mheshimiwa kaieleza ni kwamba Kamisheni ya Ardhi itairejesha eneo lile serikalini.

Mhe. Rashid Makame Shamsi aliipongeza wizara kwa juhudi zake za kupunguza migogoro ya ardhi, lakini pia anatambua kazi kubwa ambayo tunaifanya kwa kutatua migogoro ya ardhi. Pia akaitaka Mahakama ya Ardhi kuongeza bidii katika kutatua migogoro hiyo.

Mhe. Spika, ni kwamba pongezi tumezipokea na kwa sasa migogoro mingi iliyowasilishwa Mahakama ya Ardhi imeshapatiwa ufumbuzi pamoja na changamoto ndogo ndogo ambazo watendaji wa Mahakama wanakabiliana nazo. Binafsi nakubaliana na mchango wa Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara hii ni ngumu na nyeti, ni wizara yenye kuhitaji uadilifu mkubwa kwani hivi sasa ardhi ndio rasilimali iliyobakia.

Mhe. Spika, niende kwa upande wa Shirika la Nyumba Zanzibar, nianze na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alieleza kwamba wapo watendaji wawili wa Shirika la Nyumba wanafanya utapeli wananyang'anya watu nyumba kwa njia ya vilemba na watumishi hao wamechukuliwa hatua gani. Na aliuliza je, na hao walionyang'anywa nyumba utatumika utaratibu gani kwa kurejeshewa nyumba hiyo.

Mhe. Spika, ni kwamba hatua iliyochukuliwa kwa watuhumiwa hawa waliohusika na utapeli huo kesi yao imepelekwa katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi *(ZAECA),* lakini huyu mtu aliyedai kuwa katapeliwa nae aliipata nyumba hiyo kwa njia zisizo halali na baadae akataka kuiuza kwa njia za kilemba ndio maana shirika ni kuichukua na kuipangia matumizi mengine nyumba hiyo.

Lakini Mhe. Mussa Foum Mussa alieleza kuhusu nyumba za Kengeja ambazo wananchi wamepewa fidia na zipo katika hali mbaya na wananchi wanaoishi katika nyumba hizo ni wanyonge hawawezi kuzifanyia matengenezo.

Lakini pia alishauri zifanyiwe matengenezo na serikali na Mhe. Waziri aliombwa azitembelee nyumba hizo. Ni kwamba suala hili tumelipokea na serikali imeanza kufanya tathmini ya nyumba hizo. Shirika la Nyumba kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo wataishauri Serikali juu ya matengenezo ya nyumba hizo baada ya tathmini. Sambamba na Mhe. Mohamed Said Mohamed katika nyumba zile za

Kilimani. Lakini ushauri tumeupokea wa kuzifanyia matengenezo nyumba hizo, halikadhalika Mhe. Waziri atapata nafasi ya kutembelea nyumba hizo.

Mhe. Shamata Shaame Khamis kasema kuhusu Shirika la Nyumba kumekuwepo na nyumba za vijiji zilizojengwa na Mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume baada ya Mapinduzi. Nyumba zilizoko vijijini mpaka sasa kuna baadhi ya nyumba hakuna fedha inayopatikana kwa ukodishwaji na ulikuwepo mpango wa serikali wa kuuza nyumba zile kwa sasa nyumba zimechakaa, chafu, hazina maji, zinavuja na wanaoishi humo hawana tu la kufanya ndio maana wanaishi. Lakini pia alishauri kama ilani yetu ya chama ilivyoeleza kuhusu kuuza nyumba kwa bei nafuu ili ziweze kuwasaidia wananchi. Ni kweli kwamba nyumba za vijiji nyingi zimechakaa lakini kwa sasa serikali imesitisha uuzaji wa nyumba hizo.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Paje alieleza kuhusu Idara ya Nyumba kuna nyumba iliyoanguka huko Pemba akahitaji maelezo na kwa bei kubwa aliyopewa ya kuuzwa shilingi milioni 88,000,000 nyumba yake iko chini na yeye ndie mwenyewe, imeshanguka na ni gofu tu anahitaji maelezo.

Mhe. Spika, ni kwamba nyumba hiyo hivi sasa iko chini ya miliki ya serikali baada ya kutaifishwa. Aidha, bei hiyo ilitiwa na watathmini wa serikali kama utaratibu ulivyo. Kwa vile suala hili ndio kwanza nalipokea namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub atuachie ili tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, sasa nielekeze Mji Mkongwe naanza na Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa alieleza kuhusu Uhifadhi wa Mji Mkongwe na kuomba Mhe. Waziri nchi za wenzetu walioendelea Mji Mkongwe unakuwa ndani ya Manispaa. Anashauri ili tupate kubadilisha mji pia twende na wakati kama nchi za wenzetu walio na Mji Mkongwe kama wa kwetu.

Mhe. Spika, sababu ya Mamlaka ya Mji Mkongwe kuundwa tofauti na Manispaa hii inatokana na sababu za kitaalamu kufuatia ukaguzi uliofanyika mwaka 1982 na *UN Habitant* ni kutokana na maombi ya serikali. Ningependekeza kuundwa kwa taasisi ya kipekee inakayoshughulikia Uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao utakuwa na utaalamu wa kuhifadhi na urithi. Hii ilitokana na kuanguka kwa majengo ya kihistoria na kujengwa majengo ya kisasa kulikopelekea kupunguza uasili wake. Mbali na Mji Mkongwe wa Zanzibar taasisi kama hizi zipo baadhi ya nchi kama *Tunisia, Ihla de Mozambique* na kadhalika.

Lakini pia Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Paje aliendelea kwa kuuliza wale waliokuwa na vipenu vya duka katika jengo la *Tall Building* (Jengo la Treni) na wakati wa matengenezo ikiwa vimeondoka. Suala hili la ugawaji liko *ZSSF* kwa upande wa mamlaka inajua wale waliokuwa wakitumia Jengo la Treni kwa mujibu wa utaratibu waliorodheshwa wote na wote watapata haki zao kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Lakini Mhe. Khamis Juma Maalim alisema kuhusu kupitia na kufanyiwa marekebisho Sheria Nam. 4 ya mwaka 2010. Ni jambo jema, ni vyema wizara ikaharakisha zoezi hilo ili Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe iweze kuwa na sheria nzuri zaidi na inayokwenda na wakati. Tuseme kwamba wizara imepokea ushauri na itazidisha jitihada za kufanikisha zoezi hilo.

Mhe. Spika, sasa nigusie kwa upande wa Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* nianze na Mhe. Yussuf Hassan Iddi kasema kupatiwa umeme kijiji cha Fuoni Birikani. Mhe. Spika, ni kwamba kijiji hichi kipo katika mpango wa kupatiwa umeme kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa upande wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub alieleza tatizo la umeme mdogo Kinuni Miti Barafu na Mwera Minanasini. Mhe. Spika, ni kwamba huduma za umeme katika maeneo hayo zitaimarishwa katika Mpango wa Bajeti wa 2018/2019 na hii inatokana na *line* kuzidiwa na mahitaji ya wananchi.

Lakini pia alielezea tatizo la kukatika umeme katika eneo la Jambiani. Naomba niseme kwamba tatizo hilo linasababishwa na matengenezo ya kuimarisha miundo mbinu na njia za umeme katika maeneo ya Kusini, punde tu baada ya kumalizika kwa kazi hiyo basi huduma itatengemaa kama kawaida.

Lakini Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf walisema kwamba wananchi na wawakilishi ni vyema wasaidiwe nguzo za umeme katika maeneo yao. Mhe. Spika, niseme kwamba serikali itawasaidia wananchi nguzo kila itakapopata uwezo wa fedha.

Lakini Mhe. Bahati Khamis Kombo amekumbusha upelekaji wa umeme katika kijiji cha Mteng'ombe na Shangini Chambani. Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kazi za upelekaji wa huduma ya umeme kwa kijiji cha Mteng'ombe utafanyika ndani ya mwaka huu wa 2018 na kwa upande wa kijiji cha Shangini Chambani tayari kimeingizwa kwenye mpango wa 2020.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alielezea kuhusu wananchi kulipia gharama kubwa ya kuunganishiwa huduma ya umeme. Mhe. Spika, ni kwamba serikali inatumia fedha nyingi kununua vifaa na nyenzo za kuwaunganishia umeme wananchi, gharama hizo zingeweza kuingizwa katika bei ya umeme. Hata hivyo, kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wa bei wananchi, serikali imeweka utaratibu wa wananchi kuchangia gharama hizo wakati wa kuunganishiwa huduma hiyo. Kwa wasiokuwa na uwezo wanaunganishiwa umeme kwa njia ya mkopo, mteja kulipia gharama za kuunganisha umeme ndio utaratibu unaotumiwa na mashirika ya umeme duniani kote.

Mhe. Omar Seif Abeid alieleza kuhusiana na deni la taasisi ya serikali kwa *ZECO* na kuzitaka wizara zilipe madeni yake. Mhe. Spika, naungana na Mhe. Mwakilishi kuhimiza taasisi na wizara zote kuhakikisha zinalipia madeni yao ya huduma wanazozipata za umeme.

Mhe. Mussa Foum Mussa aliomba baadhi ya vijiji ambavyo havijafikishiwa umeme ikiwemo vijiji vya Mitondooni, Mtakatu, Mchapwe na Mivumoni vipatiwe huduma hiyo. Ni kwamba vijiji ambavyo havijafikishiwa umeme vitapatiwa umeme kama ifuatavyo.

Mtondooni mwaka 2018 panapomajaaliwa watapatiwa huduma hiyo, Mtakatu mwaka 2020 panapo majaaliwa, Mchapwe mwaka 2021 na Mivumoni mwaka 2020. Mhe. Shamata Shaame Khamis alishauri kuwa ni vyema *ZECO* ikaweka watendaji katika ngazi za Wilaya ili kuwaondolea usumbufu wananchi kwa kufuata huduma mjini.

Mhe. Spika, ni kwamba shirika limeshafungua ofisi zake za kanda kwa Unguja kule Gamba na Makunduchi na Pemba Mkoani na Wete zinatoa huduma. Aidha, maeneo ya Dunga kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba yanatarajia kufunguliwa huduma kama hizo ndani ya mwaka huu wa fedha yaani 2018/2019. Lakini pia Mheshimiwa aliendelea kuiomba serikali kusambaza umeme katika vijiji vipya vya Micheweni. Mhe. Spika, ni kwamba ombi lake tumelipokea na naomba Mhe. Mwakilishi aelewe kuwa ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inamfikia kila mwananchi popote alipo.

Mhe. Ame Haji Ali wa Jimbo la Nungwi aliomba kusambaziwa umeme katika vijiji vya Mgogoni, Mchangamle, Kibwengo na Kidagoni vilivyopo katika Jimbo la Nungwi. Mhe. Spika, kama ambavyo tumefanya kule na kwa Nungwi vijiji hivi vitapata huduma hiyo kama ifuatayo. Mgogoni atustahamilie mpaka 2021, Mchangamle 2020, Kibwengo 2020 na Kidagoni 2020 watapata umeme pale.

Mhe. Spika, tuendelee na Mhe. Machano Othman Said alitaka Wizara kupitia Shirika la Umeme kuboresha huduma ya umeme kwenye maeneo yenye umeme mdogo kwenye Jimbo la Mfenesini. Ni kwamba wizara kupitia Shirika la Umeme itaendelea kuboresha huduma za umeme kwenye maeneo yanayopata umeme mdogo katika Mpango wa Bajeti wa mwaka huu 2018/2019. Lakini pia aliendelea kuiomba wizara kuanzisha kitengo kitakachoshughulikia usambazaji wa umeme katika vijiji kama ilivyo *REYA* kwa Tanzania Bara. Ombi lake limepokewa na naomba Mhe. Mwakilishi aelewe kuwa shirika limekuwa likitoa fedha za kupeleka umeme vijijini kwa kila mwaka kama ambavyo Tanzania Bara wamekuwa wakifanya kupitia *REYA*.

Mhe. Hidaya Ali Makame ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Hidaya Ali Makame alitaka wizara kutoa taarifa za kutosha kwa wananchi wakati wa kubadilisha mita za TUKUZA. Ni kwamba shirika huwa linatoa taarifa za ubadilishaji wa mita za TUKUZA kupitia kwa Masheha wa Shehia husika. Hata hivyo, shirika litaongeza utaratibu wa kutoa taarifa hizo kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Said Soud Said ametaka wafanyakazi wa Shirika la Umeme kupatiwa vitendea kazi. Ni kwamba Serikali kupitia Shirika la Umeme linafanya jitihada za makusudi kukamilisha mahitaji ya nyenzo za kazi kwa wafanyakazi wote.
Mhe. Mohamed Said Mohamed ametaka kujua ubadilishaji wa nguzo mbovu za umeme na matokeo ya dharura yanachukua muda gani kufanyiwa kazi. Ni kwamba matukio yote ya dharura hufanyiwa kazi kwa kupata kipaumbele baada ya tathmini ya athari kutegemea na mazingira ya tukio kwa tukio. Katika hali hii shirika linajitahidi kutatua ndani ya muda mfupi kadri inavyowezekana ambapo kila siku nguzo mbovu zinahitaji kubadilishwa zinabadilishwa.

Lakini Mhe. Suleiman Makame Ali ametaka wananchi kubadilishiwa mita za zamani na kuwekewa TUKUZA bila ya malipo. Shirika linatumia fedha nyingi kununua mita za TUKUZA hivyo inawajibika kuweka utaratibu kwa wananchi

kuchangia wakati wa ubadilishaji wa mita za kawaida ambazo thamani yake ni ndogo mno ukilinganisha na mita za TUKUZA.

Mhe. Spika, wa mwisho kwa upande huu wa *ZECO* ni Mhe. Khadija Omar Kibano ambaye ametaka kujua ni lini Shirika la Umeme litafikisha nguzo zilizobakia katika kijiji cha Mkanjuni.
Mhe. Spika, ni kwamba shirika limeshaanza kufanya kazi hiyo na nguzo zilizobakia zitakamilishwa katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nimalizie kwa upande wa kuchangia pango kwa upande wa Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* kama muda utaruhusu. Nianze na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano, Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini pia Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Masoud Abrahman Masoud na Mhe. Asha Abdalla Mussa walipongeza na kukumbusha na kuhakikisha uendelezaji wa visima vyote vilivyochimbwa na Ras Al Khaimah, na Mhe. Machano Othman Said pia alizungumzia hilo.

Mhe. Spika, ni kwamba visima vyote ni 150 vilivyoendelezwa na kutoa huduma hadi sasa ni 33. Serikali kupitia *ZAWA* inaendelea na jitihada za kuviendeleza visima hivyo. Lakini ndani ya 2018/2019 visima 20 ambavyo vinategemea tutumie bilioni nne inategemea kuendelezwa na itaendelea kuviendeleza vyengine kadri uwezo wa serikali pamoja na *ZAWA* utakavyoruhusu.

Mhe. Hamza Hassan Juma aliendelea kusema kwamba *ZAWA* kuhakikisha wanakamilisha mchakato wa upatikanaji wa pesa za Mradi wa India. Mhe. Spika, Mradi wa India unaendelea vizuri ambapo Mshauri Elekezi anakamilisha ripoti ya usanifu wa mradi. Fedha za mradi huu tayari zimeanza kulipwa na zitalipwa moja kwa moja kwa kampuni inayofanya kazi kutoka *Exim Bank*. Malipo yanatolewa kutokana na kazi iliyokamilika na nawahakikishia kuwa kazi hii inakwenda kwa muda uliopangwa.

Aidha, aliendelea kusema kwamba kuanza zoezi la kuondosha majengo yaliyojengwa juu ya miundo mbinu ya maji. Mhe. Spika, niseme kwamba zoezi hili ni endelevu tunaomba Waheshimiwa Wajumbe muwe wastahamilivu pale tunapochukua hatua ya kunusuru mabomba na vianzio vyetu vya maji.

Lakini pia Mhe. Hamza aligusia kufunga mkataba na makapuni ili kufunga mita za wateja kwa nia ya kuimarisha mapato. Mhe. Spika, niseme kwamba tumepokea ila kwa sasa *ZAWA* inanunua mita zake moja kwa moja kutoka kiwandani nchini Uturuki. Lakini pia amesisitiza kwamba Serikali kuiongezea *ZAWA* fedha kwa ajili ya kuweza kutekeleza kazi zake. *ZAWA* inatoa shukrani kwa kamati kwa juhudi zake zinazowezesha kuongeza fedha kwa ajili ya kuunga visima vya Ras Al Khaimah kufikia bilioni nne.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ameipongeza *ZAWA* na hasa Mkurugenzi Mkuu. Pongezi zimepokelewa. Lakini pia aliendelea kusema deni linapelekwa katika majumba bila ya upatikanaji wa maji. Mhe. Spika, ni kwamba mteja yeyote ambaye ameunganishwa na mtandao na ambapo huduma zetu za maji zinafika wateja hao wote wanapelekewa bili. Tunaamini tatizo hilo litaondoka baada ya

kukamika ufungaji wa mita utakaosaidia kumjua mteja anayepata na asiyepata maji.

Lakini Mhe. Simai Mohammed Said alisema maeneo mengi ya Tunguu hayapati maji. Ni kwamba mapungufu yaliyobakishwa na Mradi wa *ACD* yatasawazishwa kupitia Bajeti ya Serikali, lakini pia kupitia Mradi wa India ambao unaendelea katika hatua za *DPR*.

Lakini pia Mhe. Simai Mohammed Said alieleza kuhusiana na Uzi Ng'ambwa hakuna maji na Unguja Ukuu tangi ni bovu. Mhe. Spika, ni kwamba *ZAWA* imechukua hatua za awali kwa kuanzisha mradi mdogo wa uchochaji wa maji ya chumvi kwa ajili ya kupata maji ya kunywa. Suluhisho la kudumu itapatikana baada ya matengenezo ya tangi la Unguja Ukuu ambalo linatarajia kufanyiwa marekebisho mwezi wa saba mara tu baada ya kukamilika kwa tangi la Dimani mwezi huu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali alitoa pongezi kwa *ZAWA* kwa usikivu wao, pongezi tumezipokea. Lakini pia alieleza upatikanaji wa maji Jibwemtu. Mhe. Spika, jitihada za awali zimefanyika kwa kuchimba kisima kinachotumia umeme utokanao na nishati ya jua *(solar pumping)* na kulaza mabomba katika eneo la kijiji cha Bambi Jibwemtu.

Lakini pia ameshauri kufunga mkataba na kiwanda badala ya kampuni kwa ajili ya kufunga mita.
Mhe. Spika, ushauri umepokelewa na tunaendelea kununua vifaa kutoa kiwandani moja kwa moja. Lakini pia alishauri upatikanaji wa vitendea kazi ili kurahisisha kazi kwa *ZAWA*. Mhe. Spika, ushauri umepokelewa. Lakini alishauri kuwa na ulinzi wa askari katika maeneo ya vianzio vya maji. Ushauri umepokelewa kwa kuanzia maeneo yenye vianzio vikuu vya maji tayari yanalindwa na askari.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi aliomba kumaliziwa kisima japo kimoja. Ni kwamba kisima cha Fuoni Chunga utekelezaji wake unaendelea vizuri hatua iliyobaki ni uwekaji wa miundombinu ya umeme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala la upatikanaji wa maji Michamvi litaanza lini aliomba kuelewa hilo. Mhe. Spika, ni kwamba robo ya pili ya mwaka huu wa fedha yaani 2018/2019 inategemewa kuanza *inshaallah.* Alieleza kuhususiana na kijiji cha Jozani halikadhalika kwamba iangaliwe. Ushauri umepokelewa na mafundi watalitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo.

Lakini Mhe. Suleiman Sarhan Said ...

Mhe. Spika: Naomba uhitimishe Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, namalizia Mhe. Suleiman Sarahan Said alisema kwamba zaidi ya visima 24 havifanyi kazi alitaka kujua tatizo ni nini. Tatizo ni *pump* hazifanyi kazi kutokana na kuharibika kwa *motor* zake. Hata hivyo, serikali imeshaziagiza kutoka kwa msambazaji na zitarudishwa visimani humo mara tu zitakapowasili nchini mwanzoni mwa mwezi wa Julai. Na vituo alisema kwamba havina ulinzi hali kadhalika upotevu wa maji umekuwa mkubwa. Ni kweli kuna upungufu mkubwa

wa walinzi vituoni na tunalifanyia kazi kwa kufanya mazungumzo na taasisi za ulinzi Zanzibar.

Lakini kwa upande wa upotevu wizara kupitia *ZAWA* inaendelea kuyafanyia matengenezo mabomba kadri ya uwezo na upatikanaji wa vifaa utakaporuhusu, pia kupitia mradi unaoendelea wa kubadilisha mabomba hayo eneo la Mjini Magharibi utakapokamilika 2019.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nashukuru sana kwa mchango wako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waiunge mkono hoja hii kusudi watoe nafasi kwa kwenda kutekelezwa yale ambayo yameainishwa humu, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kwa heshima na taadhima nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ili aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa karibu sana.

Mheshimiwa una saa moja lakini leo kwa namna nilivyoisikia sauti yako unaweza kwa sababu Mhe. Naibu Waziri amekusaidia kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa ufafanuzi wa hoja naomba nichukue nafasi hii kwanza kuomba radhi sana kwa sababu leo *my voice is not very good, I have a flu.* Kwa hiyo, naomba radhi sana lakini nitajitahidi kadri nitakavyoweza ili niweze kuwasilisha kile ambacho tunakisubiri.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho ya hoja, michango na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kuchangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2018-2019. Aidha, naomba kuwashukuru Wajumbe wote kwa uchangiaji wao mzuri wenye tija kwa wizara yangu.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutambua na kuelewa kwamba serikali inapofanya vizuri inabidi ipongezwe. Tumepokea pongezi zote ambazo Waheshimiwa Wajumbe mmezitoa kupitia Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, nitajitahidi kuyajibu maswali yote ambayo Mhe. Naibu Waziri bado hajayatolea ufafanuzi na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atanisaidia.

Mhe. Spika, jumla ya Waheshimiwa 40 wa Baraza lako tukufu walichangia hotuba yangu, Waheshimiwa 25 walichangia moja kwa moja na 15 walichangia kwa maandishi. Wajumbe waliochangia moja kwa moja ni hawa wafuatao naomba niwataje kwa ruhusa yako Mhe. Spika.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Simai Mohammed Said

4. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Suleiman Sarahan Said
7. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
8. Mhe. Miraji Khamis Mussa
9. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
10. Mhe. Omar Seif Abeid
11. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
12. Mhe. Asha Abdalla Mussa
13. Mhe. Mussa Foum Mussa
14. Mhe. Ame Haji Ali
15. Mhe. Machano Othman Said
16. Mhe. Hidaya Ali Makame
17. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
18. Mhe. Shaib Said Ali
19. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
20. Mhe. Shehe Hamad Mattar
21. Mhe. Mohamed Said Mohamed
22. Mhe. Suleiman Makame Ali
23. Mhe. Khadija Omar Kibano
24. Mhe. Bahati Khamis Kombo na
25. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, hawa walichangia moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwataje waliochangia kwa maandishi ni kama wafuatao:-

1. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
2. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
3. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
4. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
5. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo
7. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
10. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale
11. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
12. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
13. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
14. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora
15. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na
16. Mhe. Rashid Makame Shamsi

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wajumbe kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba nianze na Wizara katika Kitengo cha Mipango na Uendeshaji. Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano alitoa hoja ya kuomba kwamba wizara ishirikiane na Washirika wa

Maendeleo katika miradi inayokusudiwa kutekelezwa na serikali. Naomba nimwambie Mhe. Hamza kwamba ushauri wake tumeupokea lakini tunashirikiana vizuri na Washirika wa Maendeleo katika kufanya zile kazi ambazo zimekusudiwa.

Pia ameweza kukumbusha kwamba zile stahiki za Mhe. Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi basi ziweze kutolewa. Naomba nimwambie kwamba Sheria ya Mahakama ya Ardhi inasema Mwenyekiti wa Mahakama anakuwa sawa na cheo cha Jaji wa Mahakama ya Mkoa. Kwa bahati mbaya sheria haikuonesha stahiki za Mwenyekiti moja kwa moja, suala ambalo linaleta utata kiutaratibu. Masuala yote ya uajiri na stahiki za watumishi wa Mahakama zote za hapa Zanzibar zinasimamiwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama. Hivyo, wizara yangu namhakikishia itapeleka ombi maalum kuhusu kadhia hii ili iweze kuchukuliwa hatua katika Tume ya Utumishi ya Mahakama.

Mhe. Mohamed Said Mohamed aliuliza kuna sababu gani za kukosekana kwa makusanyo ya mapato ya Idara ya Upimaji na Ramani kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Naomba nimjibu kwamba kutokana na mabadiliko ya mfumo wa Taasisi za Ardhi kifedha makusanyo ya mapato ya Idara ya Upimaji na Ramani kwa mwaka wa fedha 2018/2019 yameainishwa chini ya Kamisheni ya Ardhi ukurasa N01-16 kifungu Nam.1422043 (Ada ya Upimaji wa Ramani) ambacho wamekadiriwa kukusanya milioni 500 na kifungu Nam.1422008 (Utoaji wa Viwanja na Nyaraka) ambacho kimekadiriwa kukusanya milioni 250. Naomba mfanye *reference* katika hilo buku kubwa.

Pia aliomba kupata ufafanuzi wa usahihi wa fedha Tsh 3,459,511,000/- zinazotarajiwa kutumika katika Programu PN102 na sababu za kupungua kwa fedha za maendeleo Tsh. 585,841,000/-. Naomba nimjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed kwamba fedha za jumla Tsh. bilioni 3.459 ni fedha sahihi ambazo uchanganuzi wake unapatikana kwenye kiambatanisho H1, ukurasa wa 99 wa hotuba yangu ya bajeti. Kwa upande wa kitabu cha Mswaada wa Makadirio fedha hizo zimeainishwa kwenye PN0102 ukurasa wa 18.

Mhe. Spika, kuhusu milioni 585 fedha hizo ni za awamu ya mwisho ya Mradi wa *ICI* ambao ulipangwa kutekelezwa kwa miaka mitatu ambapo fedha zake hazikugaiwa sawa sawa kwa mujibu wa *action plan* ya mradi huo.

Pia aliendelea kuuliza kwa nini kumekuwa na ongezeko la asilimia 144 kwa Programu PN0105. Ni kweli kwamba kuna ongezeko kubwa ka fedha za maendeleo katika Programu ya PN0105 (Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati) kutoka bilioni 35.463 mwaka 2017/2018 hadi bilioni 86.501 mwaka wa fedha 2018/2019. Ongezeko hilo linatokana na kuwepo kwa kipaumbele cha utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na baadhi ya miradi ya maji kufikia katika hatua za utekelezaji, hatua ambayo itakuwa na matumizi makubwa ya fedha.

Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Maji chini ya ufadhili wa Serikali ya India ambao unatarajiwa kutumia Tsh. bilioni 40.9, Mradi wa Maji wa *ADB* unaotarajiwa kutumia bilioni 21.5.

Mhe. Spika, pia naomba kutoa ufafanuzi kwenye Sekta ya Nishati ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (*ZPRA*). Mhe. Yussuf Hassan Iddi aliuliza kwamba utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia umefanyika kwa kipindi sasa. Je, kuna matokeo gani.

Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia tupo katika hatua ya kufanya utafiti kwa njia ya mtetemo (*seismic*).Utafiti huu una hatua tatu mpaka kupata matokeo rasmi. Hatua zenyewe ni kama zifuatazo kwa faida ya wajumbe.

1. Ukusanyaji/uchukuaji wa taarifa (*Acquisition stage*)
2. Usafishaji wa taarifa (*Processing stage*)
3. Kutafsiri taarifa (*Interpretation stage*).

Baada ya kukamilika hatua tatu hizi ndio tutaweza kupata matokeo ya utafiti huo. Hatua tatu hizi mpaka kukamilika kwake zinachukua muda usiopungua miaka miwili, kwa hivyo tutategemea kupata taarifa ya matokeo baada ya hatua hizi za utafiti kukamilika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa pia aliomba kupata ufafanuzi wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya uandaaji wa rasimu za kanuni na miongozo ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, naomba kumjibu kwamba fedha za uandaaji wa rasimu za kanuni na muongozo zimejumuishwa katika shughuli za mamlaka ambapo kwa sasa fedha zake zinaingizwa kama ruzuku. Jumla ya milioni 49 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya uandaaji wa Kanuni na Miongozo pamoja na kazi za ufuatiliaji.

Vile vile alitaka kujua zoezi linaloendelea linafanywa bila ya mkataba wa mafuta. Je, kuna athari gani zitakazoweza kujitokeza ikiwa zoezi hilo litaendelea bila mkataba.

Nimtoe wasi wasi Mhe. Miraji Khamis Mussa kwamba hatutegemei kuwepo kwa athari yoyote. Na zoezi la Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia kwa hivi sasa linafanywa kwa kibali maalum (*conditional permit*) pamoja na *MoU* iliyosainiwa baina ya SMZ na Serikali ya Ras Al Khaimah.

Pia Mhe. Asha Abdalla Mussa alitaka kujua kuhusiana na suala la fidia kwa wananchi walioharibiwa mazao na mali zao wakati ile kazi ya utafiti ilipofanyika. Naomba nimjulishe kwamba fidia itatolewa na Kampuni ya *Rak Gas* kwa wale wote walioharibiwa mali zao kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016 tuliyoipitisha hapa na Sheria ya Umiliki wa Ardhi ya mwaka 1992 pamoja na Sheria ya Mazao. Mara tu baada ya kukamilika taratibu za kutathmini uharibifu huo ambao unafanywa kwa kushirikiana na Masheha.

Pia Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil alitaka kujua *Progress Report* ya zoezi la mtetemo. Naomba pia kumjulisha Mhe. Ahmada kwamba zoezi la mtetemo kwa upande wa baharini lilianza tarehe 28/10/2017 na kumalizikia tarehe 28/11/2017. Zoezi la mtetemo kwa upande nchi kavu lilianza tarehe 8/02/2018 hadi tarehe 26/05/2018. Hivi sasa tupo katika hatua za kufanya matayarisho ya kuanza zoezi katika Kisiwa cha Pemba ambalo linategemewa kuanza mwezi Julai, 2018.

Vile vile aliuliza sekta ya mafuta na gesi imejipangaje kutoka kwa *Dutch Disease*. Naomba nimwambie kwamba tumejipanga Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia itatumika kukuza na kuimarisha shughuli za kiuchumi za sekta nyengine na sio kuwa sekta tegemezi ya kuendeleza taifa.

Pia nilikuwa naomba niendelee kujibu masuala yaliyojitokeza katika Sekta ya Nishati upande wa *ZURA*. Mhe. Omar Seif Abeid alitoa ushauri kwamba *ZAWA* wapatiwe za *ZURA* kwa maendeleo ya maji. Nilikuwa naomba nimjibu kwamba fedha zinazokusanywa na mamlaka kama tozo ya udhibiti zinatumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila siku za mamlaka na ujenzi wa miundombinu na uimarishaji wa mifumo ya usimamizi wa huduma hizo.

Sehemu kubwa ya bajeti ya *ZURA* kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imeelekezwa katika uendelezaji wa eneo la Mangapwani ili kuiwezesha Zanzibar kuwa na uhakika na upatikanaji wa bidhaa za mafuta na kuiwezesha serikali kupata mapato zaidi yatakayotokana na biashara ya mafuta nchini na nje ya nchi.

Vile vile Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf aliuliza kwamba bei ya mafuta kwa pipa duniani sio ghali ambayo ni kiasi cha shilini 700/- za Kitanzania lakini Zanzibar mbona bei iko juu imefikia shilingi 2,250/-. Naomba kumueleza kwamba kwa upande wa bei za mafuta katika soko la dunia, taarifa rasmi ambapo wizara yangu kupitia *ZURA* inazo kupitia mtandao rasmi unaotoa bei za mafuta duniani *PLATTS,* zinaonesha kuanzia mwezi Julai, 2017, bei za mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia zimekuwa zikipanda mfululizo ambapo hadi mwezi Juni, 2018 bei hizo zimepanda kutoka dola za Kimarekani 45 sawa na 103,500/= za Kitanzania hadi dola 76 kwa pipa ambayo ni sawa na shilingi 174,800/= za Kitanzania. Gharama nyengine zinazoingizwa katika kukokotoa bei hizo ni gharama za usafirishaji hadi bandari ya Dar es Salaam, bima, faida ya muagiziaji *premium*, gharama katika bandari ya Dar es Salaam ikiwemo uhifadhi wa mafuta, gharama za bandari na kodi nyenginezo.

Pamoja na gharama hizo, usafirishaji kutoka bandari ya Dar es Salaam kuja Zanzibar ni gharama nyengine zinazoongeza bei ya mafuta kwa Zanzibar ikiwemo kodi za serikali pamoja na faida ya mletaji bidhaa hizo. Kutokana na uhalisia kwamba mafuta yanaingia Zanzibar kupitia Bandari ya Dar es Salaam ni kweli kwamba kuna tofauti ya bei kati ya Dar es Salaam na Zanzibar. Tofauti ya bei ya mafuta kwa Zanzibar na Tanzania Bara ni kama ifuatavyo:-

- Petroli Tsh. 20-15 kwa lita
- Dizel Tsh. 84-105 kwa lita.

Kwa upande wa mafuta ya taa bei za Zanzibar zipo chini kwa Tsh. 445 kutokana na serikali kuwajali wananchi wake na kuondoa kodi katika bidhaa hiyo ambayo hutumiwa zaidi na wananchi wa kipato cha chini.

Kwa mwezi wa Juni bei ya mafuta ya petroli Zanzibar ipo chini kwa Tsh. 27 kulinganisha na bei ya Dar es Salaam. Serikali kupitia mfuko wake maalum wa kuainisha bei za mafuta (*Price Stabilization Fund*), imefidia tofauti ya bei ili kuwapunguzia wananchi makali ya gharama za kuendeshea maisha kwa kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhan na Sikukuu ya Eid el Fitri.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alitaka kujua changamoto zinazotokea wakati wa kuadimika mafuta hususan kwa sheli za Mjini ambapo mafuta hayo hupewa watu na kuuza kwa kutumia madumu. Je, Mhe. Waziri wizara yako inachukua hatua gani zaidi ya watu hao.

Kabla ya kuanzishwa kwa *ZURA* utaratibu wa kufichwa kwa mafuta kwenye vituo na baadae kuuzwa kupitia madumu lilikuwa ni jambo la kawaida. Lakini naomba niseme kwa sasa moja ya majukumu ya *ZURA* ni kusimamia udhibiti wa mafuta. Mamlaka huwa inafanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha vituo vinauza mafuta kwa wenye vyombo vya moto na sio kwa wanaonunua kwa madumu

Aidha, *ZURA* inajitahidi kudhibiti wanaoleta mafuta wachukue hatua za mapema za kuleta mafuta ili kuepusha kuadimika kwa mafuta nchini. Kusema kweli tunampongeza Mhe. Mwakilishi kwa kusaidia kutoa elimu kwa kuzungumza na makampuni ya mafuta juu ya kutoa elimu kutowapa mafuta wauzaji wa madumu kama alivyosema.

Pia Mhe. Machano Othman Said alisema kwamba *ZURA* inaposhusha bei watu wenye mafuta wanachelewa kushusha, lakini pale bei inapopanda basi moja kwa moja siku hiyo hiyo mafuta yanapandishwa bei. Ni kweli tatizo hili mheshimiwa tumeliona kwa baadhi ya wamiliki wa vituo hasa bei inaposhuka. *ZURA* hufanya zoezi la ukaguzi vituoni mara tu panapokuwa na mabadiliko ya bei za mafuta, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanauziwa bidhaa hiyo kwa bei halali iliyowekwa na mamlaka, ambapo vituo vinavyokwenda kinyume na utaratibu huo huadhibiwa kwa kutozwa faini. Fani ya juu ni dola 500 hutozwa kwa kituo ambacho kinafanya uharibifu huo. *ZURA* hufanya mikutano ya mara kwa mara na wamiliki wa vituo vya mafuta na kuwapa indhari juu ya tatizo hilo linalokiuka maadili ya biashara.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Rashid Makame Shamsi alisema mafuta ya taa huadimika mara kwa mara, baadhi ya makampuni hawaagizi mafuta haya na wananchi wanapata usumbufu mkubwa. Lakini pia walishuhudia usumbufu wa kukosekana kwa mafuta ya *petrol* na *diesel* kwa vipindi tofauti.

Mhe. Spika, ni kweli kuadimika kwa mafuta ya *petrol*, *diesel* na taa kunatokana na ukosefu wa bandari yenye uwezo wa kuhimili meli kubwa na ukosefu wa sehemu ya kuhifadhia mafuta Zanzibar. Hali hii imepelekea kutegemea Bandari ya Dar es Salaam na Mombasa kwa ajili ya uingizwaji wa mafuta Zanzibar ambazo kwa sasa zimezidiwa uwezo wake wa kutoa huduma, jambo ambalo husababisha meli zetu ndogo kuchelewa kupakia katika bandari hizo na baadae kusababisha upungufu wa bidhaa hizo hapa nchini. Hata hivyo, wizara yangu imeweka mkakati maalum wa ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi pamoja na sehemu ya kuhifadhia mafuta huko Mangapwani ili kuondosha kabisa tatizo hili.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Nishati na Madini. Naomba nianze na swali lililoulizwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed alisema katika hotuba yangu hazikuwekwa taarifa za kitaalamu za nishati mbadala. Mimi niwaambie tu kwamba ushauri wake alioutoa tunaupokea katika hotuba ya bajeti basi tutaona namna ya kuweka hivyo vipengele kila itakapostahiki. Hata hivyo, idara husika inatoa taarifa za utafiti kupitia semina za kutoa uelewa kwa makundi mbali mbali ya jamii. Kwa kuwa utafiti bado haujakamilika ripoti ya awali taarifa zake ni kama ifuatavyo ambazo tumeshirikisha wadau wengi.

Kwa upande wa jua kwa Zanzibar (Unguja na Pemba) upatikanaji wake ni wastani wa kWh/m² 2100 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha kuwekeza ni 1277 kWh/m², lakini kwa upande wa mwendokasi wa upepo ni wastani 7 m/s kwa maeneo ya Makunduchi, Matemwe, Bambi, Muambe na Micheweni. Wakati kiwango cha chini cha upepo kinatakiwa kisipungue mwendokasi wa *6 meter per second.*

Kwa ufupi viwango vya upepo wa jua vinavyopatikana Zanzibar vinatoa mwelekeo mzuri katika uwekezaji. Muhtasari wa utafiti huo unaweza kupatikana katika Idara ya Nishati na Madini Zanzibar.

Naomba pia niende na swali la Mhe. Shehe Hamad Mattar alizungumzia kwa vile nishati ni muhimu katika maisha yetu. Ni hatua gani zinazochukuliwa ili kuhakikisha elimu ya matumizi ya nishati inawafikia wananchi wa vijijini.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Idara ya Nishati imekuwa ikitoa elimu ya matumizi ya nishati kwa makundi mbali mbali ya jamii kama nilivyoeleza katika hotuba yangu kifungu cha 72, ukurasa wa 35.

Elimu ya uelewa kuhusu Nishati Mbadala kwa kutumia wasanii Kikundi cha Kachara imefanywa katika maeneo tofauti Chake Chake, Kiwani, Mkoani, Melitano, Piki, Ziwani, Mzambarauni, Mtambwe, Wete/Chake Chake, Njiampya, Micheweni, Makunduchi, Bambi, Matemwe na Unguja Mjini. Vikundi mbali mbali vya kutoa elimu vilifanya hiyo kazi.

Mbali ya maeneo niliyotajwa elimu hiyo imetolewa katika maskuli 21 ya Unguja na Pemba. Aidha, vyombo mbali mbali vya habari vilitumika katika kutoa elimu kuhusu nishati mbadala. Kazi hiyo ni endelevu itazidi kuendelea ili wananchi waweze kupata huduma.

Mhe. Spika, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti wa Kamatiya Ardhi na Mawasiliano, Mhe. Hamza Hassan Juma alitoa ushauri wa kupimwa upya eka tatu na kusema kwamba zile ambazo hazina sifa basi ziweze kubadilishiwa matumizi yake.

Wizara imepokea ushauri wa kamati na kwa kweli tayari imeanza kuufanyia kazi. Ukaguzi wa eka kwa kila Wilaya za U|nguja umeimarishwa. Kwa eka zilizopoteza sifa kwa kubadilishwa matumizi, wizara imeshazingatia kuzipanga upya matumizi yake ili ziweze kupimwa kwa ajili ya matumizi ya makaazi na huduma.
Mhe. Omar Seif Abeid alisema kwamba viwanja vilivyopimwa Tumbe ambavyo bado havijagaiwa. Tayari viwanja hivyo vimeshaanza kupangiwa wananchi mbali mbali wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi na ni matarajio ya kukamilishwa ugawaji wa viwanja hivyo mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema Idara ya Mipango Miji ina mipango mingi lakini utekelezaji hauonekani. Mhe. Jaku alichosema ni sahihi kabisa. Idara ya Mipango Miji kazi yake ni kupanga kazi nyengine zote ni shirikishi kuanzia wananchi wenyewe, Serikali za Mitaa, Manispaa, Halmashauri, Wakala wa Majengo, Wakandarasi, Shirika la Nyumba na wadau wengineo wa kuendeleza

Mipango Miji. Ndio maana mara tu, baada ya Mipango Miji kupangwa, mpango ule unawasilishwa kwa wadau wote kwa ajili ya utekelezaji.

Kucheleweshwa kutolewa kwa *land lease*. Utolewaji wa *lease* ni mchakato ambao unaanza katika hatua ya kuhakiki umiliki wa mhusika pamoja na kuthibitishwa kwa mradi unaotakiwa kuwekeza katika eneo hili kwa kupitia ofisi ya *ZIPA*. Pia, naomba Wajumbe wafahamu kuwa mkataba wa ukodishaji ardhi ni makubaliano baina ya serikali na mhusika. Kwa hivyo, taratibu za kukamilika kwa utolewaji wa mikataba ya ukodishwaji ni lazima iwasilishwe Ofisi ya Mwanasheria kwa kupitiwa. Kiujumla hakuna mikataba ya ukodishaji inayocheleshwa pindipo kutakuwa hakuna vipingamizi vya sheria na utaratibu vitakavyojitokeza. Lakini kama kutakuwa na vipingamizi basi hati hizo pia zinaweza kuchelewa. Kwa sababu hata Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inabidi ichukue muda kuvipitia na kuviweka katika utaratibu ulio mzuri.

Naomba niende kwa Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Suala la Mipango Miji kuhusu kupewa kipaumbele. Naomba kusema kwamba wizara inachukua ushauri na itaufanyia kazi kwa kadri inavyowezekana. Lakini naomba niwajulishe kwamba, serikali imeshaanza upangaji wa miji 14 kati ya miji hiyo ni mji wa Chake Chake na mji wa Wete. Taratibu za upangaji wa mji wa Chake Chake zimeshaanza na upangaji wa mji wa Wete nao utafuata.

Pia walishauri kutolewa kwa nyaraka za ardhi katika ofisi nyengine. Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa kuona tatizo la utolewaji wa nyaraka za ardhi na baadhi ya taasisi. Wizara yangu imefanya jitihada kubwa ya kukabiliana na suala hili ikiwemo kufanya mazungumzo na ofisi zinazotoa nyaraka zinazohusiana na ardhi ili kuweza kuwa na utaratibu mmoja tu wa kutolewa hati za ardhi na wizara inayohusiana na masuala ya ardhi kama sheria zetu zinavyoelekeza.

Pia wizara yangu imetoa elimu kwa wananchi na inaendelea na uhamasihsaji na nashukuru wananchi wengi kwa sasa wameweza kuelewa kuwa hati miliki za ardhi zinatoka ndani ya wizara yangu.

Aidha, natumia nafasi hii kuwatanabahisha wananchi kuwa hati za ardhi zinatolewa na Wizara ya Ardhi kupitia Kamisheni ya Ardhi. Hivyo, ni imani yangu kuwa wananchi watakapofuata utaratibu unaotakiwa utawezesha kwa kiasi kikubwa kuondoa migogoro ya ardhi

Ofisi ya Mrajis wa Ardhi ina jukumu la kusajili ardhi yote ya Zanzibar, lakini sualala mirathi limekuwa changamoto kubwa katika kufanikisha lengo hilo. Afisi ya Mrajis wa Ardhi imejipanga kutekeleza usajili wa ardhi za mirathi ikiwa ni pamoja na kuwa na kitengo rasmi cha usajili wa ardhi za mirathi ambacho kina bajeti maalum ya kukiwezesha kutekeleza kazi hiyo. Hata hivyo, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ndio taasisi mama inayosimamia suala la mirathi na Afisi ya Mrajis inafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na taasisi hiyo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud aliuliza suala la ubadilishaji wa umiliki kutoka kwa mrithi kuwa ni shilingi 250,000/- ni kubwa kwa wanyonge anaomba ipunguzwe. Mheshimiwa ni kweli ada sasa hivi ni shilingi 250,000/-, lakini ada ya

kupatiwa kitambulisho kipya cha umiliki wa matumizi ya ardhi ya eka tatu ni shilingi 20,000/- na imependekezwa kuwa shilingi 30,000/ kuanzia mwaka wa fedha 2018/19. Isipokuwa ada ya upimaji ndio shilingi 250,000/- ambazo ni kiasi cha kugharamia huo upimaji wenyewe tu. Hata hivyo, wizara inapokea ushauri wa Mhe. Masoud kwa kuweza kuwazingatia wanyonge ambao hawana uwezo wa kugharamia upimaji.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud pamoja na Mhe. Said Soud Said walisema kwa nini wananchi hawapatiwi viwanja mpaka wanafika kujenga katika maeneo sio. Kwa kweli serikali inajitahidi kupima na kugawa viwanja, viwanja vingi ambavyo mpaka sasa vimepimwa bado havijaendelezwa. Lengo la serikali wananchi kuwa na makaazi bora.

Kwa upande mwengine, serikali sasa imeamua kutilia mkazo zaidi katika kuanzisha ujenzi wa makaazi bora wa nyumba za ghorofa, badala ya kutegemea utoaji wa viwanja kwa mtu mmoja mmoja ambao kwa vyovyote vile hautaweza kukidhi mahitaji na makaazi ya wananchi.

Mhe. Omar Seif Abeid aliendelea na kusema ramani ya mji wa Konde imepitwa na wakati. Ni kweli lakini namhakikishia Mhe. Omar kwamba katika miji 14 ambayo serikali inaipanga moja ni mji wa Konde. Hivyo, ramani mpya za Mji wa Konde zitarudishwa katika mpango wake wa kisasa kama ilivyokuwa hapo awali. Naomba tu avute subira Mheshimiwa.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf nae aliendelea kwa kusema ujenzi holela Idara ya Mipango Miji ipo haja ya kutenga maeneo maalum ya kujenga wananchi ili kuondokana na tatizo hili la ujenzi holela. Lakini pia aliuliza kwamba ule ujenzi unaojengwa pale mbele wa skuli na nyumba *DCU* unautambua. Na akatoa ushauri. Wizara imepokea ushauri wa Mhe. Mjumbe na napenda kumkumbusha kuwa serikali inaendelea na upangaji wa miji 14 ambayo ndani ya miji ile itakuwa na maeneo ya makaazi, biashara pamoja na huduma nyengine zote za kijamii. Pia napenda kumjulisha na kumhakikishia kwamba ujenzi wa Skuli ya Nyuki unafuata taratibu zote za ujenzi chini ya *DCU* na hautoingia katika sehemu ya barabara.

Vile vile naomba nimjibu Mhe. Naibu Waziri wa Afya alishauri wananchi wasimamiwe wanapohitaji kujenga nyumba za kuishi ili wajenge kwa kufuata *plan* za mipango ya miji, ili iwe rahisi kupitisha gari baina ya nyumba na nyumba, au mitaa kwa mitaa kwa tahadhari ya kujikinga na majanga.

Ushauri wa Mheshimiwa umepokelewa na wizara imeanza kupitia Taasisi ya Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi kuhakikisha kwamba ujenzi unasimamiwa. Lakini kwa bahati mbaya kwamba watu wa *DCU* ni wachache lakini wanaojenga ni wengi, ndio maana tukasema kazi hii inabidi iwe kazi shirikishi, lakini wizara itaendelea kulitilia nguvu suala hili ili tuweze kufanikiwa katika kazi zetu za kila siku. Hili pia linahitaji mashirikiano ya pamoja ya sisi sote pamoja na Serikali za Mitaa na wananchi kwa ujumla, ili tuweze kutoa taarifa na elimu kwa watu wetu.

Mhe. Hidaya Ali Makame aliuliza ni zipi taarifa sahihi kuhusu ujenzi wa nyumba za maafa Fukuchani. Ni kweli kuwa serikali ilikuwa na nia ya kujenga nyumba za maafa Fukuchani, lakini kwa vile serikali tayari imeshalipanga eneo la Nungwi,

imeamua kupeleka ujenzi za nyumba hizo huko Nungwi ili wananchi wengi wafaidike na kupata huduma zitakazotolewa.

Aidha, nimhakikishie Mhe. Hidaya Ali Makame kuwa nyumba hizi hazijengwi katika eneo la vijiji na hazijengwi kwenye viwanja vya wananchi. Nyumba hizi zimepangwa katika eneo la uwanda ambako ndiko mji mpya wa Nungwi utajengwa. Eneo hili la maweni ni eneo la serikali.
Wizara itafanya ziara katika eneo hilo kama ulivyosema la Nungwi kutoa elimu zaidi juu ya upimaji huo.

Mhe. Shaib Said Ali aliuliza Mipango Miji haiendelei, lini itaanza kutumika. Napenda kumhakikishia kwamba Mipango Miji tayari inatumika, *master plan* imeshafanywa na inatekelezwa. Aidha, kwa upande wa maeneo mengine inaendelea na upangaji miji ile 14 ambayo tumeizungumza na kati ya miji hiyo kuna miji ambayo tayari imeshapangwa. Nungwi tayari kumeshapangwa, Dunga, Mkokotoni, Chwaka tayari imeshapangwa na mipango hiyo tayari inatumika. Wizara itazidi kulitilia nguvu suala hili na naomba tushirikiane na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia wilaya na masheha kuhakikisha kwamba mipango hii inatekelezeka, pamoja na wananchi wenyewe kwa jumla.

Elimu ya Mirathi ni muhimu hasa kwa vile wanaoathirika ni wanawake na watoto, hivyo elimu ya mirathi itolewe mijini na vijijini. Kama nilivyolijibu kwa Mhe. Shehe Hamad Mattar, tayari taratibu zinafanywa kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Ofisi ya Mufti kutoa elimu ya mirathi Unguja na Pemba, ili kuwaelimisha na kuwashajihisha wananchi juu ya umuhimu wa kuharakisha mirathi, ili kukamilisha usajili wa ardhi za mirathi.
Pia Mhe. Shehe Hamad Mattar aliendelea kusema je, ujenzi kutoka Amani mpaka Kiembesamaki majengo hayo yako kihalali. Je, *DCU* inafanya kazi.

Nasema kwamba *DCU* inafanya kazi na majengo yanayojengwa katika barabara ya Amani mpaka Kiembesamaki yanajulikana na serikali, na *DCU* inaujua ujenzi huu. Aidha , ujenzi wa eneo la Mazizini ni ujenzi wa serikali.

Mhe. Rashid Makame Shamsi nae aliendelea kwa kusema kwamba maeneo ya uwekezaji yasiyoendelezwa na kuikosesha serikali mapato hatua gani ambazo sisi tunazichukua. Naomba niseme kwamba wizara yangu inayashughulikia maeneo yote yaliyokuwa hayajaendelezwa na sio tu kwa maeneo ya uwekezaji peke yake, pia maeneo yaliyotolewa hati za haki ya matumizi ya ardhi. Hivyo, hatua za kisheria zimeanza kuchukuliwa kwa wale wote waliokiuka masharti ya upewaji wa maeneo hayo.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini nae aliuliza ule mpango wa *Land Use Plan* wa nchi nzima, ili kuweza kutenga maeneo maalum tukajua ujenzi uko wapi, kilimo, ufugaji na mambo mengine. Kwanza Mheshimiwa hii *Land Use Plan* tayari inatekelezwa toka mwaka 2015. Serikali ilipitisha rasmi mkakati wa taifa wa matumizi ya ardhi (*National Spatial Development Strategy – NSDS*), uliozingatia mambo yote na ambayo tayari umeshaanza kutekelezwa. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane kuhakikisha kwamba huu mpango unatekelezeka na tunautekeleza katika maeneo yetu.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini aliendelea kusema kwamba ni vyema basi tukaletewa ule mpango Barazani na Sera ya Ardhi, ili Waheshimiwa Wawakilishi nao wakaweza kuufahamu vizuri. Ushauri tunaupokea na tutajitahidi kuhakikisha kwamba semina tulete Barazani na tuweze kuja kutoa elimu ndani ya Baraza ili muweze kufahamu na kuelewa kilichopo.

Pia alisema kwamba usimamizi wa matumizi uwe imara kwa kusimamia sheria. Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini ushauri wake tumeupokea sana na ushauri tutaendelea kuufanyia kazi katika suala zima la kuwa imara katika usimamizi wa sheria na ndicho sasa hivi tunachoendelea nacho.

Pia Mhe. Asha Abdalla Mussa alizungumza kuhusu suala la upimaji wa eneo la kwa Gube. Naomba nimhakikishie Mhe. Asha kutokana na *master plan* ya eneo hili ni eneo la kilimo, wizara inataka eneo hili liendelee kuwa la kilimo. Hata hivyo, wizara itakutana na Halmashauri ya Kaskazini 'B' kulifanyia kazi suala hili ili kuona tunawasaidiaje wananchi wa eneo hilo.

Vile vile alizungumzia kuhusu kiwanja kilichopo Kiwengwa Cairo kinamilikiwa na nani. Mimi naomba niseme kiwanja hicho mwanzoni kilitolewa kwa mwananchi na kupewa Hati ya Haki ya Matumizi Ardhi na baadae kufutwa na kupewa Wizara ya Elimu. Baada ya hatua hii, suala hili lilipelekwa mahakamani na kama tunavyojua kwamba mahakama ni mhimili unaojitegemea. Kwa hivyo, wizara yangu ina heshimu maamuzi ya mhimili huo wa serikali na suala hili linaendelea kufanyiwa kazi kama taratibu na sheria zinavyoelekeza na mahakama iliweza kutoa hukumu tofauti na yale maamuzi ambayo sisi tuliweza kuyatoa.

Mh. Nadir Abdul-latif Yussuf alisema utolewaji wa viwanja kwa *Zanzibar Heroes* kuzidi idadi ya wachezaji. Tukumbuke kwamba suala la utolewaji wa viwanja umeainishwa chini ya sheria na kwamba mwananchi yeyote anayo haki ya kuomba na kupatiwa kiwanja na serikali. Aidha, utaratibu uliotumika katika kutoa viwanja walivyopatiwa *Zanzibar Heros* ulianza kwa kulipanga na kulipima eneo hilo. Hivyo, baada ya kukamilika utaratibu huu *Zanzibar Heroes* wamepatiwa pamoja na wananchi wengine.

Wakati tunapanga eneo lile na kulipima, tulikuwa na mpango wa kupima viwanja 100, lakini kwa uharaka tukapima viwanja 55 ili tuweze kukidhi haja. Kwa hivyo, *Zanzibar Heroes* tukawapa viwanja 33 na wananchi wengine tukawapa viwanja 22 na sio tisa kama alivyosema. Lakini bado tukaendelea kulipanga eneo lile kwa ule mpango ambao tulikuwa tunao na bado tunaendelea kutoa vile viwanja na tumeshatoa viwanja karibu 35 na tutaendelea kuvitoa kama sheria inavyotwambia.

Pia nimhakikishie Mhe. Nadir alisema kwamba tunatoa viwanja bila ya utaratibu. Tunatoa viwanja kwa utaratibu kamisheni inafanya kazi yake, lakini hata bodi inafanya kazi yake. Naomba nimhakikishie kwamba tunafanya kazi kwa mashirikiano makubwa sana na bodi kupitia kwa Mwenyekiti wake makini na mahiri Ndg. Abdi Khamis ambaye tunafanya kazi nae kwa pamoja kwa kila tone la taarifa, basi iwe kwake, iwe kwangu tunafanya kazi na tunapeana. Kama tunavyojua *information* yoyote *is power,* kwa hiyo taarifa hizi zote tunafanya kazi kwa mashirikiano makubwa. *(Makofi)*

Pia ameomba wizara inapotaka kufunga mikataba ya awali iwaite wahusika wasikilize hoja zao. Wizara inatoa indhari ya kufuta na kupewa muda kama sheria inavyoelekeza. Sisi tunajua kwamba hatuwaiti, lakini tunapotoa indhari maana yake ni *notice*, unampa mtu tahadhari na unampa mtu muda. Kwa hivyo, kama kuna mtu yeyote mwenye *concern* anatakiwa afike wizarani na wale wenye *concern* wote wanafika wizarani, wanaandika barua na hatua na taratibu za kisheria zinafanyika. Kwa hivyo, hili naomba nimhakikishie kwamba tuko sawa tunatenda kwa mujibu wa sheria na utaratibu ambao wizara yangu unautumia kupitia Kamisheni ya Ardhi.

Vile vile naomba kumjibu Mhe. Ame Haji Ali swali lake la maeneo ya wananchi kupewa wawekezaji bila kulipwa fidia. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu wa kutolewa Mikataba ya Ukodishaji kwa Wawekezaji unafanywa kwa kuzingatia taratibu za kupatikana maeneo hayo kama umefuata sheria na taratibu. Aidha, suala la fidia kwa wananchi linafanyiwa uhakiki wa hali ya juu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa ambapo ngazi ya Wilaya na Shehia huthibitisha fidia inayolipwa kwa eneo linalotaka kuekezwa.

Hivyo, wizara yangu haitoi mkataba wa ukodishaji iwapo eneo linalotaka kuekezwa halijalipiwa fidia kwa mwananchi mwenye haki ya matumizi ya eneo husika na ndio maana kazi hizi mara zote kama anavyosema zinakuwa shirikishi hatukurupuki. Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi zao, Halmashauri zinafanya kazi zake lakini na masheha ndio wa mwanzo kututhibitishia kwamba eneo hili tayari lina fulani na fulani, lakini na haki zao zinaweza kupatikana. Kama kuna sehemu ambayo kuna tatizo naomba Mhe. Ame basi anione ili niweze kukaa na watendaji wangu wa Kamisheni tuweze kuibua hilo tatizo kama lipo.

Vile vile Mhe. Shaib Said Ali alieleza suala kuhusu ucheleweshaji wa kutolewa hati. Nimwambie tu kimsingi utolewaji wa hati za matumizi ya ardhi hutolewa baada ya kukamilika taratibu za kuhakiki umiliki wa mhusika na kazi hii inafanyika kwa ufanisi. Aidha, niwajulishe Wahishimiwa Wajumbe kuwa wizara yangu kwa sasa inatoa hati mpya za matumizi ya ardhi. Hivyo, wajumbe wanatakiwa kuomba kupatiwa hati hizo mpya ambazo zimeboreshwa kwa kuzingatia viwango vya kisasa.

Vile vile alizungumzia suala la wawekezaji waliofutiwa Mikataba ya Ukodishaji. Serikali inaendelea na zoezi la kufanya uhakiki la kuwabaini wawekezaji wote ambao wameshindwa kuendeleza maeneo kwa muda mrefu, ambapo viwanja vya uwekezaji kwa Unguja na Pemba tayari vimesharudishwa serikalini na uhakiki wa maeneo mengine unaendelea kufanyika.

Pia alitaka kujua mwekezaji wa Mpapindi anafanya nini. Mradi wa Mpapindi unaendelea na kufanyiwa uhakiki na kuangaliwa namna kukamilisha taratibu zilizo bora za kuendeleza eneo hilo kwa kushirikiana na *ZIPA.* Labda katika hili nilifafanue kidogo kwamba suala la Mpapinde aliomba kubadilishiwa hati ambayo imechukua muda kidogo kutokana na kubadilisha kwa jina. Kwa hivyo, tukamwambia afuate taratibu za kubadilisha jina ndipo hapo aweze kupewa hati nyengine na ili aweze sasa kukamilisha taratibu nyengine.

Mhe. Mohamed Said Mohamed kwanza alitoa pongezi. Mimi nimwambie kwamba pongezi tumezipokea kwa kuanzisha *data base* ya ardhi na tutaendelea kuitumia *data base* hiyo vizuri.

Vile vile alizungumzia kadhia ya eneo la Nungwi lililofutwa na pia wazee hawaruhusiwi kulihaulisha kwa nini. Nimjibu Mhe. Mohamed bahati mbaya hayupo kwamba eneo hili limerudi mikononi mwa serikali kutokana na maamuzi ya serikali. Naomba ikumbukwe kuwa ardhi ni mali ya serikali na iko chini ya mamlaka ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

Pia alitaka kujua watu wanaomiliki eka zaidi ya moja anataka kupatiwa idadi yao. Naomba nimjibu kwamba wizara yangu inasimamia misingi ya sheria katika ugawaji wa eka ambazo zimetolewa na serikali. Kwa hivyo, kama kuna watu wanakiuka au wana vitu vingi wananunua wizara yangu haijui taarifa hiyo, hivyo tunaomba Mheshimiwa kama anazo taarifa kamili basi Kamisheni ya Ardhi ipo kwa ajili ya watu wote tunaomba atuletee taarifa hizo kamili ili wizara yangu iweze kuzifuatilia.

Vile vile Mhe. Mohamed Said Mohamed alizungumzia suala la ripoti ya Mhe. Ali Mzee ambayo anasema haijajibiwa na serikali na ni lini waziri ataleta majibu ya ripoti hiyo. Naomba niseme kwamba, kwanza taarifa hii imeshajadiliwa ndani ya Baraza hili kwa wale waliokuwepo ambapo sisi wegine tulikuwa hatupo kipindi kilichopita na maagizo yalitolewa kwa serikali, maoni na maagizo yalitolewa, lakini serikali imeyafanyia kazi kwa namna inavyoona inafaa.

Mhe. Spika, vile vile aliuliza kwamba mkakati wa usajili wa ardhi ukizingatia wananchi wengi hawana uwezo wa kusajili ardhi na ardhi ni mali ya serikali. Naomba niseme kwamba kwa sasa usajili wa ardhi unaendeshwa na serikali. Hata hivyo, wananchi wanatakiwa kuchangia ada ndogo tu kwa ajili ya kufanyia suala la usajili wa ardhi kuwa endelevu.

Mhe. Machano Othman Said nae aliuliza swali kuhusu ardhi ya Mkumbuu. Naomba nimjibu Mhe. Machano swali lake kama ifuatavyo. Eneo la Mkumbuu limekuwa likitajwa sana kuwa ni eneo la bandari au mafuta. Shirika la Bandari hadi sasa halijatoa ramani au waraka wowote kuhusu mahitaji hayo. Kadhalika hakuna taarifa zozote rasmi za kuwepo kwa mafuta katika eneo hilo. Hata hivyo, ili kuzuia migogoro na matumizi mabaya ya eneo hilo Wizara ya Ardhi kupitia Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba inatayarisha mabango kupiga marufuku ya matumizi ya aina yoyote ya kudumu ikiwemo ujenzi wa nyumba za kuishi, uwekezaji na kadhalika hadi hapo serikali itakapotoa taarifa rasmi ya eneo hilo.

Mhe. Spika, sasa niendelee katika Sekta ya Maji ambayo Mhe. Naibu Waziri alianza na akawa hakuimaliza. Niende kwa Mhe. Bahati Khamis Kombo alitupongeza sana, alimpongeza Mhe. Waziri, Naibu na watendaji wake, pongezi zimepokelewa. Na alisema kwamba miundo mbinu ya maji tuibadilishe kwa kuchimba visima ambavyo havina gharama kubwa kama wanavyochimba wananchi wenyewe. Tunamwambia wazo lake tumelipokea na tutalifanyia kazi kitaalamu. Lakini kwa mujibu wa *ZAWA* huwezi kutumia visima vidogo kwa kuhudumia watu wengi na ndio maana *ZAWA* inatumia visima virefu.

Pia Mhe. Juma Ali Khatib alitoa ushauri kwamba tuongeze bidii katika kuweka miundo mbinu ya maji na kuwa na umakini wa kuchagua pampu zilizo bora. Ushauri umepokelewa na naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hatua tayari zimechukuliwa kwa kununua pampu kiwandani moja kwa moja na pampu ambazo tumehisi ziko bora zaidi.

Lakini pia Mhe. Moh'd Mgaza Jecha aliuliza kwamba tangi la maji la Mtambile vipi mpaka leo lina uvujaji mkubwa halitoi huduma. Ni kweli, tangi hilo halitoi huduma kutoka na uvujaji mkubwa lakini wananchi wa eneo hilo wanapata maji bila ya usumbufu. Kwa hiyo, *ZAWA* wamejipanga kukarabati tangi hilo pale uwezo utakapopatikana baada ya bajeti.

Pia Mhe. Mtumwa Peya Yussuf pia aliomba wafanyakazi wanaojitolea wa kulinda vituo wapewe mishahara. Mhe. Mtumwa ushauri umepokelewa na suala hili tutalifanyia kazi, hata sisi tunaiona hiyo *concern* ila kwa sasa wanapatiwa posho ya kujikimu kwa kila mwezi.

Pia Mhe. Masoud Abrahman Masoud aliendelea katika suala la maji akasema kisima cha Kizimbani ni kisima cha kilimo au kwa ajili ya kutumia wananchi. Mhe. Masoud nikwambie kwamba kisima kile kipo kwa ajili ya wananchi na wananchi wanatumia kisima kile. Lakini vile vile na watu wa Kizimbani kwa maana ya kilimo wanatumia kisima hicho pia. Vile vile alielezea ubovu wa mabomba eneo la Dole mpaka Mfenesini. Nafikiri suala hili tunalizungumza kila siku ni suala endelevu kwamba matengenezo yanaendelea kufanywa na yataendelea kufanywa kadri hali ya ubovu wa mabomba inavyojitokeza. Pia eneo hili litanufaika kupitia mradi India wakati wa kubadilisha yale mabomba. Lakini pia visima vilivyochimbwa Bumbwisudi ni kwa ajili ya watu wa mjini nimeulizwa.

Naomba niseme kwamba visima vya mradi kwa ajili ya kuimairisha huduma za maji vya Bumbwisudi ni visima vya Mkoa wa Mjini na Magharibi. Lakini pia kulikuwa na suala la kutolewa na pampu kisima cha Kizimbani na Bumbwisudi. Swali hili pia tunaweza kulifanyia kazi pampu hizi zilikuwa mbovu lakini zitarudi baada ya muda si mrefu kwa sababu pampu zimekuja na zitakuja nyengine mwezi wa Julai mwaka huu na bado kiwanda kile kinacho tu- *supply* kitaendelea kila muda kutuletea pampu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa ametoa pongezi kwa *ZAWA,* pongezi zimepokelewa. Lakini pia Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Bahati Khamis Kombo walizungumzia kwa hisia jinsi ya mishahara mipya kwa ajili ya wafanyakazi wa *ZAWA.*

Naomba niseme Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala hili linatugusa sote kwa sababu ni hisia kwa kweli. Ni haki ya mtu na wananchi hawa ni wa kwetu lakini ni wafanyakazi wa kwetu. Lakini niwahakikishie kwamba suala hili tayari limeshafanyiwa kazi na kuanzia mwaka huu wa fedha 2018/19 basi wataanza kulipwa baada ya kupitishwa bajeti hii hapa. Tukimaliza bajeti *immediately* mwezi wa saba wanaanza kupata mishahara mipya.

Lakini vile vile Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Asha Abdalla Mussa waliuliza ujenzi wa tangi kubwa la maji Chaani umekamilika, lakini baadhi ya

vijiji bado havipati maji. Naomba nijibu kwamba serikali kupitia wizara inaendelea kuunganisha miundombinu mipya na iliyopo, mara tu baada ya kukamilika kwa bajeti hii tunayoendelea nayo ya mwaka wa fedha 2018/2019 basi kazi hii itaendelea na maji yatapatikana. Pia vijiji vya Kikobweni na Kinyasini vitapata maji kupitia mradi mpya wa Bandamaji ambao tayari serikali imeshatiliana saini na wakandarasi kutoka China.

Halafi pia liliulizwa swali wananchi wa Kichongoni fidia watalipwa lini. Naomba niseme kwamba fedha hizo zimeshaombwa kwenye robo ya tatu ya mwaka huu na malipo yatafanywa mara tu baada ya kupatikana fedha hizo. Lakini pia iliulizwa fedha za uendelezaji wa mradi wa China 2018/19 ni kiasi gani. Ni milioni 171.2.

Lakini vile vile Mhe. Said Soud Said aliluza changamoto za mashine kwenye visima. Ni kweli changamoto hiyo ipo. Hata hivyo, *ZAWA* imeanza utaratibu wa kuagiza pampu zenye ubora kutoka kiwandani moja kwa moja.

Pia Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa amemuomba Mhe. Waziri kutatua shida za maji Mkoa wa Mjini. Shida ya maji katika Mkoa wa Mjini inategemewa kumalizika baada ya kukamilika kwa miradi mitatu mikubwa wa *AfDB, India* na *JICA*.

Mhe. Shamata Shaame Khamis pia alizungumzia tatizo la maji Finya. Naomba nijibu kwamba kwa ujumla Finya hakuna tatizo na kisima cha Kwale Gongo kitapeleka maji Kinyasini baada ya kukamilika kwake. Ulipwaji wa fidia Kinyasini, wananchi wote wa Kinyasini tayari wamelipwa fidia, isipokuwa kuna tatizo kwamba baadhi ya wananchi hawakuridhika na fidia waliyolipwa kutokana na tathmini ambayo imefanywa. Lakini naomba niseme kwamba hakuna mwananchi yeyote anayedai.

Mhe. Khadija Omar Kibano pia alizungumzia tatizo la maji Mtambwe Kinazini. Naomba nimjibu kwamba Mtambwe Kinazini tayari wameshapatiwa maji kupitia Mradi wa Nishati ya Jua. Kwa hivi sasa kama ni *pilot project* na tatizo linajulikana lakini *ZAWA* bado wanaendelea kujipanga kuhakikisha kwamba changamoto hizi zote kwa dhamira ya serikali basi tunaweza kuzifanyia kazi. Lakini pia kukawa na tatizo la maji Makongeni na pia hii ipo katika mchakato wa manunuzi ya mabomba baada ya kukamilika hatua hiyo wananchi watapata huduma.

Lakini Mhe. Mussa pia alizungumzia Chole haipati maji, pampu zitakapofika irejeshwe ili huduma irejeshe. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba mara baada ya kufika kwa pampu katika mwezi wa Julai huduma hii itarudi kama kawaida. Tunaomba mvute subira na muwe wastahamilivu.

Lakini Mhe. Viwe Khamis Abdalla pia alizungumzia shida ya maji Kiuyu Minungwini. Hii ni shida ambayo kila siku Mhe. Viwe kwa hisia kubwa huwa anaisema. Lakini imetokana na kuharibika kwa pampu na inatarajiwa kurejeshwa si muda mrefu kwa sababu pampu yake tayari imeshafika Pemba.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tusikilizane kidogo minong'ono imekuwa iko juu na sauti ya Mheshimiwa nayo kidogo sio nzuri. Kwa hiyo, naomba tusikilizane msikilize amalizie kidogo. Tuendelee Mheshimiwa. Endelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Aidha, pampu ya kituo cha *Amani Road* imeshaagizwa na itarejeshwa mara tu baada kuwasili. Pampu za Pemba kununuliwa Unguja, ni kweli na ni kwa sababu ya fungu kuu la ununuzi wa pampu na vifaa vya maji linaratibiwa na Afisi Kuu Zanzibar.

Mhe. Asha Abdalla Mussa pia alitaka kujua *10%* ya Kisima cha Kipandoni. Asilimia 10 ni ya utekelezaji wa kazi hiyo kwa hatua za awali za ujenzi wa kibanda na usafishaji wa kisima. Naomba niseme ahadi ya Mhe. Waziri ya kuchimba kisima Mgambo bado iko pale pale na uchimbaji wa kisima unategemewa kukamilika tu mara baada ya bajeti hii ya mwaka 2018/19.

Lakini pia Mhe. Machano Othaman Said aliuliza hatua ya mradi wa visima vya Bumbwisudi. Naomba nimwambie hatua iliyofikiwa ni ununuzi wa pampu na ulaziji wa mabomba kupitia mradi wa *NSPT* na *STECOL* hawa ndio wakandarasi ambao tumeingia nao mkataba.

Lakini vile vile Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini aliuliza kuhusu ubovu wa tangi la Dimani. Kama nilivyozungumza nyuma nilimjibu Mhe. Mwakilishi mmoja kwamba ubovu wa tangi la Dimani ahadi hii ipo katika mikono na itatekelezwa kama ilivyoahidiwa sambamba na utayarishaji wa pampu utakaofanyika mara tu baada ya kukamilika kwa tangi hilo.

Mhe. Hidaya Ali Makame pia alizungumzia tatizo la maji Nungwi. Lakini kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya maji kunakosababishwa na ukuaji wa mji kweli maji Nungwi yamepungua. Lakini nimwambie Mhe. Hidaya kukua kwa watu na ujenzi Nungwi ni maendeleo. Kwa hiyo, na sisi tumejipanga na tutahakikisha kwamba wananchi wa Nungwi wanaendelea kupata huduma hiyo muhimu ya maji. Na niseme kila wakati huwa narejea rejea kwamba dhamira ya serikali kila tone la maji lihakikishe kwamba linamfikia mwananchi na kila mmoja anajua thamani na thawabu ya kutoa maji. Kwa hiyo, hilo tutalishughulikia na tutaendelea kulifanyia kazi.

Lakini pia Mhe. Zaina Abdalla Salum alisema tutoe elimu kwa wananchi kuhusu *ZAWA*. Ushauri umepokelewa na elimu itaendelea kutolewa.

Mhe. Spika, naona nimejitahidi kuyajibu karibu maswali yote kama kuna swali moja ambalo sijajibu, basi naomba Waheshimiwa Wajumbe waweze kunivumilia. Lakini naomba niendelee kukushukuru Mhe. Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza na kwa umakini wenu ambao mmekuwa mkiuonesha muda hadi muda. Natarajia kwa mwaka huu wa fedha *inshaallah* Mwenyezi Mungu baada ya kupita bajeti hii pia tutaendelea kushirikiana. Tumekuwa tukishirikiana sana tukifanya ziara za mara kwa mara katika maeneo mengi. Mheshimiwa Mwakilishi anapokuwa na tatizo anasema twende tukaone na tunakwenda kwa kweli tumefanya kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Lakini niendelee tu kuwashukuru ile Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Tumefanyakazi nzuri sana kwa muda mrefu na mimi hili nalisisitiza kwa sababu kila siku nasema kama jambo zuri limetungwa basi serikali pia inahitaji kupongezwa. Na mimi Mhe. Spika, kupitia Baraza lako hili tukufu naweza kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa dhamira yake ya

kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata maji, wananchi wa Zanzibar wanapata huduma zote muhimu. Lakini anafanya *effort* kubwa ya kuhakikisha kila siku anatupa muongozo na maelekezo, kuhakikisha kwamba vitu hivi vinatekelezeka. *(Makofi)*

Nakwambieni Waheshimiwa Wawakilishi naomba mtuamini. Tunaomba sana mtuamini tunafanyakazi kwa imani kubwa, tunafanyakazi kwa ujasiri mkubwa, tunafanyakazi katika kuleta maendeleo ya nchi hii na kuhakikisha Zanzibar mwaka 2020 basi utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unafikiwa kwa asilimia mia moja. Naomba kuwashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Naomba utoe hoja Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nilikuwa naomba niwahoji wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya wizara, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU N01- WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI

Kifungu N0101	Ofisi Kuu Pemba
230,000,000	
Kifungu N0105	Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe
300,000,000	
Kifungu N0107	Kamisheni ya Ardhi
9,723,878,000	
Kifungu N0109	Mahakama ya Ardhi
100,000,000	
Kifungu N0121	Wakala wa Majengo Zanzibar
200,000,000	
	Jumla ya Fungu N01
10,553,878,000	

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU N01 - WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI

Kifungu PN

Mhe. Mwenyekiti: Haya Waheshimiwa naangalia kwenye orodha yangu na nitawapa watu watatu. Kwanza nitampa Mhe. Miraji Khamis Mussa, halafu nitampa, wengine mmesimama lakini hamkutoa nia ya kuzuia hili fungu.

Waliomo kwenye orodha na ambao wapo wima Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa hiyo nitakupa wewe, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf pia yumo kwenye orodha, wengine hammo. Mhe. Hamza Hassan Juma kwa sababu ni Mwenyekiti nitakupendelea nitakupa upendeleo kwa hiyo watu watatu wengine hammo. Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Haya nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia niliweka dhamira yangu ya kulizuia fungu hili ambalo linabeba mishahara ya viongozi na nilizungumzia suala la mshahara wa *ZAWA*. Nashukuru kwa Mhe. Waziri katika majibu yake alisema mwezi Julai haya malipo yataanza.

Sasa kwa kuwa mishahara mipya ilitangazwa Aprili mwaka uliopita sasa tunajadili na hawa haki zao lazima zianzie kule. Nilitaka kujua katika uanzaji huu yale malimbikizo ya huko nyuma tulikotoka hadi kufikia sasa maana karibu ana mwaka mmoja na miezi miwili. Serikali imezingatia vipi nataka kupata majibu ya wenzetu hawa ili haki zao zinazostahiki zinazoenda na sheria na ile kauli ya Mhe. Rais iwe imetekelezwa kwa vitendo. Naomba kauli ya serikali.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake kama ifuatavyo. Kwa kuwa utaratibu wa mishahara pamoja na kutangazwa na Mhe. Rais kwenye Shirika na Mamlaka ilikuwa na miongozo maalum, na miongozo hii kwa sababu Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikuwa inasimamia na kutoa miongozo, kwa hiyo sisi tulipopata miongozo ilibidi lazima tujipange.

Kwa hiyo, mimi ninachosema tutakaa na watu wahusika Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili watupe miongozo kama walivyotupa miongozo tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, miongozo inawezekana ikatoka lakini ukaja ukatoka muongozo ambao hawalipwi stahiki zao na watu walishatumikia taifa hili na dhamira ya Mhe. Rais watu wote wapate stahiki zao. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yupo atwambie tu na ndio kauli ya serikali tunayoihitaji hawa wafanyakazi wetu ambao wakwezi na wakulima wetu ndio watoto wao watazingatiwa vipi kupata malimbikizo yao. Kauli ya serikali iseme kwa sababu haki hii Mhe. Rais kaitangaza kwa wote ndio dhamira iliyopo sasa si jambo jengine.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba nimpe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Miraji Khamis Mussa atupe muda sisi

tutakaa wizara yetu na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati tukijaaliwa ili kulitafutia ufumbuzi suala hili. Penye haki zao tukijaaliwa watapata haki zao wala msiwe na wasi wasi serikali kamwe haitomnyima mfanyakazi yeyote haki yake. Hawa ni watu wa shirika tutakaa nao tujue utaratibu ule muongozo wetu unatekelezwa vipi tutasimamia kwa karibu na wizara inayohusika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Haya nainuka kwa mara ya tatu lakini naomba Mhe. Mwenyekiti, unilinde sana kwa sababu tunaowatetea ni wafanyakazi wa nchi hii. Kauli ya Mhe. Waziri nimeisikia na amekiri kuwa watakuja kulipwa haki zao, pindipo tutakapokuja kwenye Baraza jengine hamjalipa nini kauli yako waziri utakachokifanya baada ya kukumbusha hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Miraji Khamis Mussa afahamu kwamba ikiwa kuna haki zao watalipwa kisheria, lakini kama hazistahiki kisheria kulipwa hazitolipwa. Mhe. Mwenyekiti, tutakachofanya ni kutumia utaratibu wa kisheria na utaratibu wa kulipana kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilipata majibu kwa Mhe. Naibu Waziri katika suala lao la utawala kuhusu masuala ya nyumba ya wale vijana waliotapeliwa na akakiri kwamba matapeli hao wapo. Lakini akasema kwamba hata wale walionunua wamenunua kwa njia ya kimakosa. Sasa nimwambie tu kwa sababu sijaridhika na majibu yake. Mhe. Mwenyekiti, wale walipokwenda kwenye wizara waliambiwa waende na shilingi milioni karibu 18 kununua nyumba ya kilemba na wale hawajui mambo ya sheria. Kufika pale kwenye ofisi wakaambiwa walipe risiti waje wachukue baadae, kwenda baadae hakuna lakini wakati huo wameshapewa risiti kama ya shilingi laki 2 sijui ya malipo mengine wakaambiwa kwanza kaeni na hii inafaa.

Sasa ni lini nyumba zao wale kwa sababu utapeli ulifanyika ndani ya wizara kupitia ofisi yao na ni *official* kabisa watu wamekwenda kulipa ofisini risiti wakaambiwa hazipo kwa wakati ule. Nyumba ya yule mtu aliyetapeliwa atapewa lini. Hata kwa hiyo njia ya kilemba sio lazima amiliki, arejeshewe hiyo hiyo ya kilemba.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf swali lake kama ifuatavyo. Kama tulivyojibu katika suala letu la awali kwamba mtu yule ambaye alipeleka ile hoja pamoja na matatizo yaliyojitokeza lakini yeye mwenyewe hakupata ile nyumba kihalali. Katika kumbukumbu za Shirika la Nyumba kulikuwa kuna jina la mtu mwengine, kwa hiyo yeye alikuwa kaichukua ile nyumba kinyume na utaratibu, wamepeana vipi watajuana wenyewe.

Lakini sisi kama serikali kama shirika tutaendelea kusimamia sheria na tutaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa utaratibu jina lake halikuwepo, kwa hiyo na yeye alikuwa anataka kuiuza kwa mtu mwengine. Yeye anayetaka kuuza tayari jina lake halimo katika orodha ya waliokuwa wamepewa ile nyumba, ilikuwa kuna nyumba nyengine. Katika hali kama hiyo yeye hakuwa mhusika wa moja kwa moja wa ile nyumba, kwa hiyo hatuwezi kumpa ile nyumba kwa sababu sheria zetu hazituruhusu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf hapa alizungumza kufanya kazi kwa bodi kwa kushirikiana na bodi. Bodi ilifanya kazi na kufanya maamuzi sahihi na wakayaleta kwangu na mimi nikakubaliana na maamuzi ambayo bodi imefanya. Kwa hiyo, mimi nataka nimwambie kwamba ni kitu ambacho watu walikaa waliumiza kichwa lakini kwa mujibu wa utaratibu mhusika hakuwa mmliki halali wa nyumba hiyo.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Mhe.Mwenyekiti, kauli ya Mhe. Waziri siikubali hata asilimia ziro (0%) kwa sababu jamaa wana *document* kwa jina la mama yake mzazi ambaye amemnunulia ni jamaa wenye kabila za Kihindu na walinionesha na wamedhulumiwa kupitia wizara yake husika na mambo hayo yamefanyika ndani ya ofisi *official* kabisa. Na Mhe. Mohammed ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo kabla hatujatoka kwenye wizara yao, hili suala analijua na *document copy* nilimpelekea kwa jina la huyo mtu, leo inakuwaje aniambie kwamba huyo mtu sio mmiliki au hakumiliki yeye suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atoe maelezo sahihi na sio maelezo ya kudanganya umma, mimi nafanya kitu kwa ushahidi kuna watu wengi wametapeliwa lakini nimetetea huyu kwa sababu *evidence* zake ziko *right* kabisa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naongea kitu ambacho nakifahamu Mhe. Waziri aliyoongea yote hayapo sahihi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu ambacho taarifa niliyokabidhiwa na Meneja Mkuu wa Shirika na jibu ambalo nimepewa na Meneja Mkuu wa Shirika. Naomba muelewe kwamba taasisi hii haikuwa ndani ya wizara lakini muda mfupi iliyoletwa na baada ya kuja haya maswali tulikaa nao na ndio hicho alichotwambia. Kwa hiyo, mimi nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kama kuna taarifa yoyote ya ziada basi akubali kwamba tukitoka hapa atupe hizo taarifa alete hizo *document* tutakaa na watu wa shirika halafu tutalifanyia maamuzi muafaka baada ya kupata taarifa za pande zote mbili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nafikiri ushauri wa Mhe. Waziri wala sio mbaya.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi kuna vitu inakuwa sikubaliani navyo kwa sababu haiwezekani taasisi itoe taarifa za uongo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa amekupa nafasi kwamba tukimaliza hapa ukakae nae waziri yeye anazo za upande mmoja wa serikali wewe unazo hizo nyengine za upande mwengine, mkae na waziri ili aweze kukusaidia kulitatatua hili nafikiri sio ushauri mbaya.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi nataka akubali atoe kauli pindipo nitamletea …

Mhe. Mwenyekiti: Ndio kishatoa hiyo Mheshimiwa unataka kauli itoke hapo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Subiri usinilazimishe mimi silazimishwi hapa naelezwa, mimi nina *right* yangu ya kuzungumza huwezi kunilazimisha mtu. Mhe.

Mwenyekiti, atoe kauli pindipo nitamletea kwamba mtu amemiliki kweli yuko tayari kumrejeshea nyumba yake kilemba vile vile sio ya kumiliki kama ya kilemba alivyotapeliwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado inaanguka ndani ya ushauri wa Mhe. Waziri kwa sababu utampelekea na kama kuna haki ya mtu waziri yupo, na amekubali kukuona amekubali mjadiliane hili suala mimi nafikiri hapana tatizo hapo Mheshimiwa, mimi naomba tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, dhamana hii unaichukua wewe mimi usanii siupendi isiwe najibiwa hapa halafu tukifika nje tunakuja kuzungushana. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Hakuna tatizo Mheshimiwa naomba ukae. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ile Semina ya Wajumbe inahitajika sana. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa haitofautiana sana hoja ya Mhe. Miraji Khamis Mussa. Mhe. Miraji yeye alizungumzia hoja ya wafanyakazi wa mashirika, lakini mimi hoja yangu nazungumzia *specific* Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi na hili suala Mhe. Mwenyekiti nimeshawahi kulizungumza lakini bado kauli ya waziri kidogo nafikiri labda Mwanasheria Mkuu hili anaweza akanisaidia zaidi. Kwamba kweli Majaji wa Mahakama ya Ardhi wale *level* yao ni kama Mahakimu wa Mikoa.

Kwa hivyo, utaratibu wa stahiki zao zinatoka kama Mahakimu wa Mahakama za Mikoa. Lakini Mwenyemkiti wa Mahakama ya Ardhi yeye kwanza ni mteuliwa Mhe. Rais wakati wale Wenyeviti wengine wanateuliwa na Jaji Mkuu ni vitu viwili tofauti. Lakini huyu Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi yeye ni mtawala sio kama yeye anaendesha kesi tu, yeye ndio anaongoza ofisi nzima pale, sasa huyu leo unafika zaidi ya mwaka wa tatu ana-*claim* stahiki zake bado hazijapatikana.

Sasa inapofika pahala anasimamia kesi za watu wenye fedha nyingi sana katika masuala ya ardhi wao ndio wanaotoa hukumu, ikiwa stahiki zake huyu hajashughulikiwa inaweza ikapelekea ushawishi kitu ambacho sitegemei. Sasa hili nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu ajaribu kuangalia katika zile sheria zao, wale walioteuliwa na Jaji Mkuu na huyu aliyeteuliwa na Mhe. Rais ambaye amekabidhiwa ofisi kuwaendesha wale Wenyeviti wote wa Mahakama. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nakushuruku kwa kunipa nafasi kulijibu tena hili, na kama Mhe. Hamza Hassan Juma angeisoma kanuni ya 37 angejua kama kuna jambo ambalo limeshajibiwa basi halitakiwi tena kurudia ndani ya kikao chengine cha Baraza. Na hili nililijibu wakati wa Bajeti ya Wizara yetu Mhe. Mwenyekiti, nikamwambia Mhe. Hamza kama kwa sasa mafao ambayo analipwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi ni sawa na yale ambayo analipwa Hakimu wa Mahakama ya Mkoa. *(Makofi)*

Na nikaahidi Mhe. Mwenyekiti, kwamba hili jambo tunalichukua na tutakwenda kulitizama namna gani ya kulifanyia kazi. Kwa hiyo, Mhe. Hamza Hassan Juma

astahamili kwa sababu tumeshalisema hili atuachie halafu tutakuja kumjibu namna ambavyo tumelishughulikia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, unajua kauli ya waziri tu ndio kidogo ilinishughulisha na ndio maana nikasema nirejee, lakini kwa kuwa ameshaichukua mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu naamini haki itatendeka. Ahsante sana.

Kifungu PN0101	Programu Kuu ya Uendeshaji Na Uratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba Maji na Nishati	2,250,433,000

Kifungu PN01

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali namuona.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi vifungu vyote nimewekesha.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mpo wengi lakini kanuni inatwambia tuwape watu watatu tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Yangu mimi muhimu ndio yako hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Watu wote hao waliosimama jambo lao muhimu. Mhe. Machano Othman Said nitampa. Mhe. Ali Suleiman Ali pole, tuendelee Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati nachangia hoja hii katika programu hii ya utawala wa ardhi nilizungumzia kuhusiana na changamoto ya Skuli ya Kiwengwa na majibu ya Mhe. Waziri sikuridhika nayo, na sikuridhika nayo kwa sababu ardhi ni mali ya serikali, lakini pia mahakama ni ya serikali. Lile eneo lilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya wananchi wetu, lakini Mhe. Waziri kanijibu kwamba mmiliki wa eneo lile alikuwa mwananchi wa kawaida lakini pia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ikafuta ile hati na baadae mwananchi yule akaenda mahakamani na mahakama ikatoa uamuzi. Uamuzi uliotolewa pale ardhi ile imebakia ni matumizi ya yule mwananchi.

Lakini mimi nataka kujua kwamba eneo lile ni la wananchi ambao wametengewa kwa ajili ya skuli, wanafunzi wapo pale wanasoma na kuna masomo ambayo kiutaratibu wao yanahitaji wapate eneo la michezo. Na kama uamuzi umetolewa ni wa mahakama kwamba eneo lile ni eneo la mmiliki huyoe mwananchi wa kawaida. Je, wanafunzi hawa watatumia matumizi mengine kupitia suala zima la michezo katika eneo gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake kama ifuatavyo. Kama majibu yangu mama nilivyoyasema tumechukua *effort* mbali mbali ya kuhakikisha kwamba wananchi wale wanaweza kupata ile haki kwa sababu tunajua maendeleo ni kwa wote. Lakini katika suala zima la kuheshimiana tukasema tufuate taratibu za kisheria, tulikwenda pale Cairo mimi wakati ule na Mhe. Waziri wa Elimu na

Mafunzo ya Amali, lakini tumekwenda na sasa hivi ni Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mhe. Rashid Ali Juma tulitembelea kwa pamoja eneo lile kwa mkakati ule ule na kukaa na wananchi kuhakikisha kwamba suala lile tunalimaliza.

Lakini tumejaribu kutumia busara kubwa kuongea na mwenzetu pamoja na kwamba mahakama ilimpa haki, lakini baada ya kushindwa kabisa tukaliandikia suala lile kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili atupe utaratibu wa kisheria namna gani tunaweza kufanya ili kuweza kulikamilisha hilo.

Kwa hivyo, nimwambie tu Mhe. Asha Abdalla Mussa kwamba kazi tunafanya tumechukua hatua mbali mbali lakini busara na hekima ilikuwa inatumika. Na sasa hivi tunaomba wenzetu wanasheria watusaidie katika kuhakikisha kwamba tunafanyaje. Kwa sababu mihimili hii tukianza kugongana kila mtu kumuonesha misuli haitopendeza sana na ndio maana tukawa tunafuata utaratibu wa busara mkubwa, na ndio maana tukamuandikia mwenzetu Mwanasheria Mkuu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona namna gani tunafanya katika suala hili.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili amesema kwamba lipo kwa Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria Mkuu yupo naomba sana anipe ufafanuzi ili nifahamu kwamba suala hili litamalizika lini.
Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mhe. Waziri alichosema kwanza ni sahihi kiwanja hichi kilikuwa kina mzozo na mzozo ule mwisho wake ukafika Mahakama Kuu. Mahakama Kuu ikatoa uamuzi kuhusiana na kiwanja kile na uamuzi ule ukawa ni kubatilisha uamuzi wa waziri uliotoka wa kufuta ile hati. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka Sheria ya Ardhi Nam. 12 ya Mwaka 1992 kwenye kifungu cha 56 ilikuwa ikitoa utaratibu wa namna gani haki ya matumizi ya ardhi inatakiwa ifutwe na utaratibu wa kufuatwa.

Tumebadilisha kupitia *miscellaneous amendments* kwa kuondoa vile vifungu ambavyo vilikuwepo vya utaratibu ambao ulitakiwa kufuatwa na waziri wakati anatakiwa kufuta ile haki. Tatizo lililokuwepo wakati wa kufuta ile haki utaratibu ulikuwa haukufuatwa, ndicho kilichosema mahakama. Sasa wizara ilichotakiwa ni kwamba ipokee ile *order* ya mahakama halafu ianze kufuata utaratibu rasmi sasa wa kufuta kile kiwanja. Ndio maana hata sisi kwa sababu ya yale maamuzi yaliyotoka hatukuona kwamba kuna haja ya kukata rufaa.

Kwa sababu Mahakama ilichosema ni kwamba nyinyi mmefuta lakini hamkufuata masharti ya kifungu cha 56 kwa hiyo tunairudisha kwa mwenyewe na kama mnataka kufuta fuateni sasa utaratibu wa kisheria uliokuwepo. Uzuri wake sasa sheria tumeifanyia *amendments* na ule utaratibu mzima uliokuwepo kwenye kifungu cha 56 sasa umeondoka, kwa hiyo mimi nadhani tutakaa na wizara kuhakikisha namna gani sasa suala hili tutalishughulikia tena vizuri Mheshimiwa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba nimeshamfahamu na nimemsikia anasema yuko katika utaratibu watakaa pamoja ili wahakikishe suala hili linamalizika. Lakini nilitaka kumuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati anihakikishie kwamba ni muda gani utachukua kuhakikiasha kwamba huo utaratibu wote ambao ulitakiwa ufuatwe

utakamilika na wale wananchi nao wafahamu kwamba hizi changamoto zisije zikatokea tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdalla Mussa naliona kama gumu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Asha Abdalla Mussa lakini utaratibu itategemea na utaratibu wa kisheria ambao nitaelekezwa niufanye na ndio maana tuna-*seek advice* wakati wote ili tusije tukafanya kitu tofauti. Kwa sababu kiwanja hichi ni cha muda mrefu kimefutwa hata sisi hatujaingia humu ndani yeye hayupo na mimi sipo, lakini bado tunaendela kusimamia haki za watu na tutaendelea kusimamia haki za watu. Kwa hiyo, tukielekezwa tu na wanasheria wanaojua taratibu basi tutaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwenye hii programu ya ardhi ina *sub programs* mbili, lakini nitampunguza mmoja nawaongezea wawili, nitampunguza Mhe. Machano Othman Said ataingia Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.
Mhe. Suleiman Makame Ali: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sasa Mhe. Rais wa Zanzibar siku ya Mei Mosi kule Pemba alisema hivi naomba ninukuu: "Wananchi wasikae vibarazani na kunung'unika wawafuate Wawakilishi wao kuwapa kero zao ili wawatatulie". Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Ndagoni walinipa barua yao hii hapa kuhusu suala la mgogoro wa ardhi, lakini vile vile kuna karatasi feki mimi sisemi kama ni nyaraka hata Mhe. Waziri ameniambia kwamba si nyaraka ni matapeli hawa.

Kwa sababu huyu amesema kwamba shamba hilo ni lake akatoa mipaka yake na huyu akasema kwamba shamba hilo ni lake akatoa mipaka yake shamba hilo hilo moja. Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba Mkuu wa Mkoa ameshatengeneza mabango, aliyetengeneza mabango ni Afisa Mdhamini JB nampongeza sana kwa sababu ametoa pesa zake kutengeneza mabango yale ili kwenda kulinusuru eneo lile. Sasa nataka nijue ni lini mabango yale yatakwenda kuchomekwa ili na wale wananchi wajue kwamba lile eneo ni la serikali na hawa matapeli waliofanya tatizo hili kusababisha mgogoro huu waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kadhia hii imekuwa ya muda lakini kama nilivyosema kwenye majibu yangu mama na nitaendelea kusema kuwa katika kubandika mabango yale lazima Ofisi ya Mkuu ndio mhusika mkuu sisi tunatayarisha. Ndio maana nilisema kwamba Mkuu wa Mkoa
basi ataendelea kulifanya lile zoezi ndani ya lile eneo. Lakini kama ninavyosema wakati wote kwamba ofisi yangu ni wizara mama inayoshirikisha taasisi nyingi, ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi za Wilaya, Masheha lakini na wananchi wenyewe kwa sababu watakuwa wana dhamana ya kuyalinda yale mabango.

Kwa hiyo, bado naomba uamini kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndio itakuwa ofisi simamizi ya kuhakikisha kwamba mabango yale yanasimama na yanakaa katika maeneo ambayo tutakubaliana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na Mkuu wa Mkoa nina imani hilo watalikubali, na Afisa Mdhamini jembe yule pale namuamini sana. Lakini pia kwa jukumu la wananchi mimi nitalibeba kuwashajihisha na kuwahamasisha wananchi kuyalinda na kuhakikisha kulienzi eneo lile la serikali. Lakini bado Mhe. Waziri hajanijibu kwamba wale waliosababisha kutoa karatasi hizi na kusema kwamba eneo lile ni lao, wakati wanajua kwamba lile ni eneo la serikali. Ni hatua gani za kisheria za kinidhamu watapewa watu hawa. Hilo ndio nilikuwa nikilitaka zaidi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Suleiman Makame Ali shemeji yangu ameniletea zile karatasi na nilipozisoma zile karatasi bahati nzuri si karatasi, mimi naita karatasi mchele ni *photocopy*, lakini sio hati wala haki ya matumizi ya ardhi. Kwa hiyo, nikamwambia hivi vitu vya zamani ambavyo inaonekana inawezekana ni vya kwao, lakini inawezekana watu tu wameamua kutumia, bahati mbaya sisi hatuwajui yeye ndio anawajua.

Kwa hiyo, mimi naomba kama serikali ikishakuweka yale mabango mtu yeyote atatumia pale, wananchi lakini kupitia mwakilishi na kama mnaona kuna hatua ambayo mnataka kuichukua kwa hawa ambao mnawajua, basi sheria zetu ziko wazi mkashtaki, mkafungue kesi ili muweze kuwachukulia hatua. Sisi wajibu wetu kulilinda eneo kama ninavyosema ardhi ni mali ya serikali, basi tutaendelea kulilinda eneo kama walivyokiri wenyewe mabango yako tayari. Na Mkuu wa Mkoa mara tu tukimaliza hapa nitampigia kama nilivyompigia siku ile tuko mimi na wewe, basi achukue hatua ya kutuma watu wake wayasimamie yale mabango yakafanye kazi.

Mhe Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana shemeji kwa kunikubalia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwamba wale wananchi walinishtakia mimi kwa sababu mimi ndio Mwakilishi wao, na Mhe. Rais aliwaambia hilo kwamba nendeni kwa Wawakilishi mkawape kero zenu. Nashukuru walimsikia Mhe. Rais wao na walikuja, lakini sasa hao waliofanya wanatoka wizarani kwake na wananchi hawawezi kwenda kuwashtaki wale. Sasa yeye achukue jukumu la kuwawajibisha. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa dhati nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa majibu yao mazuri. Lakini pamoja na hilo Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikiri kwamba maneno aliyosema Mhe. Suleiman Makame Ali kwamba wananchi wetu wanatutegemea sisi tuwasaidie kero zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipochangia sikusema nitazuia fungu isipokuwa nitataka ufafanuzi kama sikujibiwa. Mhe. Waziri katika jitihada zake alijibu mambo mengi, lakini nilisifu habari ya maji, mkurugenzi nimemsifu na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye usimamizi wa upangaji wa miji na matumizi ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nilimtaka waziri atoe angalau maelezo mazuri juu ya wananchi wetu ambao wanapata shida kutokana na vibali vya ujenzi. Mwananchi anatoka Nungwi, Makunduchi, Uroa na Bwejuu anakuja *DCU* Makao Makuu mjini ni kero. Wakati sheria zamani au sijui ilibadilishwa vipi wilaya na manispaa walikuwa wanatoa vibali vile ili watu waendelee na shughuli zao bila ya matatizo

wananchi wetu wanyonge. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atoe kauli hapa. Je, utaratibu ule si vyema ukarejeshwa ili wananchi waondokane na adha.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, swali hili mara nyingi nalitolea ufafanuzi. Vibali vya ujenzi kupitia *DCU* vinapatikana katika halmashauri na manispaa zote, kila mtu akitaka kujenga kituo chake cha mwanzo katika halmashauri yake ambayo anataka kujenga hiyo nyumba au eneo ambalo anatoka. Kwa hiyo, pale ndipo anapopata fomu na fomu ile inauzwa shilingi 20,000/- na maelekezo yote atapewa kutoka katika halmashauri husika. Ndio maana *composition* ya *DCU* imewashirikisha Wakurugenzi wa Manispaa, Wakurugenzi wa Halmashauri zote na ndio maana kwenye halmashauri kuna ma-*engineer*, lakini kuna wataalamu kwa sababu ya kusimamia hiyo kazi katika kuendeleza mipango miji.

Kwa hiyo, nitoe wito tu kama Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi hawajui wapi pa kupata vibali vya ujenzi hatua ya awali unakwenda kwenye halmashauri yako na unairejesha ile fomu kwenye halmashauri yako ambayo umechukulia ile fomu yako. Kwa hiyo, mtu wa Makunduchi atachukua fomu yake katika Wilaya ya Kusini kwa halmashauri yake, lakini mtu wa Kati atachukua Wilaya ya Kati kwa maana ndio Halmashauri ya Kati na wa Magharibi ataichukulia Wilaya ya Magharibi na mjini ataichukulia Manispaa ya Unguja. Kwa hiyo, hizo ndio taratibu na halikadhalika kwa Pemba.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo sana lakini wazo langu liko kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililokuwepo ukienda huko wilayani huchukua muda mrefu kupata jibu kutoka *DCU*. Je, Mhe. Waziri, kwa nini hawatoi vibali pale pale na kila kitu ili mwananchi aridhike na malipo yake yalipwe pale na sio kwa *DCU*, ili kupunguza gharama na usafiri wa yule mtu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake kama ifuatavyo. *Infact* kila kitu kinamaliziwa wilayani, lakini kikao kile lazima kikae na ni hivyo kila wiki *DCU* inakaa, ilikuwa wanakaa kila wiki mbili, lakini sasa hivi kwa kurahisisha kila wiki wanakaa. Kwa hiyo, kinachotokea ni nini, yule Mkurugenzi anapokea fomu ambazo zimerejeshwa, wanatoa na zinarejeshwa, zikirejeshwa siku ya kikao kila Jumamosi anakwenda kikaoni na fomu zake, anawasilisha maombi ya wateja wake. Kwa hiyo, yeye akitoka pale anatoka na vibali vyake.

Mhe. Mwenyekiti, kama inaonekana kwamba wiki haifai, lakini kutokana na utaratibu wa *DCU* yenyewe ilivyo kusema wakae kila siku haiwezekani. Lakini tutazungumza ili tuone namna gani ya kui-*formalize* ili kila wilaya ambayo ndio lengo letu. Kwa sababu hii ilivyoundwa iliundwa taasisi moja, lakini sasa hivi kila wilaya tunataka iwe na *DCU* yake. Tunajitahidi kuwashawishi wataalamu wetu ili tuwe na wataalamu wengi wa maeneo yote kwa sababu *DCU* pia inahitaji watu wa majengo, ma-*architecture.* Kwa hiyo, yote hayo tutafanya sasa hivi katika kuboresha hizi huduma mitaani *decentralization* basi wawepo pale ili hizi *DCU* ziweze kuwa pale. Lakini ni mpango ambao bado hatujauandaa, ni vitu ambavyo tunavifikiria.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe, basi bado aridhie kwamba watu wachukue fomu wilayani lakini na kibali kinatokea pale pale kwenye halmashauri,

lakini *just for the week*. Kama kuna vibali vinavyochelewa inawezekana wakati mwengine mtu ana kibali kimoja au viwili, basi inawezekana akaona asipeleke lakini mimi najua kwa wiki haiwezi kuzidi wiki mbili vibali vinapatikana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo. Tuendelee namuombea dua Mhe. Waziri afanye chapu chapu ili wananchi wetu wafaidike mitaani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi mambo yangu ni mawili hapa. Jambo la mwanzo nilizungumza kwamba na niliweka nia hasa ya Kamati Teule kwenye suala hili. Viwanja 33 alivyovitoa Mhe. Rais …

Mhe. Mwenyekiti: Jambo moja tu lakini nakupa. Katika hayo mambo yako mawili zungumza moja tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Katika viwanja alivyovitoa Mhe. Rais 33, kwanza nimpongeze sana kwamba vimeweza kutoka, lakini nafasi ile ile ya kauli ya Mhe. Rais, Mhe. Waziri alipeleka na yeye majina ya watu anaowataka akatoa viwanja vyengine. Sasa ni hivi alivyovitaja katika 22, wamo waliopewa ambao walioomba wa kikweli kweli wa kibinaadamu wa kusaidiwa ambao wamepata mambo ya maafa wengine walipewa, lakini kuna wengine yeye ndie aliyewapeleka kama yeye. Sasa namuomba anitajie majina ya wamiliki wote wa hivyo viwanja walivyovitoa humu ndani ili tuhakikishe kweli waliopewa ni wanyonge ama watu wake yeye.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hilo mimi silikubali pia kwa sababu haliwezekani. Kwa sababu Mhe. Waziri akupe *list* sasa hivi. Hapa tunapitisha vifungu vya pesa kwa ajili ya matumizi, unamwambia waziri akupe *list* ya watu wote aliowapa viwanja avi- *produce* hapa sasa hivi. Ni ngumu sana Mhe. Mjumbe, haiwezekani. Kwa sababu haliwezekani naomba tuendelee, tunaendelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, viwanja 22 sio vingi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba tuendelee viwanja 22 ni vingi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, wananchi unawaonea. Mimi nazungumza suala lina *point*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe naomba ukae. Naomba tuendelee.

Kifungu PN0102	Programu Kuu ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi	3,459,511,000

Kifungu PN0105

Mhe. Mwenyekiti: Naanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, haya mko watatu, Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa jinsi unavyoliendesha Baraza lako kwa umakini wa hali ya juu na unaendelea. Niwaombe tu Waheshimiwa Wenyeviti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar wajaribu kujifunza kutoka kwako katika hoja kama hizi tatu

mbili kuziongeza za wananchi. Nakuombeni kwa heshima kabisa Waheshimiwa Wenyeviti mjifunze kutoka kwa Mhe. Spika.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni ya muda mrefu. Kuna kadhia ya nyumba moja ya Bohora mmoja anaitwa Ismail Tayaballi iliyokuwepo Chake Chake, amepewa nyumba hiyo gharama yake shilingi milioni 88 kuuziwa na serikali, Wizara ya Ardhi chini ya waziri aliyepita. Hiyo nyumba nusu imeshaanguka na nusu haipo, amehangaika kwa muda mrefu kufanya mazoezi ya kupanda na kushuka kwenda na kusini, mvua jua, usiku na mchana, analalamikia bei inapunguzwa milioni 88. Nyumba uasili wake ilikuwa ni yake mwenyewe iko Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri alipokuwa akijibu ataendelea kusimamia haki ndio kwa mujibu wa wizara yake, alisema sio muda mrefu maneno hayo. Kwa hivyo, tunataka ufafanuzi wa suala hili, maelezo ya serikali ninayo milioni 88 alichokuwa akilalamika kwa muda mrefu ni kupunguziwa bei tu nyumba hiyo ambayo ni mmiliki iliyoko Chake Chake Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani Mhe. Waziri ameshafahamu. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake kama ifuatavyo. Ni kweli aliuliza hilo swali na mimi nilimpigia simu kutaka ufafanuzi, kama kawaida yangu mimi na Jaku nikazungumza nae nikamwambia anifahamishe kwa sababu suala hilo sijawahi kulisikia ndio kwanza nimelipata kutoka kwake. Akaniambia na akanieleza aliyonieleza kwamba huko nyuma waziri aliyekuwepo kulitokea hiyo kadhia kwamba bei aliyoitoa kubwa. Lakini baada ya kufuatilia na taarifa nilizopewa na wizara yangu kwamba nyumba hiyo kwanza ni mali ya serikali ilitaifishwa nyumba hiyo mwaka 1964 na ikawa ni mali ya serikali. Hilo la kwanza.

Kwa hivyo, alivyoniambia kwamba huyo Bohora ndio mmiliki, nikamwambia yeye sio mmiliki kwa sababu tayari imeshataifishwa, kwa hiyo bado itabaki kwenye mikono ya serikali. Lakini mtu huyo mimi simjui anaitwa *somebody* Nabawal akasema kwamba alitaka auziwe na nyumba ile ikafanyiwa tathmini ni nyumba ambayo ni sinema ya Chake Chake, kwa wale wa Chake Chake wanaijua. Kwa bahati nzuri nimekaa Chake Chake hilo jengo nalijua, alivyoniambia tu Chake Chake pale barabarani karibu na Skuli ya Madungu. Kwa hiyo, nikamwambia nimelipokea na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kulisikia kutoka kwako, nipe muda ili tukae mimi na wewe tulitafutie ufumbuzi na tulifanyie kazi. Lakini tathmini iliyotiwa na wizara yangu wakati huo ilikuwa ni milioni 88, kwa hiyo bado itaendelea kuwa ni tathmini halali mpaka hapo itakapofanywa *review*.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yangu mama nilimwambia kabisa kuwa nimelipokea na namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub aniachie ili niweze kulifanyia kazi kwa kushirikiana na yeye kwa sababu yeye ndiye mwenye *document* zote. Kama kawaida nasema mimi na Jaku namwambia wewe niletee, mimi na yeye tunapeana kwa hiyo hakuna shida tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wewe na Mhe. Waziri mna mawasiliano mazuri sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema "maneno mazuri humtoa nyoka pangoni", lakini mdomo na vitendo tofauti. Mdomo utazungumza vingi lakini vitendo ndio kuna kazi, na "ukitaka kitu cha mvunguni ni lazima uiname".

Mhe. Mwenyekiti: Twende kwenye hoja Mhe. Mjumbe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwenye hoja. Hiki kitu kiko wazi wala hakitaki tochi kumurika, hata Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Hamza Hassan Juma hili suala analijua kwa muda mrefu walihangaika nalo sana, nimshukuru sana Mhe. Hamza kwa suala hili. Lakini ilifika pahala wale walionituma ni majirani zangu kwa muda mrefu wanaona kama hii kazi yao siifanyi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake ni kupunguziwa bei tu hii shilingi milioni 88 na Mhe. Waziri kajibu vizuri nimpongeze kwa dhati kabisa. Hoja ni hii milioni 88 apunguziwe na hiyo nyumba ni kama anaomba kiwanja upya tu. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, anaomba punguzo tu la bei shilingi milioni 88 umshushie sijui. Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nirejee, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alivyoniambia nilimwambia kwa sababu tathmini imefanywa kitaalamu na tathmini ile inafanywa kwa mashirikiano, kwamba wafikia tathmini ndio wanaofanyakazi. Kwa hivyo, nilimwambia basi alete ili nikae nao, tulifanyie kazi na tuone kama tunaweza ku-*review* bei. Kwa hiyo, bado naendelea kumwambia kwamba nafasi yake ipo kama kawaida yake, ailete tukae pamoja ili tuone namna ya kumsaidia huyo mtu kama inawezekana. Lakini nasema sijui tathmini iliyofanywa iliangalia vigezo gani. Kwa sababu niseme ile nyumba mimi naijua sinema ya Chake Chake nilikaa Madungu. Kwa hiyo, lile jengo ni la zamani lakini lina hadhi yake na lina haiba tofauti na majengo hata haya yanayojengwa leo, inawezekana kuna vitu ndani yake vimeangaliwa.

Kwa hiyo, yote haya nilimwambia akija akileta tutakaa na watia tathmini, lakini na hawa wasanifu wa majengo, basi watuambie kwa nini bei ile imekaa hivi halafu atapata jibu, na kama kuna uwezo wa kuweza kuona tunapunguza basi tutafanya hivyo. Lakini ni lazima kwanza tuheshimu hayo maamuzi halafu tutajua nini cha kufanya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri inaeleweka. Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa sababu inaonekana kwa mujibu wa maelezo shilingi milioni 88 ilikuwa ni ya lile jengo, sasa wewe unasema jengo halipo pana kiwanja kitupu. Sasa kwenye hilo kaa na Mhe. Waziri halafu muone ni namna gani mnaweza mkalimaliza hilo, nafikiri hata hilo suala la bei serikali kwa sababu inawahudumia wananchi, nadhani wanaweza wakaliangalia hilo. Mimi naomba tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ushauri wako na nitakaposhindwa nitarudi tena kwako utakuwa kama mwanasheria wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Karibu sana. Tunaendelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bado mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Eee! Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nimekusahau.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, lile la mwanzo umelikataa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nenda kwenye hoja usianze kubishana na kiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Hapana, nakuja jengine usije na hili ukasema pia halifai. Mhe. Waziri tokea kaingia kwenye madaraka kafuta sehemu mbili au kavifuta viwanja karibu viwili, halafu kaweza kuwapa watu wengine. Sasa atueleze viwanja vilivyokuwepo Kwa Mchina pale vinne alivyoongea Mhe. Abdalla Ali Kombo, viwanja vile vinne atutajie majina ya watu aliowapa kwa sababu ni watu wake wa karibu kawagaia viwanja vile. Tunaomba majina ya watu wale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nafikiri sio pahala pake hapa. Hapa tunapitisha vifungu Mheshimiwa. Jambo hilo ilikuwa ulilete kwenye mchango wako ulizungumze, lakini wewe hukulidai kwenye mchango, umeli-*raise* sasa hivi baada ya kukukatalia yale mengine majina 22 uliyoyataka ndio maana sasa hivi unataka majina mengine manne. Kwa heshima na taadhima naomba kulikataa na hili pia ili tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said nilikusahau.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa mimi nataka pia hoja hii niiondoe nije katika fungu 0105.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu PN0103	Programu Kuu ya Uhifadhi na Uimarishaji wa Makaazi	1,442,300,000

Kifungu PN0105

Mhe. Mhe. Mwenyekiti: Haya, Mhe. Machano Othman Said nitakupa nafasi ya mwanzo, kuna watu huwa siwaoni sana kusimama simama, mheshimiwa nitakupa, halafu Mhe. Omar Seif Abeid. Haya tuendelee Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesimamia hoja kuhusu maji. Mhe. Waziri bahati nzuri alijibu maswali na sina hamu sana ya kuzuia kifungu cha waziri kwa sababu wengi ni rafiki zangu na wengine ni wanafunzi wangu wa siasa kwa hiyo sitaki kuzuia fungu. Isipokuwa katika majibu ya Mhe. Waziri katika mchango wangu nilizungumzia visima vya Bumbwisudi, visima vya Ras Al Khaimah na Mradi wa India. Kwa bahati nzuri nazungumzia hili kwa niaba ya majimbo sita, Jimbo la Mfenesini, Jimbo la Bububu, Jimbo la Mtoni, Jimbo la Mtopepo, Jimbo la Welezo na Jimbo la Mwera, bahati nzuri watatu ni mawaziri hawawezi kuzungumzia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Magharibi "A" ndio ambayo inazalisha maji zaidi ya asilimia sabini kwa mji wa Unguja. Nataka Mhe. Waziri atuweke wazi. Kwanza, kuhusu visima vya Bumbwisudi, visima vyote tisa maji yanakuja mjini moja kwa moja bila ya kupata Wilaya ya Magharibi "A". Pili, Mradi wa Ras Al Khaimah ambao Mhe. Waziri amesema kwamba visima karibu 30 vitatengenezwa au 20. Je, vipo vya wilaya hii maana yake mimi jimboni kwangu kuna visima sita vya Ras Al Khaimah na hakuna hata kimoja kinachofanya kazi. Tatu, kujua huu Mradi wa India ambao tumeanza kuusikia tangu mwaka jana unatarajiwa lini kufanya kazi na ramani yake ikoje katika mradi huu wa India. Ni hayo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini swali lake kama ifuatavyo. Kwanza, naomba nimjibu kuhusu visima tisa vilivyochimbwa Bumbwisudi. Visima vilivyochimbwa Bumbwisudi ni vya mradi, ni visima ambavyo vinapeleka maji Mkoa wa Mjini na Magharibi, lakini katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika *mapping* ya ule mradi maji yanakuja mjini na kuna *path* za Magharibi ambazo zitapata maji. Bumbwisudi na Mfenesini haimo katika visima vile, Mhe. Machano namuelewa sana kwa sababu na mimi ni mdau wa Magharibi "A" kwamba basi angalau visima viwili vipelekwe kule.

Lakini kuna miradi ambayo nilishaainisha na nilikwisha isema muda mwingi kwamba yenyewe itasambaza maji kule ukiwemo mradi huu wa India lakini pia na ule *ADB* kuna sehemu inakwenda kule, lakini na mradi wa Wachina ambao utapeleka maji Miwani utakuja ku-*serve* mpaka Kizimbani na maeneo mengine ya karibu.

Kwa hiyo, hizi kazi zote zinafanya *integrated* kwamba sio kama kipo hapa lazima yawepo hapa, lakini pia *scheme* ya mradi inatokana na ile *project concept* ambayo iliombewa zile pesa. Kwa hiyo, hili nilikuwa najaribu kumfahamisha sana wakati mwengine tunaweza kujenga nyumba hapa lakini matumizi yake yakawa si ya mtu wa hapa.

Kwa hiyo, hayo yote ile *project concept* ndio inayo-*indicate* wapi iende nini na kipi kiende wapi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe tu kwa kuwa nia yetu ni nzuri na dhamira ya serikali hii ni nzuri na haya yote ni *effort* ya Mhe. Rais wetu kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata maji safi na salama. Hata mimi inaniuma kwanza niseme ukweli Magharibi "A" *it's my own area* kwamba ni *part* ya maisha yangu. Kwa hiyo, nilimuelewa na nilipiga kelele sana tuchukue kisima, yeye aliomba viwili mimi nikaomba hichi kimoja kwenye mradi, lakini *mapping* ikanikatalia. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Machano Othman Said aridhike na mipango ya serikali kwamba maji yatakwenda mjini na *path* za magharibi na ile miradi mingine itakwenda katika maeneo ya kwake, naomba aridhike.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri kwamba hatupati Bumbwisudi watu wa Jimbo la Mfenesini, lakini bado nilitaka kujua katika hayo mategemeo au matarajio ambayo tunaahidiwa hapa ya mradi wa India hebu atueleze Mradi wa India unapita sehemu gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa India ni mpana kwa ujumla wake, kwanza ina-*cover almost the whole* Magharibi, inakwenda inashuka mpaka Tunguu, inakwenda *parting down* to Fumba, lakini

pamoja na Magharibi. Halafu kuna *a score part* ya mjini ile mitaa ya juu kule ya ng'ambu ya juu kama Welezo lakini bado magharibi sio mjini ina-*serve a small part*. Kwa hiyo, labda kimoja ambacho nitakifanya siku ambayo tutafanya semina ya *policy* ya ardhi na *land use plan* na kuwaonesha vile vitu vyengine kwenye ardhi niombe nichukue jukumu kwamba na watu wa maji basi nije waoneshe zile *mapping* za miradi yote.

Kwa sababu labda Waheshimiwa wakiona zile *mapping* wataona namna gani ile *concept* ya *project* zilivyo na wapi na wapi itafika, lakini India *it's cover a lot* na sasa hivi tuko vizuri kama nilivyojibu katika swali lako la awali na fedha imeanza kutumika na Mshauri Elekezi anafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, mimi niombe tu kwa sababu bado tupo katika *schedule of work* ambayo hatujachelewa tuko vizuri, basi muendelee kutuamini tuweze kulifanyia kazi. Siku hiyo ya semina mimi nitaomba na watu wa maji waje ili muweze kupata hiyo *concept* na muweze kujua kwa undani kabisa kila kitu ambacho kitakuwepo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Machano Othman Said nadhani utakuwa umeridhika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo sitaki kuzuia shilingi, naunga mkono sana serikali yetu lakini tunawawakilisha wananchi wanatakiwa wajue nini kinafanywa kwa ajili yao, kwa maisha yao na kwa maendeleo ya nchi yao. Sasa Mhe.Waziri nilikuwa nakuomba nafikiri hili utalikubali ufanye semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi uje na *mapping* yako kwa sababu miradi ya maji ni mikubwa na inagharimu fedha nyingi za serikali na wafadhili, ili kila Mwakilishi aweze kujua mradi huu mfano wa India unapita wapi, utasaidia nani na watu kiasi gani, ili na sisi tuweze kuwaeleza wananchi wetu kwa sababu wananchi wana subira kubwa ya maji. Ukienda kuwaeleza wananchi kwamba kuna mradi huu utapita hapa na hapa basi wananchi na wao watatulia na serikali itaweza kufanya mambo yake, lakini lazima kwanza sisi tupate elimu ya kuelewa hiyo miradi yenyewe ikoje.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe.Waziri semina ya maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Nimepokea ushauri wake na nitalifanya hilo ambalo amenishauri.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia Mhe. Waziri namshukuru kajitahidi kunijibu lakini kuna jambo moja hakuweza kunijibu. Nimesema hivi, mwaka 2015 wananchi wa Kidoti walichimba kisima pale kwao Afisa wa Wilaya alisimamia, lakini katika kukamilika kisima kile pesa zikapungua wananchi wale kwa pamoja wakashauriana kwamba wakope kwa miadi kwamba *ZAWA* watalipa baada ya kukamilika. Sasa mwaka wa tatu pesa zile hawajalipwa, nilitaka maelezo ya kina watalipwa lini pesa hizi. Pesa ni shilingi 1,110,000/- nimezisema leo mara ya tano.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Ame Haji Ali swali lake kama ifuatavyo. Naomba nilipokee na najua hiki kisima kilijengwa kwa dhamira njema na Mkuu wa Mkoa na watu akawafanyisha kazi wakati ule anakaimu Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud na bahati nzuri kisima kile kimekabidhiwa *ZAWA.* Lakini wakati tumekabidhiwa tulikuwa hatujakabidhiwa yale madeni. Lakini kupitia kwake kwa sababu la

mwisho alisema nafikiri sijui kwa nini sikulijbu, lakini nijibu kwamba acha nilipokee hii pesa shilingi 1,110,000/- sio nyingi, basi tutaweza kuifanyia kazi tutaihakiki tu, tupate taarifa za uhakiki kama ni sawa basi tutazilipa hazina shida yoyote bila wasi wasi wowote na kwa muda mfupi. Na kile kisima nimwambie kwamba sisi tumekipokea *ZAWA* kilichimbwa huko na Mkuu wa Mkoa kwa mashirikiano na wananchi lakini sasa hivi wametukabidhi sisi, kwa hiyo sisi tutakitumia vizuri. Hili nimelipokea na nitalifanyia kazi.

Mhe. Ame Haji Ali: Nashukuru Mhe. Waziri kukubali kulifanyia kazi yeye, mimi nishachoka kuzungushwa na watu wa *ZAWA.* Kwa kuwa amekubali kwamba atalifanyia kazi yeye na nadhani wananchi wa Kidoti sasa wananisikia nitakwenda kwake ili tulimaze jambo hili. Ahsante tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi. Mheshimiwa mimi wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwamba nina nia ya kulizuia fungu la *ZURA* linalohusiana na programu hii, tukitilia maanani kwamba mwaka jana walipewa shilingi bilioni 41 lakini mara hii wapo shilingi bilioni 91. Nikaliona hilo na nikaelezea sababu zangu za msingi kwamba wao ni waratibu sio watoa huduma, wanatoa tozo sehemu nyingi na pesa zile hatuoni miradi ya maendeleo ya wananchi iliyofanywa. Lakini kwenye kifungu HN 01050106 wamesema kwamba wataimarisha miundombinu ya maji mijini na vijijini kwa kutilia mkazo hilo wamewekewa shilingi bilioni 44. Sasa nataka nijue ni miundombinu gani hiyo ya maji ambayo amepanga kuitekeleza kuisimamia kwa pesa zote hizi wakati wanaonunua hizo ni *ZAWA* na vifaa hivyo vinanunuliwa na *ZAWA.*

Lakini kama wanasimamia hayo maji safi mimi katika kisima changu cha Konde nilizungumza hapa kwamba maji yaliyokuwa yanatoka Konde hayawezi kunyweka na wao wapo. Nataka nijue ni hatua gani waliyoichukua wa kuyasimamia ili wale wananchi wa Konde wakayapata yale maji safi na salama. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu swali lake Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo. Kwa kweli hizi fedha zilizokuwepo hapa hii ni *sub* sijui Kiswahili nisemeje, yaani ile *component* nzima ya *program* ina *program* nyingi chini yake. Kwa hiyo, hizi shilingi bilioni 44 ni za mamlaka sio za *ZURA,* lakini kifungu chote kinakuwa ndani ya programu kuu halafu programu ndogo ndogo. Sasa hizi programu ndogo ndogo ile 44 aliyoisoma hapa ya miundombinu ni mamlaka ya maji *ZAWA* katika kuimarisha sio ya *ZURA.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nimfahamishe kwamba programu ile inakuwa ni moja ambayo inaitwa *sub program* ndio maana ukaiona hapa. Na katika hii programu ina vitu vingi hata Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* iko hapa, *ZPRA* iko hapa kila kitu lakini imo ndani ya taasisi moja. Naomba kumuelewesha hivyo Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa sawa hilo nimemuelewa nilitaka nijue *ZURA* kwa kuwa wao ndio wasimamizi kwa upatikanaji kama hicho kifungu nilichokisoma ambacho hakuniambia. Kukuza huduma za maji safi na salama na wao ndio wasimamizi na kisima kile kinatoa maji machafu kama maji ya mto, na juzi katika swali walikiri Naibu Waziri wao *ZURA* wapo na moja ya jukumu lao ni hili. Vipi wataendelea kuhakikisha hili kwamba kisima kile kinatoa maji safi na

salama kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Jimbo la Konde kwa usalama wao. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu tena kwa mara nyengine Mhe. Omar Seif Abeid rafiki yangu, kwamba suala hili la la kisima kile cha Konde ambayo maji tulikuwa tuna wasiwasi na *iron luxcine* tulianza Chake Chake tukenda kule. Lakini kisima kile *ZAWA* wenyewe hawajashindwa. Lakini *ZURA* katika suala la usimamizi na huduma wao wanajaribu kudhibiti kodi, wanajaribu kudhibiti huduma kuona huduma zinapatikana, lakini wanashauri katika utaalam. Ndio maana *last time* kama mtakumbuka nilijibu kwamba pia kuna vikao vya pamoja hizi bodi zote zilizokuwa chini ya taasisi mara nyingi zinakaa pamoja katika kuangalia changamoto na kuona mwelekeo unakwendaje katika kufanikisha hizi kazi. Lakini bado *ZAWA* inafanya kazi zake na jukumu la kuhudumia visima na kuvisafisha visima.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Omar Seif Abeid nafikiri kwa sababu sijui kama unajaribu kuchanganya vitu tofauti au vipi, yaani hata na mimi nilikuwa sielewi kidogo. Yaani kazi za *ZAWA* sasa unataka zifanywe na *ZURA*, wale ni wasimamizi tu *regulators, ZAWA* ndio wanaofanya hiyo shughuli ambayo wewe unaidai hapo. Hebu tuachie tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu nilitaka wale *ZURA* maana yake nilizungumza kama tozo wanazozitoa hazirudi na ndio maana nikawa nipo huko. Lakini kwa sababu Mhe. Waziri mimi namuamini kwamba akisema jambo lake anatekeleza, nataka nione hilo kwamba *ZURA* kile wanachokitoza maslahi yake nayo yanarudi *direct* kwa wananchi kwa mpango kama huu wa kuwasimamia wananchi wetu. Ahsante sana tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani wameshasikia, halafu kuna Waheshimiwa wawili kila mara mnasimama. Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Mhe. Viwe katika *list* niliyonayo programu ambayo ina jina lako ambayo ulitia nia ni moja na ni ile ya mwanzo na hukusimama wakati ule. Sasa unataka kusimama kwenye programu ya nne ambayo hamna jina lako silioni, hilo moja. Mwengine ni Mhe. Nadir nilidhani tulikwisha kumaliza Mheshimiwa nilikwisha kukunyima nafasi tena huwezi tena kunyanyuka kulazimisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, haya mawili sasa hivi muhimu sana ya wananchi na nimeweka nia vifungu vyote mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeshamaliza Mheshimiwa kwa sababu ni watu watatu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Hapa sijaongea mimi na una fursa Mhe. Mwenyekiti, ya kuongeza mtu mmoja kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio ninayo nafasi hiyo lakini naomba hiyo nafasi nibaki nayo mwenyewe nisikupe. Mhe. Viwe Khamis Abdalla bado hujaridhika. *(Makofi)*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, samahani ukinizuia kuisemea kero ya wananchi hapa utanionea ndipo nilipopiga hii hapa mimi nilisema kifungu

PN00 nilipokuwa nachangia, kabla sijachangia nilisema *Bismillah Rahman Rahim* nikaanza na kifungu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nina *list* hapa, *list* ina jina lako.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Labda hao walikosea lakini nia yangu nilizuia hapa, na hata Mwenyezi Mungu alisikia. Mhe. Mwenyekiti, nakuhehimu naomba unipe nafasi ya upendeleo kwa sababu gani, kero ya wananchi wangu nitakuwa sijaisemea na ndio hapa tu sina buti jengine, hapa tu.

Mhe. Mwenyekiti: Inahusu nini Mheshimiwa, niambie mimi Mwenyekiti inahusu kitu gani ili kama naweza kukupa upendeleo naweza kufanya hivyo lakini nilijue hilo jambo lenyewe linahusu nini.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Waziri alipokuja alijibu lakini alijibu kuwa bomba wenye mamlaka ya kununua ni wizara yenyewe pamoja na mashine. Kwa hiyo, mimi mwenyewe bado sijaridhika na majibu yake aliyonipa, nataka anipe kauli ili wananchi wasikie kwa sababu imeshakuwa kero ya muda mrefu, *hansard* za miaka mitatu hizi hapa tokea mwaka 2015. Hapa nataka kauli ya serikali leo wananchi wasikie huu mwezi wa sita maji hawapati. Mhe. Mwenyekiti, naomba unipe ruhusa.

Mhe. Mwenyekiti: Wananchi wepi hao, wa wapi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwakilishi wa Viti Maalum nasimamia Mkoa mzima wa Kaskazini Pemba, wananchi wa Kiuyu Minungwini nilipozaliwa, pale nilipozikiwa kitovu changu.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani majibu yalitolewa umesema hujaridhika nayo, basi nimpe waziri. Hebu waziri mtosheleze kidogo Mhe. Viwe Khamis Abdalla.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, labda nimjibu tena Mhe. Viwe Khamis Abdalla swali kale la Kiuyu Minungwini ambalo kila siku tumekuwa tukilirejea. Ni kweli kwamba limechukua muda lakini kwa utaratibu ambao tulikuwa nao. Sasa hivi *pump* ya Kiuyu Minungwini imo ndani ya mikono ya Afisa Mdhamini wa Pemba, Ndg. Mshindo. Kwa hiyo, ni jukumu sasa la kwao na wameniahidi baada ya bajeti hii itafungwa, sasa nimuombe Mhe. Mwakilishi tukitoka hapa Mshindo yuko juu basi akae nae aone kwa sababu tayari imeshafika sio zile ambazo bado hazijafika, ilikuwa katika *lot* ya kwanza na tayari ipo. Kwa hiyo, akae nae aone ni lini wataweza kuifunga lakini *pump* ya Kiuyu Minungwini ni suala la muda mrefu hata sisi kama tunavyosema tunalijua na tunalifanyia kazi kwa umakini sana. Basi ndani ya mwezi Julai mimi naamini kwa nilivyoambiwa kwamba itakuwa imefungwa na yeye aendelee kuisimamia kupitia Mkurugenzi Mkuu *ZAWA* Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Mheshimiwa naomba tuendelee itoshe hiyo basi. Mheshimiwa kanuni zinaruhusu watu watatu tu mimi nimekupa upendeleo unataka kulazimisha, hebu kaa na Mhe. Waziri na watendaji wake.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, tupo hapa kuisimamia serikali, sijaridhika na majibu aliyonipa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi naomba ukae basi, Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Sawa tuendelee lakini sijaridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu PN0105	Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati	91,252,043,000
	Jumla Kuu	**98,404,287,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bia ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa japo naona haikuungwa mkono, lakini sasa nitawahoji wale wanaoiunga mkono hii hoja wanyanyue mikono yao, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, niwashukuru watendaji kwa mashirikiano ambayo wameyatoa, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu.
Waheshimiwa Wajumbe tunapokuwa tunachangia nitakumbusha tena tuwe makini sana na vile vifungu ambavyo tunataka kuvizuia huwa mnatoa nia tu nataka kuzuia kifungu fulani, lakini kazi niliyowaachia Makatibu Mezani hapa ni kwamba mtu akitia nia tu ya kukizuia kifungu anaorodheshwa ndio utaratibu ambao umefuatwa na orodha ilikuwepo pale kwenye meza.

Lakini si hilo tu, kanuni zetu sasa kwa kila kifungu hatuwezi kuhoji zaidi ya watu watatu tunafanya tu kama upendeleo ni mambo ya siasa tu, najua na mahitaji huko mitaani tunasema basi tunaruhusu mtu wa nne au wa tano. Lakini sasa inapotokezea kama hivyo halafu sasa Mwakilishi anataka kulazimisha lazima ile ihsani iliyotolewa sasa anataka kuitumia kwa nguvu, sasa hapo inakuwa ndio mnapata hayo mavutano na viti ambayo sio nzuri sana, Waheshimiwa Wenyeviti wanajitahidi. Mimi nadhani Mhe. Jaku Hashim Ayoub hapa alikuwa anazungumza kwamba labda waige mfano sote bado tumo katika kuendelea kujifunza, hata mimi Spika vile vile sio bingwa wa kanuni, Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma nadhani yeye ni bingwa wa kanuni kuliko mimi Spika kwa sababu yeye ni mwalimu na ameshaihifadhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kazi ambazo wanakuwa wanafanya hapa wanahitaji sana mashirikiano yenu ili kuweza kulisimamisha hili liende vizuri. Haya mambo pamoja na ubingwa unaokuwepo lakini yanakuwa yana mitihani maana yake muda mwingi sana inabidi itumike hekma kum-*control* mtu ambaye amehamaki yuko kwenye hasira kujaribu kumleta chini ili waweze kuwasiliana na serikali. Wakati mwengine Serikali ndio inakuwa kali Mawaziri wakiwa wakali unajaribu kucheza na *balance*. Kwa hivyo, Waheshimiwa kubwa ninaloomba ni kupewa mashirikiano lakini zaidi tuzizingatie kanuni katika kufanya shughuli zetu, wakati mwengine tunazipinda kwa nia njema tu kanuni kwa ajili ya kuruhusu faida kwa ajili ya wananchi. Kwa hivyo, tunawapa watu hiyo ziada ambayo ipo. Lakini ikitokezea Mwenyekiti anahisi wakati mwengine pia tunacheza na wakati.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe mimi nishukuru sana kwa mashirikiano ambayo tunayapata kutoka kwenu, muendelee kutupa mashirikiano ili tuendeshe Baraza letu kwa uangalifu sana. Baada ya hayo, sasa nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Fedha na Mipango

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018-2019.

Mhe. Spika, kama ulivyo utaratibu wetu, naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia amani, utulivu na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika mkutano huu wa 10 wa Baraza la Tisa la Wawakilishi. Leo hii Baraza linapokea na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa Fedha 2018-2019.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara na jitihada zake anazozitumia katika kuiongoza nchi yetu ambapo sote ni mashuhuda wa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wake. Aidha, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa ujasiri na umakini wake wa kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais na kama Kiongozi wa Serikali hapa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, makadirio haya yanawasilishwa baada ya kazi kubwa na mashirikiano na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza lako hili. Naomba uniruhusu niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, mara hii wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Hamida Abdalla Issa kwa uweledi, umakini na uchambuzi wa kina kuiongoza Kamati hii kwa ufanisi mkubwa. Nachukua fursa hii pia kumpa pole Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa mtihani wa maradhi. Kwetu waja, mitihani ni jambo la kawaida. Tunamshukuru Allah kwa kumponesha na kumuwezesha kurudi tena hapa Barazani kuungana nasi katika kuwatumikia wananchi. Tunamuomba Mwenyezi …

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Fedha kumradhi kidogo naomba nimpishe Mwenyekiti ili nami nikaweze kusimamisha sala.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema ili Baraza liendelee kunufaika na mchango wake mkubwa wa uongozi mahiri kutokana na utaalamu na uzoefu wake mkubwa alionao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Donge ambao ndio walionichagua kupitia Chama chetu cha Mapinduzi ili kuwa Mwakilishi wao katika Baraza hili. Aidha, naomba kuwashukuru tena kwa stahamala na uvumilivu wao wanaouchukua wakati nikiwa katika harakati za kutekeleza majukumu niliyopewa na serikali yetu. Na mashirikiano yao makubwa yanayofanya nisaidiane nao vyema katika kushughulikia maendeleo yao.

MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi hakuna mabadiliko katika majukumu ya msingi ya Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, kumefanyika mabadiliko ya Muundo wa Wizara ya Fedha na Mipango, kufuatia kuanza kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali namba 11 ya 2016 na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya 2016. Kwa azma ya kuongeza ufanisi uwajibikaji na kushughulikia vyema maendeleo ya Sekta ya Fedha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mabadiliko yafuatayo kwa muundo wa Wizara.

i. Idara mpya ya Ukaguzi wa Ndani na kuondoa jukumu hilo kutoka Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Hatua hii itasaidia kuimarisha Utawala Bora kwa kuimarisha Ukaguzi wa Ndani na kuufanya wenye kujitegemea zaidi;

ii. Kuanzishwa Idara mpya ya kushughulikia Sera za Kodi na Maendeleo ya Sekta ya Fedha; na

iii. Kuanzishwa Mamlaka inayojitegemea ili kusimamia masuala ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, eneo ambalo limejitokeza kuwa na changamoto nyingi.

Mhe Mwenyekiti, hata hivyo, muundo wa Bajeti ya Wizara unaendelea kuundwa na mafungu makuu matatu likiwemo; Fungu F01-Wizara ya Fedha, F02-Mfuko Mkuu wa Serikali na F03-Tume ya Mipango. Wizara ya Fedha na Mipango ina jumla ya Idara kumi na tatu na Taasisi tisa zinazojitegemea. Kwa sasa tayari wakuu wa Idara zote hizo wameteuliwa. Jadweli namba 1 linaonesha muundo wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mabadiliko hayo ya muundo majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yameendelea kubaki kama yalivyokuwa awali ikisimamia majukumu ya msingi yafuatayo:

i. Kusimamia fedha za umma kwa kukusanya mapato ya serikali kutokana na vyanzo vya ndani na nje ya nchi pamoja na kusimamia matumizi yake;

ii. Kusimamia rasilimali za umma kwa kusimamia ununuzi, uhifadhi na uondoshaji wake.

iii. Kusimamia mwenendo wa Deni la Taifa;

iv. Kutoa huduma za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani Serikalini;

v. Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha;

vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira kuu ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye Mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuangalia masuala ya Idadi ya watu na mahitaji yake;

vii. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi;

viii. Kushajiisha na kufanikisha uwekezaji wa sekta binafsi; na

ix. Kusimamia maendeleo ya Uchumi.

Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango Kwa Kipindi cha Julai-Machi 2017/2018

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Baraza lako katika mwaka 2017-2018, iliidhinishia Wizara ya Fedha na Mipango kusimamia upatikanaji wa mapato ya TZS 1.087 trilioni kwa ajili ya Bajeti ya Serikali. Kati ya mapato hayo asilimia 97.4 sawa na TZS 1.059 trilioni ilipangiwa kuzisimamia na kuzikusanya kutoka vyanzo mbali mbali vya ndani ikiwemo:

i. TZS 347.29 bilioni zilipangwa kukusanywa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar *ZRB*;
ii. TZS 258.72 bilioni zilipangwa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato- Tanzania *TRA*Tawi la Zanzibar;
iii. TZS 21.0 bilioni kutoka SMT ikiwa ni kodi ya mapato *PAYE* kwa wafanyakazi wa Taasisi za Muungano ambao wanafanya kazi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Ruzuku na Mikopo kutoka nje, Wizara ilitarajia kupokea TZS 380.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kukopa TZS 30.0 bilioni katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya Bajeti kwa mwaka 2017-2018.

Mhe. Mwenyekiti, Kiwizara, Wizara ya Fedha na Mipango, ilikadiriwa kukusanya TZS 22.40 bilioni kutoka vyanzo tofauti visivyokuwa vya kodi vikiwemo:

i. TZS 15.0 bilioni zilizopangwa kukusanywa kupitia mapato ya Idara ya Uhamiaji;
ii. TZS 3.0 bilioni za Gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania;
iii. TZS 3.0 bilioni ikiwa ni Gawio kutoka katika Mashirika ya SMZ ; na
iv. TZS 1.4 bilioni ambazo zinajumuisha kodi za majengo na Bohari za Serikali, uuzwaji wa vifaa vichakavu na usajili wa wazabuni wanaotaka kutoa huduma kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Wizara imekusanya jumla ya TZS 683.36 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 99.6 ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa. Makusanyo hayo yanaonesha ukuaji wa asilimia 52.6 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 448.16 bilioni zilizokusanywa na Wizara kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017. Kati ya kiasi hicho mapato ya ndani ni TZS 532.34 bilioni na ya nje ni TZS 151.02 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, **k**wa mapato ya ndani utendaji kitaasisi ni kama ifuatavyo:

i. TZS 238.96 bilioni zimekusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar, sawa na asilimia 96 ya makadirio ya TZS 269.5 bilioni zilizopangwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi tisa. Mapato yaliyokusanywa na *ZRB* yanaonesha ukuaji wa asilimia 31 ikilinganishwa na TZS 197.53 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi cha Julai, 2016 - Machi, 2017;

ii. TZS 190.51 bilioni zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Tawi la Zanzibar. Ukusanyaji huu umefikia asilimia 99 ya lengo la TZS 193.2 bilioni zilizopangwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi tisa. Aidha, mapato haya yanaonesha ukuaji wa asilimia 25 ikilinganishwa na jumla ya TZS 152.66 bilioni zilizokusanywa na *TRA* kwa kipindi cha Julai, 2016 - Machi, 2017;

iii. Mapato yatokanayo na kodi ya wafanyakazi wa Taasisi za Muungano waliopo Zanzibar ni TZS 15. 75 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, mapato kutokana na ruzuku na mikopo kutoka nje, utendaji halisi kwa kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ni kama ifuatavyo:

i. Jumla ya TZS 151.02 bilioni zimepokelewa kama Ruzuku na Mikopo kwa Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya kiasi hicho, TZS 34.10 bilioni ni ruzuku na TZS 116.92 bilioni ni mikopo nafuu. Kiwango hicho ni sawa na asilimia 83 ya matarajio ya TZS 125.58 kwa kipindi cha miezi tisa;

ii. TZS 3.15 bilioni zimepokelewa ikiwa ni Misaada ya Kibajeti *GBS*; na

iii. Aidha, Wizara imefanikiwa kukusanya TZS 18.57 bilioni sawa na asilimia 83 za makadirio ya kukusanya TZS 22.4 bilioni kutoka katika vyanzo visivyokua vya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2018 Idara ya Uhamiaji imekusanya TZS 15.94 bilioni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya TZS 15.0 bilioni kwa mwaka 2017-2018. Makusanyo haya yanaonesha ukuaji wa asilimia 78 ikilinganishwa na TZS 8.99 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017. Miongoni mwa sababu zilizopelekea ukuaji wa mapato hayo ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa wageni kutoka nje ya nchi ; na
ii. Hatua ya Serikali kubadili viwango vya ugawaji wa fedha zinazokusanywa na Idara ya Uhamiaji.

Mhe. Mwenyekiti, mgao wa fedha zinazokusanywa na Idara ya Uhamiaji, Tawi la Zanzibar kwa sasa uko katika uwiano wa 25:75 ukilinganishwa na ule uwiano wa zamani wa 50:50. Mgao huu ulifikiwa baada ya kufanya tathmini na uchambuzi wa mahitaji ya matumizi na kukubaliana na Idara husika.

MATUMIZI YA WIZARA KWA PROGRAMU

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017-2018 ilikadiriwa kutumia TZS 219.41 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa programu kuu saba ambazo zinatekelezwa kupitia programu ndogo 16. Kwa kipindi cha miezi tisa, Wizara imepatiwa jumla ya TZS 160.77 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio ya mwaka. Fedha hizi zilitumika kutekeleza programu na miradi mbali mbali ya Wizara kama ifuatavyo:

Programu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na Usimamizi wa Fedha za Umma. Programu inaundwa na programu ndogo tatu zinazohusika na utekelezaji wa majukumu yafuatayo:

i. Usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutokana na vyanzo vya ndani na nje ya nchi;
ii. Matayarisho na usimamizi wa Bajeti ya Serikali;
iii. Usimamizi wa Hazina na utoaji wa huduma zote za kiuhasibu; na
iv. Ukaguzi wa ndani wa Serikali.

Mhe. Spika, programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 64.84 bilioni kwa mwaka 2017-2018. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya TZS 33.91 bilioni zilitumika kwa programu sawa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo unapatikana kuanzia kifungu cha 21 hadi 31 katika hotuba yangu.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hazina

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hazina ina jukumu la kufanikisha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na usimamizi wa fedha za umma. Kwa mwaka wa fedha wa 2017-2018 imepangiwa kutumia jumla TZS 35.97 bilioni hadi kufikia Machi imetumia jumla TZS 25.07 bilioni sawa asilimia 70. Mambo yaliyotekelezwa ni pamoja na haya yafuatayo:

i. Kuratibu ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali ya TZS 506.61 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya TZS 675.8 bilioni;
ii. Kuratibu ukusanyaji wa Fedha za Mfuko wa Miundombinu TZS 24.26 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 70 ya makadirio ya TZS 34.82 bilioni ya bajeti ya mwaka;
iii. Kusimamia matumizi ya Serikali ya TZS 676.86 billioni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya Bajeti ya TZS 1.087 trilioni;
iv. Kutoa mafunzo kwa wahasibu wa ngazi mbali mbali ikiwemo mafunzo ya juu ya uhasibu, masuala ya viwango kwa uhasibu wa umma *(CPA)* na *(IPSAS*. Aidha,Programu Ndogo imejenga uelewa wa tasnia ya Kihasibu Kimataifa kwa kuhudhuria Kongamano la Kimataifa la Wahasibu Wakuu wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika *(ESAAG)*;
v. Kusimamia matayarisho ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya 2016 ambapo tayari rasimu ya awali imeshaandaliwa;
vi. Kuimarisha Mtandao wa Matumizi ya Serikali *IFMS* kutoka *ERP* 10.0 kwenda *ERP* 10.1, pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji wapya na wazamani;
vii. Kujenga Kituo cha Kuhifadhia Kumbukumbu za Mtandao wa *IFMS* kwa kukabiliana na majanga *(Disaster Recovery Site)* kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibari *(PBZ)*;
viii. Kuimarisha ukusunyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kuunganisha vituo kumi na nne vya ukusanyaji mapato ya ndani na hivyo kuimarisha usimamizi wa mapato hayo kwa kuondokana na kupokea Fedha taslim;
ix. Kuendesha vikao vya kamati ya ukomo wa matumizi *(Expenditure Ceiling Committee).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa azma ya kuimarisha ufanisi wa utendaji katika bajeti ya mwaka 2017-2018. Wizara nne na Ofisi tatu zilianzishwa utaratibu wa kuingiziwa kwa majaribio matumizi mengineyo *(Other Charges)* ya miezi mitatu mwanzoni mwa kila robo mwaka. Wizara hizo ni Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Ofisi zilizonufaika na utaratibu huo ni Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa ikitanguliziwa matumizi hayo mengineyo wiki ya kwanza ya kila mwezi.

Programu Ndogo ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Usimamizi wa Hesabu za Ndani ina jukumu la kuratibu, kufuatilia, kusimamia ukaguzi wa hesabu za ndani ya Wizara, Idara, Taasisi, Wakala na Serikali za Mitaa. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 programu hii ndogo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 3.03 bilioni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 programu ndogo hii imeingiziwa jumla ya TZS 419.77 milioni sawa na asilimia 14 ya makadirio na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kufanya Ukaguzi wa Ndani kwa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Serikali na kutoa Ripoti kila baada ya miezi mitatu;

ii. Kukamilisha Ripoti ya ukaguzi wa Ndani ya mwaka 2016-2017 na kufanya mapitio ya Ripoti za ukaguzi wa ndani za robo mwaka 2017-2018 katika Wizara na Taasisi zake;

iii. Wakaguzi wa Ndani 116 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi wa ndani pamoja na uandishi wa ripoti za ukaguzi;

iv. Kufanya usajili wa uanachama wa Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi ya ukaguzi Tanzania kwa Wakaguzi 15 na kununua vitabu 20 vya Muongozo wa Kimataifa wa Ukaguzi;

v. Kufanya ukaguzi maalum unaohusiana na uendelezaji wa visima vya Ras Al Khaimah katika Mamlaka ya Maji Zanzibar; na

vi. Kuwapatia mafunzo kwa vitendo Wakaguzi 5 katika Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani Tanzania Bara.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii ina jukumu la kuandaa Bajeti ya Serikali kwa kugawa fedha ki-fungu, kusimamia utekelezaji wa Bajeti kwa kufuata ukomo wa matumizi kulingana na matarajio ya mapato ya kila mwezi na kutoa miongozo na ufuatiliaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, programu ndogo inasimamia malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2017-18 programu ndogo ilitengewa jumla ya TZS 23.69 bilioni. Kati ya Fedha hizo, TZS 23.0 bilioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara Serikalini na TZS 692.24 milioni ni kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 programu ndogo imetumia jumla ya TZS 7.28 bilioni sawa na asilimia 32 kwa ajili ya marekebisho ya mshahara na TZS 654.36 milioni sawa na asilimia 95 kwa utekelezaji wa shughuli za programu ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, aghlabu marekebisho makubwa ya mshahara hufanyika katika robo ya mwisho ya utekelezaji wa bajeti kutokana na ajira mpya na marekebisho mengine ya nyongeza za mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Usimasmizi wa Bajeti ya Serikali imetekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia na kuchapisha vitabu 500 vya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018;

ii. Kuratibu shughuli za kibajeti, kuandaa na kusambaza muongozo wa Bajeti uliotoa mgao wa fedha kwa Wizara na Idara zinazojitegemea;

iii. Kuandaa Mkabala wa Bajeti ya Serikali *(Budget Framework Paper)* na kuwasilishwa kwa wadau na hatimae katika Baraza la Wawakilishi kwa kufuata matakwa ya Sheria Mpya ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016;

iv. Kusimamia malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali ili yaendane na miongozo ya Utumishi wa Umma bila ya kuathiri Bajeti.

v. Kuimarisha mtandao wa bajeti ili uende sambamba na bajeti ya miaka mitatu na;

vi. Kufanya warsha na mafunzo ya kuwaelimisha wakurugenzi, maafisa mipango, wahasibu juu ya uimarishaji wa uwekaji gharama katika muundo wa miaka mitatu *(MTEF)* kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Mapato Yatokanayo na Kodi

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi ina jukumu la kuandaa, kufuatilia na kutathmini Sera za Mapato na Maendeleo ya Sekta ya Fedha kwa lengo la kuimarisha rasilimali za ndani ili ziendane na mahitaji ya uwekezaji nchini. Aidha, programu ndogo inahakikisha uunganishaji wa Sekta ya Fedha (Mabenki, Bima, Hifadhi ya Jamii) na Soko la Mitaji kwa upande mmoja na Wizara kwa upande mwengine ili kuhakikisha ustawi wa Sekta hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017-18 programu ndogo hii ilitengewa jumla ya TZS 328.18 milioni. Kati ya Fedha hizo, TZS 18.13 milioni ni kwa ajili ya mishahara na TZS 149.49 milioni ni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi mwezi Machi, 2018 programu ndogo hii imetumia jumla ya TZS 167.62 milioni ambayo ni sawa na asilimia 51 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera za Kodi na kutoa mapendekezo ya hatua ya kuimarisha mapato ya ndani;

ii. Kufanya vikao na wadau mbalimbali kwa ajili ya kujadili mfumo bora wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2018/19;

iii. Kufanya makadirio ya mapato ya Serikali na kuandaa mswada wa Fedha 2018/19;

iv. Kukamilisha kanuni ya wakala wa ukusanyaji wa ushuru wa stempu na kufanya mapitio ya kanuni ya wakala wa ushauri wa kodi na kuanza mapitio ya Kanuni ya Udhibiti Utakatishaji wa Fedha haramu;

v. Kushiriki katika vikao vya kitaifa, kikanda na kimataifa juu ya mikakati ya kodi, fedha na rasilimali zisizorejesheka;

vi. Kushiriki katika vikao vya utengamano ya Jumuiya ya

Afrika Mashariki; na

vii. Kuratibu kazi zinazoendelea za mapitio ya mfumo wa mapato nchini kwa azma ya kuweka mfumo bora kwa maendeleo ya uchumi.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje ina jukumu la kuimarisha mashirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutafuta na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar kupitia Mkakati wa Tatu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.82 bilioni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 jumla ya TZS 318.7 milioni sawa na asilimia 17.5 zimetumika kwa kukamilisha shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu upatikanaji wa Ruzuku na Mikopo ambayo jumla ya TZS 151.01 bilioni zimepatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 39.68 ya makadirio ya mwaka ya TZS 380.5 bilioni. (Ruzuku ni TZS 34.01 bilioni na Mikopo ni TZS 116.91 bilioni).
ii. Kufanya Uchambuzi wa kifedha kwa miradi mipya ambayo inatarajiwa kuwasilishwa kwa Washirika wa maendeleo.
iii. Kuratibu mikutano ya robo mwaka kwa taasisi za Serikali pamoja na zisizo za kiserikali.
iv. Kufanya ufuatiliaji wa miradi na kutayarisha ripoti ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
v. Kushiriki mikutano ya ndani pamoja na ya kimataifa ya kwa ajili ya utafutaji wa rasilimali fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na

vi. Kuratibu mawasiliano na Washirika wa Maendeleo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mashirikiano yao na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa programu ndogo hii kifedha ni mdogo kutokana na kutokamilika kwa ununuzi wa mashine za kutolea risiti *(EFD machine)* ambapo hatua za ununuzi zinaendelea.

Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kusimamia Mali za Umma na kuhakikisha kunakuwepo na tija katika uwekezaji katika Mitaji ya Umma. Programu hii inasimamia utekelezaji wa jukumu la usimamizi wa Mali za Serikali ambalo linahusisha ununuzi, utunzaji, udhibiti, uondoaji wa Mali za Serikali na usimamizi wa Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Mashirika ya Umma na Kampuni Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 9.51 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa Fedha 2017-2018. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii ilitumia TZS 5.26 bilioni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo ndani ya program hii umeelezwa katika kifungu namba 34 hadi 36 ndani ya kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Programu Ndogo ya Mitaji ya Umma

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma ni kusimamia uwekezaji katika Mitaji ya Umma ikiwemo Mashirika ya Umma na Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Kampuni Binafsi. Aidha, programu ndogo inasimamia utunzaji, udhibiti na uhakiki wa Mali za Serikali.
Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 9.33 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2017-2018. Hadi kufikia Machi, 2018 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma ilitumia TZS 5.07 bilioni sawa na asilimia 54 ya makadirio ya mwaka TZS 9.33 na kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya TZS 945.80 milioni ikiwa ni mapato yanayotokana na ukodishwaji wa Mali za Serikali na TZS 1.58 bilioni kutoka katika gawio la faida ya Mashirika ya Serikali;

ii. Kusimamia mapitio *(review)* ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya 2002 pamoja na Uandaaji wa Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali *(Public Asset Management Policy);*

iii. Kuhakiki maombi ya fidia kwa majengo yatakayoathirika wakati wa ujenzi wa barabara ya Chake Chake-Wete na kuthamini majengo 82 yaliopo katika eneo la Kizimbani;

iv. Kusimamia uandaaji wa Daftari la Kielektroniki la Mali za Serikali kwa kukusanya taarifa, kuthamini, kuziwekea alama tambuzi mali za Serikali na kuziingiza katika daftari. Kwa mwaka 2017/18 jumla ya Wizara zote za Serikali zinaendelea kufanyiwa zoezi hili.

v. Kusimamia Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali ambapo kwa mwaka huu mradi utakaotekelezwa ni ujenzi wa majengo pacha kwa Wizara tatu Pemba, ikiwemo Wizara Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hadi Machi, 2018 mradi umefikia asilimia 70;

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii ina jukumu la kusimamia ununuzi na uondoaji wa mali za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, programu ndogo hii ilitengewa jumla ya TZS 175.8 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 programu ndogo hii imetumia jumla ya TZS 185.7 milioni sawa na asilimia 105.6
Mhe. Mwenyekiti, ongezeko la programu ndogo hii imetokana na kugharamia uanzishwaji wa Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali Serikali, iliyoanzishwa mwezi wa Septemba, 2017 kwa lengo la kuimarisha udhibiti katika ununuzi na uondoaji wa mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuandaa Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali Nam. 11 ya 2016;

ii. Kuendesha mikutano minne kwa wakuu wa vitengo vya ununuzi *(PMU)* kwa Unguja na Pemba na kujadili utendaji na chagamoto katika kazi za manunuzi;

iii. Kujifunza namna ya kuimarisha shughuli za Mamlaka kupitia Mamlaka kama hizo Tanzania Bara;

iv. Kuhudhuria mkutano wa mwaka wa Bodi ya Taifa ya Manunuzi *(PSPTB)* wa kutathmini utendaji, uimarishaji na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa kazi za ununuzi Tanzania;

v. Kuanza ujenzi wa Mamlaka hiyo mpya kitaasisi kwa kuipatia ofisi, watendaji na vifaa vya kufanyia kazi; na

vi. Kushughulikia rufaa tano (5) zilizowasilishwa kuhusiana na masuala ya Zabuni za Ununuzi ambazo ni:

a. zabuni inayohusiana na ujenzi wa ofisi ya *ZURA*;

b. zabuni inayohusiana na uzamiaji na kuunganisha bomba za meli za mafuta;

c. zabuni inayohusiana na utoaji wa huduma;

d. zabuni inayohusiana na usambazaji wa mita za umeme; na

e. zabuni inayohusiana na ujenzi wa barabara ya Bububu, Mahonda, Mkokotoni 31km, Fuoni-Kombeni 8.582km, Pale-Kiongele 4.611km na

f. Matemwe-Muyuni 7.580 km.

Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha ina jukumu la utayarishaji wa Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha na kutoa huduma ya uendeshaji na kiutumishi. Progamu hii ina programu ndogo tatu. Katika mwaka wa fedha 2017-2018 programu ilipangiwa kutumia TZS 34.514 bilioni kwa kutekeleza shughuli zilizopangwa. Fedha zilizotumika kwa Kipindi cha Julai 2017-Machi 2018 ni TZS 23.25 bilioni sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka. Shughuli zilizotekelezwa ndani ya program ndogo zinaonekana kuanzia kifungu nambari 38 hadi 40 ya hotuba yangu kama ifuatavyo:

Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ina jukumu la kutoa huduma za uongozi wa rasilimali watu na utawala kwa wizara ili kuimarisha mazingira bora ya kazi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii ilitengewa TZS 7.25. billion Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya TZS 5.47 bilioni sawa na asilimia 75 zimetumika na kutekeleza yafuatayo:

i. Kuwejengea uwezo wafanyakazi 125 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

ii. Kuratibu vikao vya utendaji na kufanikisha ziara za wafanyakazi wanaohudhuria mikutano ya ndani na nje ya nchi kikazi;

iii. Kufanya matengenezo na matunzo ya majengo na vifaa vya kazi;

iv. Kutoa huduma za kiutawala ikiwemo ununuzi wa huduma na bidhaa;

v. Kuwapatia posho la likizo wafanyakazi 68 ambao waliostahiki kulipwa ; na

vi. Upatikanaji wa usalama na mazingira mazuri ya kazi.

Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha ina jukumu la kuandaa mipango, sera na tafiti za sekta ya fedha pamoja kutathmini programu na miradi iliyopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii ilipangiwa kutumia jumla TZS 26.16 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2018 TZS 16.76 bilioni sawa na asilimia 64.06 zilitumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu shughuli za Wizara katika Baraza la Wawakilishi.

ii. Kukusanya takwimu za kifedha kwa robo, nusu na mwaka mzima.

iii. Kufanya utafiti wa msamaha wa ushuru kwa bidhaa za unga wa ngano, mchele na sukari.

iv. Kuandaa na kufanya mapitio ya mpango kazi waWizara.

v. Kuandaa ripoti ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

vi. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za Wizara.

Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ina jukumu la kuratibu na kutekeleza shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Katika Bajeti ya mwaka 2017-2018 programu ndogo hii ilitengewa jumla ya TZS 1.11 bilioni ili kuweza kutekeleza majukumu yake, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 programu ndogo imetumia jumla TZS 1.01 bilioni sawa na asilimia 91 na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji wa ofisi Pemba.

ii. Kukagua shughuli za uondoaji wa mali chakavu katika Wizara na taasisi za serikali zilizopo Pemba;
iii. Kusimamia na kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini pamoja na kuimarisha kitengo chake cha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Wizara na Taasisi za Serikali;
iv. Kuratibu na kuendesha mafunzo ya kada mbali mbali kwa wafanyakazi na wadau.
v. Kuunganisha utekelezaji wa programu kuu na ndogo za Wizara Pemba.

Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 101.11 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za Mfuko. Kwa kipindi cha miezi tisa programu hii ilipatiwa jumla ya TZS 93.88 bilioni sawa na asilimia 92.8 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kulipa riba na mikopo ya TZS 10.13 bilioni;

ii. Kulipa mafao ya kiinua mgongo cha TZS 17.77 bilioni kwa wastaafu 1,104 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. Kulipa pencheni ya kila mwezi kwa wastani wa wastaafu 12,250 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo jumla ya TZS 16.56 bilioni zimetumika kwa kipindi cha miezi tisa;

iv. Kulipa madeni ya Wazabuni yenye thamani ya TZS 7.9 bilioni; na

v. Kulipia gharama za matumizi mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jumla ya TZS 41.52 billioni zimetumika kwa kipindi cha miezi tisa.

Usimamizi wa Deni la Taifa

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 Deni la Taifa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limefikia jumla ya TZS 519.7 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 37.8 ikilinganishwa na Deni la Taifa lililoripotiwa mwishoni wa mwezi Machi, 2017 la TZS 377.1 bilioni. Deni hilo la TZS 519.7 billioni linajumuisha TZS 158.3 bilioni ikiwa ni deni la ndani na TZS 361.40 bilioni ni Deni la Nje.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa sababu zilizopelekea ukuaji wa Deni la Taifa ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa kiwango cha ulipaji wa kiinua mgongo kwa wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

ii. Mabadiliko ya kiwango cha sarafu ya Tanzania dhidi ya Fedha za Kigeni;

iii. Kuongezeka kwa Mkopo wa Dola za Kimarekani *USD* 35.2 milioni TZS 78.9 bilioni zilizolipwa kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo jipya la abiria kwa Uwanja wa Ndege wa Unguja *Terminal III*; pamoja na

iv. Kuongezeka kwa mkopo mpya wa TZS 20.0 bilioni uliochukuliwa katika kipindi cha mapitio kuondoa nakisi ya bajeti.

Usimamizi wa Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017-2018, Mfuko wa Miundombinu ulikadiriwa kukusanya TZS 34.9 bilioni kutokana na vyanzo vya ndani. Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Mfuko wa Miundombinu umekusanya TZS 24.3 bilioni sawa na asilimia 70 ya makadirio ya mwaka. Fedha hizi zinajumuisha TZS 6.85 bilioni sawa na asilimia 51 ya makadirio ya TZS 13.55 bilioni kutokana na vyanzo vya Mfuko wa Miundombinu vinavyosimamiwa na *TRA* - Zanzibar na TZS 17.41 bilioni sawa na asilimia 82 ya TZS 27.30 bilioni kutoka katika vyanzo vinavyosimamiwa na *ZRB.*

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 matumizi ya Mfuko wa Miundombinu yamefikia jumla ya TZS 20.9 bilioni sawa na asilimia 60 ya makadirio ya kutumia TZS 34.9 bilioni kwa mwaka. Fedha hizo zimetumika katika miradi ifuatayo:

i. Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais umeombewa na kupatiwa TZS 12.50 milioni kwa ajili ya matayarisho, sawa na asilimia 3 ya lengo la TZS 500 milioni kwa mwaka;

ii. Uimarishaji wa Taasisi ya Viwango umeombewa na kupatiwa TZS 517.80 milioni sawa na asilimia 26 ya makadirio ya TZS 2.0 bilioni;

iii. Usambazaji wa umeme vijijini umeombewa na kupatiwa TZS 625.76 milioni sawa na asilimia 40 ya lengo la TZS 1.58 bilioni;

iv. Ujenzi wa barabara ya Mzambarau takao hadi Madenjani Pemba umeombewa na kupatiwa TZS 1.78 bilioni sawa na asilimia 88 ya lengo la TZS 2.0 bilioni;

v. Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete Pemba umeombewa na kupatiwa TZS 41.26 milioni sawa na asilimia 3 ya lengo la TZS 1.50 billioni;

vi. Mradi wa Uimarishaji Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali umeombewa na kupatiwa TZS 120.0 milioni sawa na asilimia 8 ya lengo la TZS 1.60 billioni;

vii. Uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi umeombewa na kupatiwa TZS 15.18 bilioni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya TZS 20.0 bilioni; na

viii. Ununuzi wa boti za uokozi umeombewa na kupatiwa TZS 2.13 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya mwaka ya TZS 2.10 billioni.

Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi ina lengo la kuimarisha uratibu wa mipango ya maendeleo na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya kitaifa. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu. Programu imepangiwa TZS 1.52 bilioni, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 programu hii imetumia jumla ya TZS 1.19 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji kwa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umaskini

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umaskini ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 927.2 milioni kwa mwaka 2017/2018. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii ilitumia jumla ya TZS 669.59 milioni sawa na asilimia 72 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

i. Kusimamia utekelezaji wa *MKUZA III* kwa kufanya mikutano katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba na kwa Watendaji Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Kuratibu utekelezaji wa mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/18

iii. Kukamilisha Rasimu ya Muelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018-2019 na Muongozo wa Utayarishaji wa Mipango Mikakati ya Sekta;

iv. Kufanya maadhimisho ya wiki ya Umaskini kwa kufanya ukarabati wa madarasa manane ya Skuli ya Langoni;

v. Kuhakiki miradi 11 ya maendeleo na kuiingiza katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018-2019; na

vi. Kuanza majadiliano ya awali juu ya matayarisho ya Mpango mpya wa maendeleo wa muda mrefu (Dira) kuchukua nafasi ya Dira ya 2020 inayokaribia kumaliza muda wake.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 419 milioni kwa mwaka 2017 – 2018. Hadi kufikia

Machi, 2018 programu ndogo hii ilitumia jumla ya TZS 296.92 milioni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

i. Kuchapisha madaftari kwa ajili ya kusajili taarifa za watu katika Shehia, kutoa mafunzo ya ujazaji wa madaftari hayo na kuziingiza taarifa katika mfumo wa kielektroniki;

ii. Kukamilisha na kuwasilisha Rasimu ya Mapitio ya Sera ya Idadi ya Watu Zanzibar 2018 na Mkakati wake, hatua zinazofuata ni kuwasilisha katika ngazi za maamuzi Serikalini;

iii. Kukamilisha uandaaji wa ripoti ya hali halisi *(situation analysis)* ya Sera ya Maendeleo ya Watendakazi Zanzibar;

iv. Kuchapisha Ripoti za Masuala ya Rasilimali Watu Zanzibar ; na

v. Kutoa mafunzo ya kuibua fursa na vikwazo vya maendeleo kwa Makatibu wa Masheha wa Wilaya tano za Unguja na Pemba na;

Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 170 milioni kwa mwaka 2017– 2018. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii ilitumia jumla ya TZS 219.49 milioni sawa na asilimia 129 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

i. Kufanya ufuatiliaji wa miradi na programu za maendeleo ambapo ziara tatu zimefanyika Unguja na Pemba. Jumla ya programu na miradi 43 kati ya miradi 70 iliyoingiziwa fedha ikiwa sawa na asilimia 61.4 ya miradi ilitembelewa.

ii. Kutayarisha na kuwasilisha ripoti za ufuatiliaji na tathmini za programu na miradi ya maendeleo kwa wadau mbali mbali ikiwemo ripoti za ziara na ripoti za utekelezaji. Jumla ya ripoti 15 zimetayarishwa na kuwasilishwa.

Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu

Mhe. Mwenyekiti, lengo la programu hii ni kuandaa sera madhubuti za kiuchumi na sera za kodi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetengewa kutumia TZS 6.2 bilioni. Kwa kipindi cha mapitio, jumla ya TZS 2.47 bilioni sawa na asilimia 40 zimetumika. Utekelezaji kwa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi na Takwimu

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 6.1 bilioni kwa mwaka 2017 – 2018. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii ilitumia jumla ya TZS 2.44 bilioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa programu ndogo ni kama ifuatavyo:

i. Kufanya mapitio ya moduli ya kifedha *(Financial Programming)* pamoja na kuanza kutumia moduli ya utabiri wa faharisi za bei za bidhaa na huduma ambazo husaidia kufanya makadirio ya mwenendo wa uchumi na mfumko wa bei;

ii. Kuratibu utafiti wa usarifu wa zao la mwani na utafiti wa ongezeko la vyombo vya moto na hali ya miundombinu ya barabara iliyopo;

iii. Kufanya uchambuzi wa miradi ya uwekezaji na kutambua fursa za kiuchumi na kijamii;

iv. Kukamilisha uchambuzi na utoaji wa ripoti za kitakwimu ikiwemo, Pato la Taifa, faharisi ya bei ya mlaji, utalii na uzalishaji viwandani;

v. Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na uwekaji wa thamani; na

vi. Kukamilisha ununuzi wa vifaa vya *TEHAMA* kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa ndani na nje *(LAN and WAN)*.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Mhe. Mwenyekiti, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 80 milioni kwa mwaka 2017/2018. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii ilitumia jumla ya TZS 32.6 milioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufanya upembuzi yakinifu wa awali wa Mradi wa Ujenzi wa Bohari ya Mafuta *(Oil Terminal)* katika eneo la Bumbwini/Mangapwani;

ii. Kutembelea na kuibua miradi 13 ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi *(Public Private Partnership)* awamu ya mwanzo *(bundle I)* kwa kushirikiana na Halmashauri za Mikoa na Mabaraza ya Miji ya Unguja na Pemba. Miradi hiyo kwa sasa iko katika hatua za kufanyiwa upembuzi yakinifu wa awali.

iii. Kukaa na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuibua miradi mipya ya awamu ya pili *(bundle II)* ya *PPP*;

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Programu hii ina programu ndogo moja na ilitengewa jumla ya TZS 1.7 bilioni. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2018 programu hii imetumia jumla ya TZS 821 milioni sawa na asilimia 48 ya makadirio na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 6 na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 22 ili kuongeza ujuzi wa kiutendaji katika fani mbali mbali zinazohusiana na kazi zao.

ii. Kuratibu vikao 16 vya Tume ya Mipango vikiwemo, Kamati ya Wataalamu, Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani.

iii. Kuweka mfumo wa elektroniki wa kurikodi mahudhurio ya wafanyakazi na,

iv. Kutoa huduma za kiutawala na kiuendeshaji.

UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2017 -MACHI 2018

Mradi wa Usimamizi wa Mageuzi ya Fedha za Umma *(PFMRP)*

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Mageuzi ya Fedha za Umma *(PFMRP V)* ni mradi unaotekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wa Zanzibar Mradi huu upo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mwaka wa fedha wa 2017-2018 mradi uliidhinishiwa matumizi ya TZS 2.6 bilioni kwa ajili ya utekelezaji kazi za Mradi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha tathmini Mradi umepokea jumla ya TZS 287.12 milioni na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuwapatia mafunzo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Bajeti.

ii. Kuwapatia mfunzo ya Ukaguzi wa Utakatishaji wa

Fedha haramu, wafanyakazi 30 wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

iii. Kulipa gharama za ushauri kwa matayarisho ya Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali;

iv. Kutoa mafunzo ya Bajeti inayozingatia Programu *(PBB)* kwa wafanyakazi 147 wa Serikali za Mitaa Unguja na Pemba;

v. Kununua mtambo wa kuchapa *(Bar code)* kwa mali Wizara za Serikali; na

vi. Kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma *(Public Investment Act)* namba 11 ya 2002 kwa nia ya kutunga mpya.

Mradi wa Uimarishaji Utawala Bora Awamu ya Tatu *(ISPGG III)*

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la mradi ni kukuza uchumi kwa kuimarisha utawala bora wa kiuchumi na kifedha kupitia ufanisi wa usimamizi wa fedha za umma na mazingira bora ya biashara. Kwa mwaka wa Fedha 2017-2018, Mradi wa *ISPGG III* ulipanga kutumia jumla ya TZS 3.8 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2018 mradi umetumia jumla TZS 1.7 bilioni sawa na asilimia 45 ya makadirio. Shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya ufuatiliaji na tathmini kwa wafanyakazi 16 wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali *(ZPPDA),*

ii. Kutoa Mafunzo kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya ukaguzi wa misingi hatarishi *(Risk Based Audit),*

iii. Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wafanyakazi wa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

iv. Kutoa mafunzo juu ya Sera na Mikakati ya sera kwa Wafanyabiashara Binafsi Unguja na Pemba;

v. Kuwawezesha wafanyakazi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi *(ZAECA)* kufanya ziara za kimasomo;

vi. Kutoa mafunzo juu ya mpango wa usimamizi wa mfuko wa pensheni;

vii. Kutoa mafunzo juu ya makubaliano na mazungumzo ya ufuatiliaji wa rasilimali fedha; na

viii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya ufuatiliaji na tathmini kwa watendaji wa Idara ya Fedha za Nje.

Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Mradi ni kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Kwa mwaka wa Fedha 2017-2018 Mradi ulipangiwa kutumia jumla TZS 700.00 milioni. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2018 mradi umetumia TZS 54.70 milioni sawa na asilimia 7.8. Kuchelewa kupatikana kwa fedha kutoka kwa wahisani kumepelekea utekelezaji mdogo kwa mradi huu katika kipindi cha tathmini. Aidha, mradi umetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar juu ya Sheria na Kanuni zinazohusiana na huduma za maji na nishati;

ii. Kutoa mafunzo ya kodi yaliyojumuisha wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Tawi la Zanzibar na wadau wake na;

iii. Kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji wa kodi katika bodi ya Mapato Zanzibar kwa kulipa gharama za washauri
14 watakaofanya kazi za uimarishaji wa mfumo huo.

Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017-2018, Programu ya ujenzi wa Ofisi za Serikali ulihusisha ujenzi wa Ofisi tatu za Serikali kwa upande wa Pemba ambazo ni Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto na Ofisi ya Rais, Katiba,

Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ukarabati wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi na Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Unguja.
Kwa mwaka 2017-2018, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 5.57 bilioni. Hadi mwezi wa Machi 2018 jumla ya TZS 4.02 bilioni zimetumika sawa na asilimia 72.1 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa Ofisi tatu Pemba hadi kufikia mwezi Machi 2018 hali ya ujenzi ilikuwa kama ifuatavyo:

i. Kukamilika kwa ujenzi wote wa majengo *(super structure);*

ii. Kukamilika kwa upigaji plasta nje na ndani;

iii. Kuwekwa miundombinu ya njia za umeme na maji; na

iv. Kuwekwa njia za TEHAMA, simu na mifumo ya ulinzi *(Security System).*

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha utekelezaji wa programu hii,Wizara imelipa gharama zifuatazo:

i. Jumla ya TZS 3.2 bilioni zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa wizara tatu Pemba.

ii. Jumla ya TZS 200 milioni zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya pili katika jengo la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Unguja;

iii. Jumla ya TZS 275.8 milioni zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Tume ya Uchaguzi na Tume ya Kurekebisha Sheria;

iv. Jumla ya TZS 222 milioni zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vya kufundishia madaktari kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar; na

v. Jumla ya TZS 123 milioni zimetumika kwa ajili ya kumalizia malipo ya awamu ya mwisho ya ujenzi wa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria.

Programu ya Uimarishaji wa Huduma za Jamii Mijini *(ZUSP)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 Mradi wa Huduma za Jamii Mijini *(ZUSP)* umetekeleza kazi mbali mbali katika maeneo ya mabaraza ya miji ya Wete, Chake Chake, Mkoani na Manispaa ya Mjini Unguja. Katika kipindi hicho, program imetekeleza miradi ifuatayo:

Ujenzi wa Ukuta wa Bahari wa Mizingani

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa ukuta wa bahari wa Mizingani umekamilika pamoja na kutengeneza barabara, njia za kupita kwa wanaokwenda kwa miguu pamoja na bustani zake na kuzinduliwa katika shamrashamra za kutimiza miaka 54 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwezi wa Januari 2018. Mradi unaendelea na awamu ya pili kwa ujenzi wa eneo la Mizingani na barabara ya waendao kwa miguu hadi mlango wa kuingia abiria bandarini Malindi. Jumla ya TZS 8.00 billioni zilitumika kutoka Julai 2017 hadi Machi 2018.

Ujenzi wa Misingi ya Maji ya Mvua

Mhe. Mwenyekiti, mradi umeshakamilisha ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka eneo la Darajabovu hadi daraja la Saateni *(System I)* wenye urefu wa mita 2,400 na ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka Shehia ya kwa Binti Amrani hadi Kilimani *(System E)* wenye urefu wa mita 1,700. Aidha, ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka Kwamzushi hadi Mtopepo *(System G)* wenye urefu wa mita 1,400 nao pia umekamilika. Kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 jumla ya TZS 2.4 billioni zimetumika.

Ulipaji fidia

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia mradi wa ZUSP kwa mwaka 2017-2018 imelipa fidia kwa wananchi 138 ili kupisha ujenzi wa misingi ya maji ya mvua katika eneo la Jang'ombe, Mpendae, Nyerere, Chumbuni, Saateni na Kwamtipura. Katika zoezi hilo jumla ya TZS 4.32 billioni zilitumika.

Jaa la Kibele

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu, usanifu wa michoro ya jaa na barabara za kuingilia Kibele na Maruhubi. Taratibu za ununuzi za kumpata mkandarasi wa kujenga jaa la kisasa zinaendelea na zabuni zimepokelewa kwa ajili ya uchambuzi. Serikali imelipa Jumla ya TZS 440 milioni kwa kazi ya upembuzi yakinifu ikiwa ni mchango wake katika mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Baraza la Mji wa Chake Chake, na kufanya ukarabati wa Ofisi za Mabaraza ya Miji ya Wete na Mkoani pamoja na ununuzi wa samani. Jumla TZS 4.98 bilioni zimetumika.

Mradi wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kuwawezesha wananchi kuweza kutumia rasilimali za biashara na ardhi katika kujikwamua na umasikini. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 400 milioni. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya TZS 376 milioni zimepatikana sawa na asilimia 94 na kutekeleza yafuatayo:

i. Kuvitambua viwanja 1,000 katika eneo la Mpendae kwa Binti Amrani. Hatua inayofuata ni kuwasilisha utambuzi wa viwanja hivyo kwa Mrajisi wa Ardhi kwa lengo la kutoa Hati za Usajili wa viwanja hivyo;

ii. Kutoa mafunzo juu ya uendeshaji na usimamizi wa biashara kwa wafanyabiashara 100 kwa Wilaya ya Kaskazini A na Micheweni,

iii. Kujenga uelewa kwa Wilaya tatu za Unguja na mbili za Pemba kuhusu MKURABITA;

iv. Kushiriki katika mafunzo ya kubadilishana uzoefu kwa Maafisa watano Tanzania Bara katika urasimishaji wa Ardhi; na

v. Kukamilisha hatua za awali za ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za urasimishaji Unguja na Pemba.

Mradi wa Kupunguza Umaskini

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umelenga kuratibu shughuli za kupambana na umasikini katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 mradi huu ulitengewa TZS 105 milioni. Hadi kufikia Machi 2018 Jumla ya TZS 54 milioni zimepatikana sawa na asilimia 51 kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

i. Kutoa mafunzo kwa Maofisa 35 juu ya uchambuzi wa kitaalamu wa masuala ya umaskini;

ii. Kuanza kwa hatua za awali za ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya kufanya uchambuzi zaidi kuhusiana na umaskini katika Wilaya ya Mkoani. Uchambuzi huo unazilenga Shehia zilizojitokeza kuwa na umaskini zaidi kwa mujibu wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Zanzibar *(HBS)* ya mwaka 2014/15.

iii. Kukamilika kwa hatua ya awali ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mfumo wa uwekaji na usimamizi wa taarifa za vijiji masikini.

Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsi na Umaskini

Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala yanayohusiana na idadi ya watu, afya ya uzazi, jinsia na umasikini katika mipango ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 Mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 269 milioni. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya TZS 158.0 milioni sawa na asilimia 58.7 ya makadirio ya mwaka zilitumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa mafunzo ya ujazaji wa Daftari la Shehia kwa Masheha na Wasaidizi wao Unguja na Pemba, kuchapisha madaftari hayo na kufanya ufuatiliaji wa ujazaji sahihi wa madaftari;

ii. Kuingiza taarifa za daftari la Shehia katika mfumo wa kielektroniki; na

iii. Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Idadi ya Watu Zanzibar 2018 na Mkakati wa Utekelezaji wake.

Mradi wa Kuendeleza Tafiti na Ubunifu

Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kuinua matumizi ya matokeo ya tafiti kwa maendeleo ya Zanzibar ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 225 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mwaka 2017-2018. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya TZS 70 milioni sawa na asilimia 31 ya makadirio ya mwaka zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilika kwa hatua za kukusanya taarifa za utafiti wa kuongeza thamani ya zao la mwani kutoka kwa mkulima hadi kwa mtumiaji wa mwisho kwa bidhaa zitokanazo na zao hilo. Utafiti huo umejumuisha usarifu wa bidhaa mbali mbali za zao la mwani;

ii. Kukamilika kwa ukusanyaji wa takwimu za utafiti wa athari za ongezeko la idadi ya watu na miundombinu ya barabara.

Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2017-2018 mradi ulipangiwa kupatiwa TZS 5.85 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2018 mradi ulipatiwa jumla ya TZS 2.79 bilioni sawa na asilimia 47 ya makadirio. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali pamoja na uwekaji wa samani ambapo jengo hilo limeanza kutumika;

ii. Kuanza kwa maandalizi ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya 2018/19;

iii. Kukamilisha ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa ndani na nje *(LAN and WAN);* na

iv. Kufanya mapitio na kuimarisha takwimu za Pato la Taifa kwa kuweka mwaka mpya wa kizio 2015. *(Rebasing of National Account).*

v.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017-2018 KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO.

Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)*

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kuu la *ZRB* ni kukusanya mapato yote ya Serikali na kutoa huduma bora kwa walipa kodi. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018, Bodi ya Mapato ilikadiriwa kupokea ruzuku ya TZS 18.6 bilioni kwa kutekeleza shughuli za bodi ikiwemo ukusanyaji wa Mapato ya Serikali ya TZS 347.29 bilioni. Kwa kipindi cha mapitio 2018, ZRB imepokea Ruzuku ya TZS 12.27 bilioni sawa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka 2017/18. Aidha, *ZRB* imekusanya mapato ya kodi ya TZS 259.23 bilioni, ambayo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya TZS 347.29 bilioni ya mwaka 2017/18 sawa na asilimia 97.95 ya makadirio ya TZS 306.23 bilioni ya kipindi cha Julai, 2017 - Machi, 2018.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jukumu la msingi la ukusanyaji wa mapato, *ZRB* pia ilitekekeleza shughuli mbalimbali zenye mnasaba na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai, 2017 - Machi, 2018 ni pamoja na:

i. Kulipa mishahara ya TZS 3.15 bilioni kwa wafanyakazi wa *ZRB;*

ii. Kutoa mafunzo kwa watendaji na walipa kodi kuhusu Sheria mpya ya Ushuru wa Bidhaa na Sheria Mpya ya Ushuru wa Stempu, zote za mwaka 2017 pamoja na kuanza kwa matumizi yake;

iii. Kurekebisha moduli za mtandao wa *ZITAS* ziliopo kwa kuziongezea uwezo na kuondosha kasoro zinazojitokeza. Aidha, moduli za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Mawizara ya usajili wa vyombo vya moto *(CMVRS)* na usimamizi wa

Ritani na Malipo *(Return and Payment Processing)* zimekamilika na zimeanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli nyengine zilizotekelezwa na *ZRB* ni pamoja na :

i. Ugomboaji wa deni la TZS 5.44 bilioni sawa na asilimia 43.9 ya makadirio ya deni la TZS 12.30 bilioni;

ii. Kufanya utafiti wa kubaini ukubwa wa magendo ya mafuta hapa nchini na mapato yanayokosekana kutokana na magendo hayo;

iii. Kupitia vigezo vya usajili wa walipakodi katika Idara ya Walipakodi Wakubwa pamoja na kufanya marekebisho, ambapo jumla ya walipakodi 14 wameingizwa katika orodha ya Walipakodi Wakubwa;

iv. Kukutana na Wakuu wa Wilaya za Unguja kuzungumzia usimamizi wa mapato ya Serikali; na

v. Kusajili walipakodi wapya 1,678 sawa na asilimia 90.70 ya makadirio ya kusajili walipa kodi 1,850.

Mfuko wa Barabara *(ZRF)*

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Barabara Nam. 02 ya 2001, majukumu ya msingi ya Mfuko huo ni haya yafuatayo:

i. Kutunza fedha kwa ajili ya matunzo na matengenezo ya barabara;

ii. Kuhakikisha kuwa mapato ya Mfuko wa Barabara yanakusanywa na kuwasilishwa kwenye hesabu ya Mfuko; na

iii. Kusimamia matumizi ya Mfuko wa Barabara ili kuhakikisha kuwa yanatumika kwa ufanisi na madhumuni yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017-2018 Mfuko ulikadiriwa kupokea jumla ya TZS 12.13 bilioni ambapo TZS 10.55 bilioni zingetokana na Kodi katika uingizaji wa mafuta (*Road Development Levy)*, TZS 1.50 bilioni zingetokana na kodi ya uingizwaji wa magari *(Motor Vehicle Levy)* na TZS 75.00 milioni kutokana na ukodishwaji wa eneo katika Jengo la Mfuko wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai 2017-2018 Mfuko umekusanya jumla ya TZS 9.6 bilioni, sawa na asilimia 80 ya makadirio ya mwaka 2017-2018. Makusanyo hayo yanajumuisha TZS 8.4 bilioni kutokana na kodi ya mafuta, TZS 1.10 bilioni kwa Uingizaji wa vyombo vya moto; na TZS 73.4 milioni ikiwa ni kodi ya jengo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, Mfuko wa Barabara ulikadiriwa kutumia jumla ya TZS 12.06 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali zilizopangwa na Mfuko kwa mwaka 2017-2018. Fedha hizi zinajumuisha; TZS 9.10 bilioni zilizopangwa kutumika kwa ajili

ya kazi za matengenezo ya barabara kuu; TZS 1.60 bilioni kwa matengenezo ya barabara za ndani; na TZS 1.36 bilioni kwa kazi za uendeshaji Mfuko.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa kazi za uendeshaji Mfuko kwa kipindi hicho ulikuwa ni asilimia 79. Kwa upande wa Wakala (Watendakazi) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Usafirishaji na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ utekelezaji wake ni asilimia 26 ya makadirio. Hali hii ya matumizi madogo kuliko makadirio inachangiwa zaidi na kuchelewa utekelezaji wa miradi mikubwa ya matengenezo ya barabara, kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuchelewa kukamilika taratibu za Zabuni;

ii. Uhaba wa Wakandarasi unaopelekea kutowezekana kuendesha, kandarasi kubwa zaidi ya mbili kwa wakati mmoja; na

iii. Kuchelewa kukamilisha kandarasi ziliopo, kunatokana na uchakavu wa vitendea kazi viliopo.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017-2018 **m**fuko ulikadiria kukusanya mapato ya TZS 94.14 bilioni, kutokana na michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji. Hadi kufikia Machi, 2018 mfuko umekusanya TZS 67.02 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Fedha hizi zinajumuisha michango ya wanacha ya TZS 46.14 bilioni sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka na mapato yaliyokusanywa kutoka chanzo cha uwekezaji ni TZS 20.88 bilioni sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi mfuko ulipanga kutumia jumla ya TZS 94.14 bilioni ikiwemo TZS 5.63 bilioni kwa gharama za uendeshaji wa Mfuko na TZS 34.61 bilioni kwa ajili ya kulipia mafao na TZS 52.86 bilioni kwa ajili uwekezaji. Hadi kufikia Machi, 2018 mfuko umeshatumia jumla ya TZ 4.08 bilioni kwa gharama za uendeshaji ikiwa ni asilimia 71 ya makisio ya mwaka, TZS 20.16 bilioni kulipa mafao kwa wanachama ikiwa ni asilimia 57 ya makisio ya mwaka na TZS 42.77 bilioni kwa uwekezaji ikiwa ni asilimia 80 ya makisio ya mwaka.

Shirika la Bima *(ZIC)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha miezi tisa Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Shirika limendelea kutoa huduma zake kwa wateja pamoja na kutekeleza mikakati kwa ajili ya kuongeza mapato ya Shirika kutoka katika vianzio mbali mbali. Kwa mujibu wa Mpango Kazi 2017-2018 malengo Makuu ya Shirika ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza mapato kwa asilimia 25 kila mwaka;

ii. Kuongeza mapato ya uwekezaji kwa asilimia 10 kila mwaka;

iii. Kuanzisha mfumo wa udhibiti wa majanga ;

iv. Kuimarisha utoaji wa hudma zenye viwango kwa wateja; na

v. Kuimarisha mazingira bora ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha miezi tisa July 2017 hadi Machi 2018 Shirika la Bima limekusanya jumla ya TZS 26.16 bilioni sawa na asilimia 138 ya makadirio ya kukusanya TZS 19.02 bilioni. Aidha, kwa upande wa matumizi, Shirika limetumia TZS 13.14 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya TZS 15 bilioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Matumizi ya kawaida ni TZS 4.42 bilioni;

ii. Ulipaji wa madai halali yaliyowasilishwa na yaliyohakikiwa ya TZS 6.53 bilioni; na

iii. TZS 2.19 bilioni kwa ulipaji wa ujira kwa mawakala na madalali wa Shirika.

Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)*

Mhe. Mwenyekiti, Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* ni Taasisi ya Serikali inayofanya biashara ya kibenki nchini kwa Sheria ya Mabenki ya mwaka 2006 *(BAFIA, 2006).* Hii ni benki pekee nchini Tanzania ambayo makao makuu yake yapo Zanzibar, na yenye umiliki wa asilimia 100 wa Serikali. *PBZ* ina jumla ya matawi kumi na nne (14) na vituo vitano (5) vya kutolea huduma kwa wateja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2017, *PBZ* imekusanya TZS 68.0 bilioni sawa na asilimia 104 ya makadirio ya TZS 65.3 bilioni. Sababu iliyopelekea kuvuka malengo ya mwaka ni ongezeko la asilimia 18 la uwekezaji wa mikopo binafsi kwa wateja *(personal loans),* ambapo hadi kufikia mwisho wa mwaka 2017, mikopo hiyo ilifikia TZS 239.1 bilioni ikilinganishwa na matarajio ya uwekezaji wa TZS 203.1 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, benki imetumia jumla ya TZS 52.50 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka 2017 ya TZS 61.50 bilioni. Matumizi haya yamejumuisha:

i. TZS 46.6 bilioni kwa kazi za kawaida ; na

ii. TZS 5.9 bilioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenendo wa *PBZ* bado ni mzuri na wa kutia matumaini. Kwa mwaka 2017 Benki imefanikiwa kupata faida (kabla kodi) ya TZS 21.4 bilioni sawa na asilimia 117 ya lengo la faida TZS 18.3 bilioni. Mafanikio haya yamesababishwa na mapato yatokanayo na biashara za fedha za kigeni pamoja mikopo binafsi kwa wateja. Mali za Benki ya Watu wa Zanzibar *(Total assets)* zimefikia TZS 602.7 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 97 ya matarajio ya kufikia TZS 623.8 bilioni kwa mwaka 2017. Aidha, Amana za wateja zimefikia TZS 512.3 bilioni ikijumuisha amana zilizokusanywa mwaka 2017 za TZS 502.9 bilioni. Amana za wateja wa Tawi la Benki ya kiislam zinatoa mchango wa asilimia 21 katika jumla ya amana zote za benki baada ya kufikia TZS 106.6 bilioni sawa na asilimia 73 ya matarajio ya kukusanya TZS 145.9 bilioni. Mtaji wa benki umefikia 73.7 bilioni dhidi ya makadirio ya kufikia TZS 71.6 bilioni kwa mwaka.

Mamlaka ya Uwekezaji na Uendelezaji Vitega Uchumi *(ZIPA)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017-2018, Mamlaka ilikadiria kukusanya kiasi TZS 2.40 bilioni kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Mamlaka imeweza kukusanya jumla ya TZS1.51 bilioni sawa na asilimia 80.15 ya makadirio ya mwaka wa makusanyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ilikadiria kutumia jumla ya TZS. 3.61 bilioni kwa kazi za kawaida na za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 Mamlaka imetumia TZS 1.65 bilioni kwa kazi za kawaida ambayo ni sawa na asilimia 57.08 ya makadirio ya mwaka, vile vile Mamlaka imetumia TZS 64.19 milioni kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 14.93 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi hicho cha miezi tisa kazi zilizotekelezwa ni:

i. Kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi Fumba;

ii. Kuendelea kusimamia na kuelekeza utekelezaji wa miradi mitano mikubwa *(strategic investments)* ya *Penny Royal,* Fumba *up town living, Mtoni Marine, Verde Hotel, CPS Life na Fumba Satelite City* ambayo kutekelezwa kwake kutaleta manufaa makubwa ya kijamii na kiuchumi nchini; na

iii. Kuimarisha kituo cha kuharakisha huduma za uwekezaji *One Stop Center* ambapo Mamlaka imeweza kupitia tena sheria hiyo na kuiwasilisha Serikalini ambako imeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni taasisi iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria nam.9 ya mwaka 2007. Kwa kipindi cha Julai 2017-Machi 2018, Ofisi imepatiwa jumla ya TZS 1.53 bilioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya TZS 2.22 bilioni. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kukusanya takwimu za hali ya uchumi, bei za bidhaa na huduma, biashara, elimu na afya;

ii. Kuandaa Ripoti za kila mwezi za takwimu za faharisi ya bei ya mlaji pamoja na Mfumko wa bei;

iii. Kuandaa Ripoti ya kila mwezi ya takwimu za utalii;

iv. Kuandaa Ripoti za robo mwaka za Takwimu za pato la Taifa kwa mwaka 2017;

v. Kuandaa ripoti yay a Muhtasari wa takwimu Zanzibar *(Zanzibar Statistical Abstract)* ya mwaka 2017; na

vi. Kutoa matokeo ya utafiti wa hali ya kiuchumi na kijamii kwa mwaka 2017.

MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2018-2019.

Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018-2019

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2018-2019, Wizara imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020 inayoendana na maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoyatoa katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi hili la Tisa la Wawakilishi;

ii. Kumaliza ujenzi wa Jengo la Ofisi za Wizara tatu-Pemba pamoja na uwekaji wa samani;

iii. Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango katika eneo la Mazizini-Unguja ambapo michoro imeshawasilishwa katika Kamati Tendaji ya Wizara kwa mara ya kwanza;

iv. Kusimamia uanzishwaji wa Kampuni ya Taifa ya Mafuta *(Zanzibar Petroleum Development Company);*

v. Kuendelea na mapitio ya Dira ya Maendeleo ya 2020 pamoja na kuandaa DIRA mpya ya Maendeleo ya Taifa;

vi. Kufanya sensa ya Kilimo-Zanzibar;

vii. Kusimamia mradi wa Uendelezaji wa Bandari ya Mangapwani; na

viii. Kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya kwa 2018-2019.

Mapato yatakayokusanywa na Wizara kwa mwaka 2018-2019

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018-2019. Wizara imepangiwa kukusanya TZS 1.28 trilioni ikijumuisha mapato yatakayokusanywa na Taasisi zifuatazo:

i. Mapato yatakayokusanywa na Bodi ya Mapato- Zanzibar ni TZS 405.36 bilioni;

ii. Mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato-Tanzania Tawi la Zanzibar ni TZS 301.10 bilioni;

iii. Mapato yatokanayo na kodi ya mishahara ya wafanyakazi wa Taasisi za Mungano wanaofanya kazi-Zanzibar ni TZS 21.00 bilioni;

iv. Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 467.00 bilioni; na
v. Mikopo itakayochukuliwa katika soko la fedha la ndani ni TZS 40.0 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mapato yasiyokuwa ya kodi, Wizara imepangiwa kukusanya TZS 42.03 bilioni ambao uchambuzi kutokana na vyanzo vyake unaonekana katika jadweli nam.4.

MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2018-2019

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka ujao wa fedha Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kufanya matumizi kupitia Mafungu matatu ya Bajeti. Kiujumla kwa mwaka 2018-2019, Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 295.61 bilioni ikiwemo; TZS 154.76 bilioni za matumizi ya F01-Wizara ya Fedha na Mipango; TZS 134.03 bilioni za matumizi ya F02-Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali; na TZS 6.82 bilioni kwa matumizi ya F03-Tume ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018-2019 imepangwa kutekelezwa kupitia programu saba zifuatazo:

i. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma inakadiriwa kutumia TZS 57.86 bilioni. Programu hii itatekelezwa kupitia Programu ndogo zifuatazo:-

   a. Programu ndogo ya Usimamizi wa Hazina inaombewa TZS 39.1 bilioni.

   b. Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali inaombewa TZS 16.1 bilioni.

   c. Programu ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje inaombewa TZS 370.4 milioni.

   d. Programu ndogo ya Usimamizi wa Hesabu za ndani inaombewa TZS 1.53 bilioni.

   e. Programu ndogo ya Kusimamia Sekta ya Fedha na Mapato yatokanayo na Kodi inaombewa TZS 783.4 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, programu ya pili ni programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma inakadiriwa kutumia TZS 19.92 bilioni yenye Programu ndogo zifuatazo:-

   a. Programu ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma ambayo inaombewa jumla TZS 17.91 bilioni.

   b. Programu ndogo ya Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali ambayo inaombewa TZS
   2.01 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, programu ya tatu ni Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha inakadiriwa kutumia TZS 77.00 bilioni; ambayo itatekelezwa kupitia Programu ndogo zifuatazo:-

   a. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara inayoombewa TZS 5.33 bilioni;

   b. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha inayoombewa TZS 69.91 bilioni; na

   c. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezani wa shughuli za Wizara Pemba inayoombewa TZS 1.75 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, programu ya nne ni Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali inakadiriwa kutumia TZS 134.04 bilioni; kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo inaombewa idhini ya kutumia TZS 134.04 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, **p**rogramu ya tano ni ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi imekadiriwa kutumia TZS 1.62 bilioni. Programu hii ina Programu ndogo zifuatazo:-

a. Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini ambayo inaombewa TZS 913.2 milioni;

b. Programu ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Maswala ya Idadi ya Watu ambayo inaombewa TZS 407.3 milioni; na

c. Programu ndogo ya Ufatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo ambayo inaombewa TZS 304.0 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya sita inayokadiriwa kutumia TZS 3.403 bilioni na itatekelezwa kupitia Programu ndogo zifuatazo:-

d. Programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi ambayo inaombewa TZS 385.0 milioni;

e. Programu ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi ambayo inayoombewa TZS 80 milioni na

c. Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Takwimu Zanzibar ambayo inayoombewa TZS
2.94 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti**,** programu ya saba na ya mwisho ni Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango inayokadiriwa kutumia TZS 1.79 bilioni. Programu hii ina Programu ndogo zifuatazo:-

a. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango ambayo inaombewa TZS 1.72 bilioni; na

b. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango Pemba inayoombewa kuidhinishiwa TZS 70 milioni.

MIRADI YA WIZARA ITAYOTEKELEZWA KWA MWAKA 2018-2019

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa miradi, Wizara inatarajia kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Serikali uliopangiwa kutumia TZS 15.0 bilioni;

ii. Mradi wa Kuimarisha Huduma za Jamii ni TZS 52.00 bilioni;

iii. Mradi wa kuimarisha upatikanaji wa Rasilimali Fedha ni TZS 1.00 bilioni;

iv. Mradi wa Kusimamia Utawala Bora *(ISPGG III)* ni TZS 6.85 bilioni;

v. Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Mali Asili umepangiwa kutumia TZS 4.18 bilioni;

vi. Programu ya Kusaidia Taasisi Zisizo za Kiserikali-Zanzibar unatarajiwa kutumia TZS 250.20 milioni;

vii. Programu ya Kuimarisha Maendeleo Endelevu itatumia TZS 273.29 bilioni; na

viii. Mradi wa Uendelezaji wa Bandari ya Mpigaduri Mangapwani ni TZS 4.2 bilioni.

MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA

Bodi ya Mapato-Zanzibar *(ZRB)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018-2019, Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 485.33 bilioni ikiwa ni wastani wa TZS 40.44 bilioni kwa mwezi. Kati ya fedha hizo, TZS 405.33 zinatokana na vianzio vya kodi na ada mbali mbali na TZS 80.0 ni mapato ya Mawizara na gawio la Mashirika.

Lengo hilo la mapato kwa mwaka 2018-2019 linaashiria ukuaji ikilinganishwa na makusanyo halisi yanayotarajiwa hadi Juni, 2018 ya TZS 485.33 bilioni. Mapato ya kodi yanatarajiwa kukua kwa asilimia 16 kufikia TZS 728.35 bilioni zinazotarajiwa kwa mwaka 2018/2019 kutoka TZS 627.01 mwaka 2017/2018, wakati ukuaji wa mapato yasiyo ya kodi unatarajiwa kuwa asilimia 87 kufikia TZS 42.03 bilioni kwa mwaka 2018/2019 kutoka TZS 22.42 bilioni mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria, *ZRB* itapatiwa ruzuku ya asilimia tano ya mapato inayokusanya moja kwa moja, sawa na TZS 18.25 bilioni. Mbali na ukusanyaji wa mapato *ZRB* pia itatekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa elimu kwa walipakodi na wananchi kwa ujumla kupitia njia mbali mbali ikiwemo Semina, Mikutano, Matangazo kupitia TV na vyombo vyengine vya kupasha habari, kushajihisha ulipaji wa kodi kwa hiari, kupiga vita magendo ya mafuta, utoaji wa risiti pamoja na kujua umuhimu wa kodi kwa Serikali;

ii. Kutayarisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa huduma kwa wateja *(e-services);* ikiwemo kukamilisha ufungaji wa mfumo wa risiti za elektroniki *(EFDS);*

iii. Kuendelea na taratibu za ujenzi wa jengo la Ofisi ya *ZRB* - Pemba;

iv. Kuanza maandalizi ya ujenzi wa Ofisi za *ZRB* katika Mikoa yote ya Zanzibar;

v. Kukamilisha moduli ya madeni na ukaguzi wa ndani kwa lengo la kupata taarifa katika mtandao wa kompyuta;

vi. Kuendeleza ukaguzi wa walipakodi ikiwemo Sekta ya Utalii; na

vii. Kuendeleza na shughuli nyengine za kawaida zinazotekelezwa na *ZRB* zilizolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi *(ZIPA)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018-2019, *ZIPA* inatarajiwa kukusanya TZS 3.75 bilioni ambapo TZS 2.46 bilioni ni kutoka katika vyanzo vyake vya ndani, TZS 634.24 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 650.00 milioni ni Ruzuku kutoka Serikalini.
Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2018-2019, *ZIPA* imeelekeza nguvu zaidi katika kutimiza vipaumbele vikuu vitatu vya MKUZA III kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha Sekta ya Utalii - *ZIPA* itafanya utafiti wa soko jipya la utalii ili kutangaza na kushajihisha uwekezaji kwa kulenga wawekezaji kutoka nchi za Asia ya mbali, Ulaya Mashariki na nchi za Ghuba;

ii. Mamlaka itaendelea kuratibu uwekezaji wa mji mpya wa biashara Fumba;

iii. Kuimarisha Sekta ya Kilimo (Kilimo, Mifugo na Uvuvi) *ZIPA* itaendeleza jitihada za kutangaza fursa zilizopo za uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na kutafuta wawekezaji watakaoshirikiana na Serikali na wadau wengine kuwekeza katika sekta hiyo;

iv. *ZIPA* itaandaa Mpango Mkuu wa Kina wa uwekezaji (*Detailed Plan*) katika mtaa wa viwanda (*Industrial Park*) eneo la hekta 100 tayari limeshatengwa; na

v. *ZIPA* itatayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi (*Land Use Plan*) wa maeneo huru ya Micheweni Pemba.

Mfuko wa Barabara *(ZRF)*

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2018-2019 unatarajia kukusanya TZS 15.63 bilioni kutoka vyanzo vifuatavyo:

i. TZS 13.54 bilioni zitakazokusanywa katika tozo ya TZS 100 kwa kila lita ya petroli au dizeli inayoingizwa nchini;

ii. TZS 2.02 bilioni ambazo zitakusanywa kupitia tozo ya TZS 100 kwa kila kipando cha moto kinachoingizwa nchini; na

iii. TZS 84.97 milioni zitakazopokelewa ikiwa ni kodi ya pango la ofisi katika jengo la Mfuko wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko umepanga kutumia jumla ya TZS 15.63 bilioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Matengenezo ya barabara kuu kwa kutumia TZS 11.96 bilioni;

ii. Matengenezo ya barabara za ndani yanatarajiwa kutumia TZS 2.11 bilioni; na

iii. TZS 1.56 bilioni zitatumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za kawaida za mfuko.

Shirika la Bima la Zanzibar *(ZIC)*

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima kwa mwaka 2018-2019 linatarajia kukusanya jumla ya TZS 28.5 billioni kutoka katika vianzio vyake vya mapato. Shirika limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuongeza idadi ya wateja wa biashara zisizokuwa za magari katika mtandao wa Shirika;

ii. Kufuatilia matatizo ya wateja baada ya kuwapa huduma;

iii. Kuzidisha mashirikiano kwa mawakala na madalali na kuwapatia vivutio zaidi; na

iv. Kutoa taaluma kwa wananchi na taasisi mbali mbali juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya TZS 12.85 bilioni ikijumuisha matumizi yafuatayo:

i. Matumizi kwa kazi za kawaida ya kuendeshea shughuli za Shirika ni TZS 6.60 bilioni;

ii. Matumizi kwa kazi za maendeleo ni TZS 4.3 bilioni. Fedha hizi zimepangiwa kukidhi mahitaji ya ununuzi wa vitendea kazi Makao Makuu na ofisi zote za Kanda, gharama za ununuzi wa mtandao mpya ya Shirika, gharama za kufanya tathmini Mfuko wa Shirika (*General Insurance Fund*) na gharama za ukarabati wa jengo la ofisi ya Shirika namba 559 liliopo Vuga; na

iii. TZS 1.3 billioni zinatarajiwa kuwekezwa katika amana za muda mrefu (*fixed deposit*); TZS 500 milioni katika Dhamana za Hazina (*Treasury Bills*) na TZS 150 milioni katika ununuzi wa hisa kwenye makampuni tofauti.

Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2018 *PBZ* imekadiria kukusanya jumla ya TZS 70.5 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 8 zaidi ya makisio ya mwaka 2017 ya TZS 65.3 bilioni.
Mapato yatokanayo na riba za mikopo na uwekezaji yanatarajiwa kufikia TZS 49.5 bilioni sawa na asilimia 70 ya mapato yote.
Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi *PBZ* inatarajia kutumia jumla ya TZS 54.7 bilioni kwa kazi za kawaida na TZS 15.5 bilioni kwa kazi za maendeleo.
Mhe. Mwenyekiti, mambo makuu yatakayoshughulikiwa na *PBZ* ni kama ifuatavyo:

i. Kukamilisha uwekaji wa mtandao wa Shughuli Kuu za Kibenki *(Core Banking System);*

ii. Kuweka miundombinu ya mtandao na vifaa vya kuwekea taarifa *(Servers, Network Equipment and Storage);*

iii. Kuanza ujenzi wa majengo ya ofisi Mazizini na Malindi;

iv. Uwekaji wa njia kuu ya mawasiliano kati ya benki *(Revenue Gateway);*

v. Kuanzisha *Agency Banking*; na

vi. Kuanzisha rasmi utoaji wa mikopo kwa wastaafu.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018-2019 mfuko unategemea kukusanya mapato ya jumla TZS 116.95 bilioni. Jumla ya TZS 71.45 bilioni zinatarajiwa kutokaka na makusanyo ya michango ya wanachama na TZS 45.52 bilioni ni kutokana na mapato ya uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na matumizi Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unategemea kutumia jumla ya TZS 116.95 bilioni ikijumuisha matumizi yafuatayo:

i. TZS 7.14 bilioni kwa uendeshaji wa shughuli za Mfuko;

ii. TZS 30.13 bilioni kulipia mafao ya wanachama; na

iii. TZS 79.65 bilioni kwa ajili ya Uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, mambo makuu yatakayotekelezwa na *ZSSF* ni pamoja na:

i. Kuongeza wigo wa wanachama kutoka ukuaji wa asilimia 6 hadi 8 kwa mwaka katika sekta rasmi na isiyo rasmi;

ii. Kuuendeleza ujenzi wa Mradi wa Nyumba za Mbweni, Mradi wa Michenzani Makontena na kuanza kwa Mradi wa Nyumba za Kwahani; na

iii. Kuongeza usahihi wa kumbukumbu na taarifa za wanachama kutoka asilimia 50 iliyopo sasa hadi asilimia 85.

Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018-2019, Mamlaka ya Usimamizi na Uondoshwaji wa Mali za Serikali inatarajia kupokea ruzuku ya TZS 2.1 bilioni kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Ulipaji wa mshahara kwa wafanyakazi wa Mamlaka ni TZS 890.00 milioni; na

ii. TZS 1.12 bilioni zitatumika kuendeshea shughuli za kawaida za Mamlaka zikiwemo:

a. Kujenga uwezo wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali namba 11 ya 2016 kwa Wakuu wa Vitengo wa Ununuzi, Wajumbe wa Bodi za Zabuni, Watendaji Wakuu wa Serikali pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

b. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali ili waweze kusimamia vyema majukumu yao;

c. Kuendesha Vikao vya Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Kamati mbali mbali ili kukidhi mahitaji ya Sheria; na

d. Kununua vifaa mbali mbali kwa ajili ya utendaji wa kazi za Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali *(OCGS)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2018-2019, Ofisi ya Mtakwimu wa Serikali inaombewa Ruzuku ya TZS 2.9 bilioni kutoka Serikalini. Fedha hizi zinajumuisha TZS 1.46 bilioni za mishahara na TZS 1.47 kwa kazi za kawaida. Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

i. Kuratibu, kusimamia, kukusanya na utoaji wa takwimu rasmi kwa ajili ya kujitathmini ;

ii. Kufanya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kwa mwaka 2018-2019;

iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utawala ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo kitaaluma watumishi;

iv. Kuendelea kutoa ripoti za kila mwezi za hali ya bei na mfumko wa bei nchini; na

v. Kufanya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii *(Social Economic Services)* kwa mwaka 2018 na kutoa taarifa zake.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kukamilisha hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, naomba kuzishukuru sana nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yaliyojitolea kuisaidia Serikali na Wizara kuweza kutekeleza majukumu tuliyojipangia.

Aidha, nazishukuru pia Taasisi na Asasi za Kiraia pamoja na sekta binafsi kwa mashirikiano yao ya kila siku. Naomba wote watambue kuwa sisi tunafarijika sana na mashirikiano haya muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena, naomba kukushukuru sana wewe binafsi, lakini pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Spika wa Baraza hili, Mhe. Naibu Spika wa Baraza hili, pamoja na Mhe. Mwenyekiti Bi Mwanaasha Khamis Juma kwa mashirikiano yenu makubwa mnayotupatia katika Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Shukrani maalum ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, lakini pia shukrani zetu ziende kwa Makamu wake Mhe. Hamida Abdalla Issa, na tunawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa miongozo yao ya mara kwa mara. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia na wanaoipatia Wizara yetu ikiwa tunatekeleza majukumu ya Serikali yetu. Mashirikiano makubwa tunayoendelea kupata kwa Uongozi na Wajumbe wa Baraza hili yametusaidia sana kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kazi yangu inanufaika sana na utendaji makini wa wasaidizi wangu na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa dhati kabisa ninawashukuru sana watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu mahiri, Ndg. Khamis Mussa

Omar, Katibu Mtendaji - Tume ya Mipango, Ndg. Juma Hassan Reli, Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Iddi Haji Makame, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bi Mwanahija Almas Ali na Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii Unguja na Pemba kwa juhudi zao za kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninawashukuru wananchi wote wa visiwa vya Zanzibar kwa kudumisha amani ya nchi yetu ambayo inatuwezesha kutimiza wajibu wetu kwao kwa ufanisi. Shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Donge walionichagua kuwawakilisha katika Baraza hili kwa imani yao kubwa kwangu, mashirikiano yasiyo na mfano na uvumilivu wao unaoniwezesha kutimiza majukumu ya Taifa, kwao wao na kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, mara hii tumepata neema ya kuwasilisha Mapendekezo ya Bajeti za Wizara zetu tukiwa tuko katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Pamoja na swaumu inayoendelea, ufanisi wa kazi zetu katika Baraza hili haukutetereka. Nachukua fursa hii kuwatakia funga njema, msamaha wa Muumba wetu na matayarisho mema ya kusherehekea sikukuu ya Iddi - el - Fitri kwenu nyinyi wote na kwangu mimi pia.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu tumebahatika pia kupata neema ya mvua kubwa za masika zilizonyesha hivi karibuni. Naomba kutumia nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Zanzibar, Tanzania na Afrika Mashariki ambao kwa namna moja au nyengine waliathiriwa na barka hiyo ya mvua ya masika. Tuendelee kukumbushana juu ya kuchukua hadhari dhidi ya maradhi ya miripuko yanayoweza kusababishwa na mvua zinazomalizika. Sote tunapaswa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wetu wa afya ikiwemo kuweka usafi wa mazingira yetu, kuhifadhi vyema vyakula na kuchemsha maji kabla ya kunywa.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo niliyoyatoa, kwa heshima na taadhima, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umoja wao kuidhinisha Mapendekezo ya Ukusanyaji wa Mapato ya TZS 1.28 trilioni zitakazokusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018-2019. Aidha, Wizara iweze kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka huu, nawaomba pia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kuidhinisha jumla ya matumizi ya TZS 295.62 bilioni kwa mafungu F01, F02 na F03. Maelezo na shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka huu yanapatikana katika Kitabu cha 3 *(Volume 3)* cha Bajeti ya Serikali.

T. VIAMBATANISHO

TABLE

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Khalid Salum Mohamed, sasa Waheshimiwa Wajumbe ni wakati wa kuweza kuchangia. Samahani nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo aje kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Allah, mwingi wa rehma kwa uwezo na mapenzi yake ya kutukutanisha hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie uzima na akipe kheri na baraka kikao chetu hiki hususan tukiwa katika kumi hili la tatu la kuachwa huru na moto la mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan. Aidha, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa, wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa namshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu kwa busara na uadilifu wa hali ya juu unaopelekea wananchi wetu kuzidi kujenga imani kwake. Tunawaomba wananchi waendelee kumuamini pamoja na kumpatia mashirikiano ya hali na mali hususan katika kudumisha amani na utulivu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, tunazidi kumpongeza Mhe. Rais kwa kutekeleza ahadi zake alizozitoa katika Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2015 alipokuwa akitetea kiti chake cha Urais katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, salamu za pekee zimuendee Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa hekima na uwezo wake mkubwa aliojaaliwa kuwa nao hususan katika usimamizi wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili muhimu la kuwawakilisha wananchi. Kwa kweli ni kiongozi wa kupigiwa mfano ambapo nasi Waheshimiwa Wajumbe tunatakiwa tuchote busara na hekima kutoka kwake ili tuweze kuwaongoza vyema wananchi wetu katika Majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa viongozi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zake hususan Mhe. Waziri, Dkt. Khalid Salum Mohamed, Katibu Mkuu Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu, Maalim Iddi Makame Haji, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bi Mwanahija Almas Ali, Afisa Mdhamini, Ibrahim Saleh Juma na watendaji wote wa Wizara hii kwa utekelezaji mzuri wa malengo yao waliyojipangia katika mwaka wa fedha 2017/2018. Vile vile, Kamati inawashukuru sana kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia yaliyoiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake pasi na kuwepo kikwazo cha aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, kwa kuthamini na kutambua michango na ushauri uliotolewa na Kamati yetu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ya Fedha na Mipango, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Makatibu ambao wametusaidia ipasavyo katika kutekeleza majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe
5. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
6. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
8. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

9. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imepitia na kujadili mafungu yote ya Wizara hii na kufanya baadhi ya marekebisho madogo madogo na hatimae Kamati iliyaridhia na kuyapitisha Makadirio ya Mapato ya shilingi 1.28 trilioni ikiwa ni mapato kupitia vyanzo mbali mbali vya Serikali sawa na ongezeko la 22 milioni ukilinganisha na makadirio ya mapato ya mwaka 2017/2018 ya 1.06 trilioni. Kwa upande wa makadirio ya matumizi, Kamati iliridhia jumla ya shilingi 154.76 bilioni kwa Wizara hii ya Fedha na Mipango, jumla ya shilingi 134.04 bilioni kwa Mfuko Mkuu wa Serikali na jumla ya shilingi 6.82 bilioni kwa Tume ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa programu mbali mbali za Wizara hii ambazo Kamati yetu imezitolea ushauri na maelekezo kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Fedha na Mipango pekee ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 22.40 bilioni kutoka vyanzo vyake vya mapato vinavyokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar, gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania, gawio kutoka Mashirika ya Serikali pamoja na Bohari za Serikali. Hadi kufikia Machi, 2018 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 18.57 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya mwaka 2017/2018. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa ongezeko hilo la mapato na inaitaka kuongeza juhudi ili mapato yaongezeke mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imefarijika sana kuona matunda hayo yamepatikana, lakini Kamati yetu bado inasisitiza kwamba kuna vyanzo vyengine Wizara haijavifanyia kazi ipasavyo ambavyo kama vitafanyiwa kazi kikamilifu vitaweza kuiingizia na kuiongezea mapato maradufu Serikali yetu, ikiwemo kuanzisha utaratibu mpya wa uvunaji wa rasilimali ya mchanga kwa upande wa Pemba na rasilimali nyengine za mawe na kifusi, pamoja na ukusanyaji wa Kodi ya Mali. *(Property Tax).*

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaiomba Wizara inapopanga viwango vya fedha za makusanyo kwa Taasisi za Serikali ni busara ikazingatia hali halisi ya makusanyo ya Taasisi husika kwani imebainika kuwa kuna baadhi ya Taasisi hizo huwekewa makadirio makubwa ya makusanyo ukilinganisha na uwezo wa makusanyo ya Taasisi hizo. Sambamba na hilo, Kamati yetu inaelewa juhudi zinazochukuliwa na Wizara hii katika kuhakikisha suala zima la ugatuzi linafanyiwa kazi ipasavyo kwa kutoa milioni 300 zitakazotumika kusimamia zoezi hilo. Kamati inaitaka Wizara pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kusimamia matumizi ya fedha hizo ili ziweze kutumika vizuri na kuleta tija iliyokusudiwa kulingana na thamani halisi ya fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukusanyaji wa mapato sio la Wizara ya Fedha na Mipango peke yake, bali hata sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi tuna jukumu kubwa la kuhakikisha mapato ya Serikali yanaongezeka kwa kuwahamasisha wananchi wetu kwenye Majimbo yetu kudai risiti kila wanaponunua bidhaa au kupatiwa huduma, kwani kuna baadhi ya manunuzi yanafanyika ama mnunuzi hadai risiti au hata kama anadai basi hapatiwi risiti hiyo. Hili linatokea sana katika maduka ya vyakula, nguo, vifaa na hata katika vituo vya uuzaji na ununuzi wa mafuta. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha ununuzi wa mashine za elektroniki za *EFD* ili Serikali iongeze wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango imeundwa na baadhi ya Taasisi zinazojitegemea kimafungu. Hivyo, Bajeti ya Wizara hii inatekelezwa kupitia mafungu makuu matatu (3) yanayojumuisha Fungu FO1 linalokusanya programu zote za Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu F02 la Mfuko Mkuu wa Serikali na Fungu F03 linaloelezea Programu za Tume ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu ilipokuwa ikipitia Mapato ya Idara ya Forodha *(TRA - Zanzibar)*, iligundua kwamba kifungu kinachoelezea Faini ya Uingizaji Bidhaa mapato yake yameongezeka maradufu kwa tofauti ya ongezeko la shilingi 116.61 milioni, ambapo mwaka 2018/2019 imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 189.53 milioni, lakini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kifungu hicho kilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 72.92 milioni. Kamati yetu imetaka kujua sababu ya kuwepo ongezeko hilo. Aidha, Kamati yetu pia ilidadisi mapato ya kifungu cha Idara ya Kodi za Ndani *(TRA - Zanzibar)* kinachohusu Mapato ya Wafanyakazi wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar (*PAYE*) kwamba yameongezeka kutoka jumla ya shilingi 46.75 bilioni kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na jumla ya shilingi 58.83 bilioni kwa mwaka 2018/2019 sawa na tofauti ya shilingi 12.08 bilioni ukilinganisha na mapato ya mwaka huu tunaoumaliza.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu pia ilijadili kifungu cha Uuzaji wa Vifaa Vikongwe ambapo kwa mwaka 2018/2019 kifungu hicho kimepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 286.82 milioni lakini hakuna hata shilingi moja iliyoainishwa katika kifungu hicho kwa mwaka huu wa 2017/2018. Wizara iliielekeza Kamati kwamba mapato hayo hayaonekani kwa sababu ya kuanzishwa kwa Mamlaka mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali isipokuwa yanaonekana katika Idara ya Uhakiki Mali yenye shilingi 200 milioni.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, kupitia programu hii, Wizara imetumia jumla ya shilingi 17.77 bilioni kwa kulipia viinua mgongo kwa wastaafu 1,104 na jumla ya shilingi 16.56 bilioni kwa malipo ya pencheni kwa wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hata hivyo, bado kuna wafanyakazi wetu wanaostaafu wanachelewa sana kupatiwa maslahi yao ya viinua mgongo pamoja na kwamba utaratibu wa matayarisho ya viinua mgongo hivyo huwa unaanzia katika Wizara au Taasisi ambayo mtumishi amemalizia utumishi wake. Hali hii husababisha malalamiko na uduni wa maisha yao kwani hadi Kamati inaandaa hotuba hii kuna baadhi ya watumishi wamestaafu tangu mwaka jana na viinua mgongo vyao bado havijalipwa. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango itekeleze kivitendo usemi unaohitaji mfanyakazi *kulipwa ujira wake kabla jasho lake halijakauka.* Ikiwezekana wastaafu wasizidi miezi mitatu tokea wamalize utumishi wao wawe tayari wameshapatiwa maslahi yao. Aidha, Kamati yetu inaiomba Wizara kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha inafuatilia katika Wizara na Taasisi za Serikali ili waweze kuelewa changamoto zinazosababisha kuchelewa kufika kwa fomu za maombi ya maslahi ya wastaafu wetu katika Wizara ya Fedha na Mipango na kuzitatua ili waweze kuwaenzi na kuwaondolea khofu wafanyakazi wetu kuhusu hatma ya maisha yao baada ya kustaafu.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya shilngi 9.51 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2018 programu hii iliingiziwa jumla ya shilingi 5.26 bilioni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Kupitia programu hii, Kamati yetu imeridhishwa na hatua ya ujenzi wa majengo mapya matatu na ya kisasa huko Pemba ambao umezingatia watu wenye mahitaji

maalum. Majengo hayo yatatumiwa na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Juhudi kama hizi zinafaa kuungwa mkono na Wizara na Taasisi nyengine ambazo bado hazijakuwa na majengo ya kisasa. Aidha, Kamati yetu inaisisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha kuanza ujenzi wa ofisi yake kwa upande wa Unguja ili iweze kuwaondolea wafanyakazi kero ya ukosefu wa eneo la kutosha la kufanyia kazi, kwani hivi sasa kuna idara na vitengo kama cha *Payroll* kinafanya kazi katika mazingira yasiyokuwa na nafasi ya kutosha na kurudisha nyuma ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Mhe. Mwenyekiti, programu hii imekamilisha ujenzi wa ukuta wa Mizingani - Forodhani kupitia Mradi wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Fedha kwa kujenga ukuta wa kuzuia maji yasiweze kuvamia eneo la ardhi linalotumiwa na wananchi wetu, ujenzi wa barabara, njia za wanaokwenda kwa miguu pamoja na bustani zake. Kamati yetu inaipongeza Wizara kwa utekelezaji mzuri wa ujenzi katika maeneo hayo ambapo tayari umeshakamilika. Sambamba na hilo, Kamati yetu imefarijika na ujenzi wa misingi ya maji ya mvua katika eneo la Darajabovu hadi Saateni, msingi wa Kwabinti Hamrani hadi Kilimani, ujenzi wa msingi wa Kwamzushi hadi Mtopepo ambayo imekamilika na kuwaepusha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo dhidi ya maafa ya mvua za masika zilizonyesha msimu huu. Aidha, Wizara ihakikishe inaandaa mpango madhubuti wa kuondosha tatizo la maji yaliyotuama katika eneo la Mwanakwerekwe, Ziwa maboga na Kibonde mzungu ili kupunguza maafa na mafuriko kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inazitaka Taasisi zote zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi na udhibiti wa ujenzi holela kuhakikisha maeneo yote yaliyolipwa fidia katika Mradi wa Mtaro wa Kwabinti Hamrani hakuna jengo litakalojengwa tena karibu na mtaro huo ili mtaro huo uweze kudumu kwa muda mrefu zaidi. Programu hii pia imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Mji la Chake Chake na kuliingizia samani jengo hilo, wakati jengo la Mabaraza ya Miji Wete na Mkoani yamefanyiwa ukarabati mkubwa na kuwekewa samani. Mafanikio hayo yasingelipatikana pasi na kuwepo kwa usimamizi mzuri wa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA UCHUMI MKUU NA TAKWIMU

Mhe. Mwenyekiti, programu hii imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Mazizini ambapo sote ni mashuhuda kwamba jengo hilo limekamilika ujenzi wake, ununuzi wa samani na tayari jengo hilo linatumiwa na watendaji wa ofisi hiyo. Kamati haina budi kuipongeza Wizara kwa usimamizi mzuri wa ujenzi huo na kuitaka Ofisi ya Mtakwimu kulitunza jengo hilo kwa manufaa yetu sisi na vizazi vijavyo, kuthamini fedha nyingi zilizotumika ili liweze kudumu kwa muda mrefu kama lilivyokadiriwa.

PROGRAMU YA KURATIBU MIPANGO YA KITAIFA NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kuchapisha na kutoa mafunzo ya ujazaji wa Madaftari ya Shehia kwa Masheha na Wasaidizi wao Unguja na Pemba. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, Wizara hukabiliwa na changamoto kadhaa zinazorudisha nyuma ufanisi wa kazi

zao ikiwemo mahitaji ya gharama kubwa za utoaji elimu pamoja na kukosekana kwa mwamko kwa wananchi wetu kuhusu utoaji wa taarifa za vizazi na vifo kwa kipindi ambacho mtu anajifungua au anafiliwa na mtu wake. Kamati yetu inatoa wito kwetu sisi Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi wetu tueleweshane umuhimu wa kuwasilisha taarifa zetu kwa Masheha ili kupatikane taarifa sahihi za vizazi na vifo kwa lengo la kuiwezesha Serikali kupanga mipango yake ya maendeleo iliyo sahihi kwa maslahi ya wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kukaa pamoja na Wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa ili kutatua tatizo la ukosefu wa mafunzo kwa baadhi ya Masheha na wasaidizi wao kunakosababishwa na kubadilishwa kwa Sheha ambaye tayari ameshapatiwa mafunzo na kuteuliwa Sheha mpya ambaye nae huwa anaunda Kamati yake na kuteua Wajumbe wengine na kuacha kumteua hata Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Sheha aliyepita. Kuendelea kuwepo changamoto hii kutaisababisha Serikali kutumia rasilimali fedha kwa shehia ambazo tayari zimeshapatiwa mafunzo. Kamati inashauri ni busara iwapo atateuliwa Sheha mpya basi japo Wajumbe wawili wa zamani wabakishwe ili waweze kuwapa uelewa Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Sheha mpya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea programu hizo za Wizara ya Fedha na Mipango, kutokana na umuhimu wa Taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii, sasa naomba nizielezee baadhi ya Taasisi hizo kama ifuatavyo:

BODI YA MAPATO ZANZIBAR *(ZRB)* NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA - ZANZIBAR *(TRA)*

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zina jukumu la kukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia Machi, 2018 *ZRB* imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 238.96 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya shilingi 269.5 bilioni zilizopangwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi tisa. Kwa upande wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania - Zanzibar imekusanya jumla ya shilingi 190.51 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya shilingi 193.2 bilioni zilizopangwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi tisa. Kamati inaendelea kutoa pongezi za dhati kwa watendaji wa Taasisi mbili hizo kwa ubunifu wao wa kufuatilia na kuwahamasisha walipa kodi walipe kwa hiari bila ya kushurutishwa pamoja na kutafuta njia mbadala za kuongeza mapato kupitia vyanzo vya mapato viliopo bila ya ongezeko lolote la kodi. Kamati yetu inaendelea kuzisisitiza Taasisi hizo kwamba waongeze juhudi ili waweze kukamilisha makusanyo yaliyobaki kwa kipindi cha Aprili – Juni, 2018.

Aidha, Kamati yetu inawataka watendaji wa Taasisi hizo wasibweteke na mafanikio hayo badala yake waongeze bidii zaidi ili mwaka wa fedha 2018/2019 waweze kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato ya jumla ya shilingi 405.36 bilioni kwa *ZRB* na shilingi 301.10 bilioni kwa *TRA.*

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR *(PBZ)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaupongeza Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kwa jitihada na mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika benki hiyo hususan kwa kufunga mashine mpya katika eneo la Saateni na maeneo mengine. Licha ya juhudi hizo zenye tija na mafanikio, Kamati yetu haijaridhishwa na utoaji wa huduma za *ATM* hizo kutokana na kukosekana kwa huduma mara kwa mara za kifedha jambo linalosababisha wananchi wetu kupunguza imani ya kutokuwa na uhakika wa kupata huduma ya kifedha kupitia *ATM Card* hizo kwa muda wa masaa 24 kama yalivyokuwa matarajio yao. Sambamba na hilo, Kamati yetu imehuzunishwa sana na utendaji

wa Wizara kwa kutozipatia utatuzi changamoto zinazozikabili mashine hizo zikiwemo kuharibika mara kwa mara, kupotea au kuruka kwa mtandao pamoja na baadhi ya wakati *ATM* hizo kukosa fedha za kutosha. Kamati inaielekeza Wizara kwamba matarajio ya wananchi wetu kwa matumizi ya *ATM* hizo ni makubwa, hivyo, ni vyema Wizara izibadilishe changamoto hizo na kuwa fursa ya kuwaingizia wao mapato. Aidha, Kamati yetu inaendelea kuitaka Wizara kufanya mambo yafuatayo:-

a. *PBZ* iharakishe inafunga mashine mpya za *ATM* za kuweka na kutoa fedha ili kupunguza msongamano kwenye matawi ya benki hizo.

b. *PBZ* iendelee kuwahimiza na kuwaelimisha wananchi kuhusu utumiaji huduma za kibenki kupitia mitandao mbali mbali ya simu za mkononi *(Mobile Banking);* pamoja na kukamilisha ufungaji wa mfumo mpya wa benki *(Core Banking System).*

c. *PBZ* ihakikishe inajenga jengo jipya litakalowezesha ushindani na benki nyengine na kuimarisha ufanisi wa benki hiyo.

d. *PBZ* ihakikishe inatumia fursa iliyopo ya Soko la Afrika Mashariki kutanua wigo wake wa kibiashara na sio kuishia Tanzania tu; na

e. Kamati inawaomba wateja wa *PBZ* na wananchi wote watumie huduma za *ATM* ambazo zipo katika maeneo mbali mbali. Huduma hizo ni rahisi, salama na bora zaidi hususan katika kupunguza msongamano kama sio kuumaliza kabisa kila ifikapo mwisho wa mwezi. Aidha, sisi Wawakilishi wa wananchi pia tuna jukumu la kuwaelimisha wananchi katika majimbo yetu kuhusu matumizi ya huduma za *ATM*.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII *(ZSSF)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza wizara na watendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake hususan kwa ubunifu wanaouonesha katika kuwekeza fedha za mfuko kwenye miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya nyumba za makaazi ziliopo Mbweni - Unguja na ukarabati wa Jumba la Treni (*Chawl Building*). Kamati ina wasi wasi na mfuko huu kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa mji wa kisasa katika eneo la Kwahani, kwani ina miradi mingi ambayo bado haijaikamilishwa na mengine hata bado hawajaanza kuifanyia kazi. Kwa hivyo, kuwabebesha jukumu jengine la ujenzi wa mji huo wa kisasa wa Kwahani ni kuwakwaza na kudumaza ile miradi inayoendelea nayo wasiweze kuikamilisha kwa wakati.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima la Zanzibar ni shirika ambalo linafanya vizuri kila uchao licha ya ushindani mkubwa uliopo kutoka katika Makampuni mengine yanayotoa huduma hii ya bima hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Kamati inaishauri uongozi wa Shirika la Bima uwe makini na mawakala wao, kwani imebainika baadhi ya mawakala huwa wanapewa uwakala pasi na kuweka fedha ya dhamana baada ya kukabidhiwa vitabu vya bima. Aidha, kamati inaendelea kuzishauri Taasisi na Mashirika ya Serikali ambazo zimekata bima kupitia mawakala wengine, wabadilike na wakate bima zao moja kwa moja kwenye Shirika letu la Bima Zanzibar, kwani ni Shirika lenye uaminifu na uadilifu wa hali ya juu.

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, hii ni mamlaka mpya ambayo imeundwa Septemba, 2017 ambapo hapo awali ilikuwa inafanyakazi zake chini ya usimamizi wa Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Kamati yetu inaipongeza mamlaka hiyo kwa kuanza kutekeleza vizuri majukumu yake kwa kutoa uelewa kwa Wizara na Taasisi kadhaa za Serikali pamoja na kuwawezesha watendaji wao kuwajengea uwezo huko Dar es Salaam kuhusiana na majukumu na uwezo wa mamlaka na vipi wenzao wanatekeleza kazi zao hususan katika utumiaji wa mbinu mpya za kufanya tathmini za ununuzi wenye thamani halisi na fedha zilizotumika katika ununuzi au uondoshaji wa mali za Umma. Kamati yetu inaitaka mamlaka kutoa uelewa kwa taasisi binafsi zinazohusiana na ununuzi na utoaji wa huduma kwa Taasisi za Serikali. Sambamba na hilo, mamlaka ihakikishe inamaliza kuifanyia kazi Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili watendaji wapate meno ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko huu wa Barabara upo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambao una lengo la kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara, kufuatilia na kukagua matumizi ya fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu na imara itakayosaidia harakati za kiuchumi. Kamati inautaka Mfuko wa Barabara utoe fedha za matengenezo ya barabara kwani tumeshuhudia barabara nyingi za mjini na za mashamba zimeharibika kwa mvua za masika zilizonyesha hivi karibuni. Tunawaomba watendaji wa Mfuko wa Barabara wachukue hatua za haraka ili kuzinusuru barabara hizo zisiendelee kuchimbuka na kuruhusu kuweza kupitika vizuri na kwa urahisi zaidi.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Yussuf Hassan Iddi anapenda kuwashukuru sana sana Mhe. Spika, Katibu wa Baraza, Wajumbe wa Baraza, wafanyakazi wote wa Baraza na wananchi wake wa Jimbo la Fuoni kwa msaada wenu mkubwa wa hali na mali mliompatia hususan katika kipindi hiki kigumu alichopitia cha kuugua, hatimae leo Mwenyezi Mungu amemjaalia kupona na kuwa nae katika harakati zetu za kuhakikisha tunawatumikia na kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Kwa niaba yake anasema ahsanteni na anashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kamati yetu imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili tumuwezeshe waziri na watendaji wake kutekeleza na kufanikisha yale waliyojipangia katika mwaka wa fedha ujao kama alivyoomba katika hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Makamu Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti, sasa tunaanza kuchangia hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango na mchangiaji wetu wa mwanzo ambaye ninae hapa ni Mhe. Ali Suleiman Ali akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti yake ya mwaka 2018-2019.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu na viongozi wa taasisi zote za Wizara ya Fedha pamoja na wafanyakazi sehemu mbali mbali kwa kazi nzuri wanayofanya na juhudi yao tunaona hali inavyokwenda katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama wajibu wangu au wajibu wa wawakilishi tuna haki ya kuchangia, lakini ikiwa huna la kusema basi kutoa shukurani na pongezi pia inafaa. Kwa hivyo, mimi nimetanguliza kwanza kusema hilo baadhi ya taasisi nilizozikuta humu nakiri kwamba zote nimeziunga mkono, kwanza hotuba hii nimeikubali kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele.

Mhe. Mwenyekiti, tulivyosomeshwa katika maadili ya kuishi hakuna jambo zuri kuliko kushukuru. Kwa hivyo, mimi nachukua fursa hii kuishukuru kwa dhati kabisa Wizara ya Fedha na Mipango kwa juhudi zao wanazofanya na kazi nzuri wanazofanya na juhudi yake inaonekana katika maendeleo ya nchi yetu. Pia pamoja na hilo kwa usimamizi mkuu wa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni mkuu wa shughuli za serikali kwa mwongozo mzuri anaowapa Wizara ya Fedha na Mipango na kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya mapato ya nchi yetu yamekuwa. Mimi nizipongeze taasisi zote zinazohusika na kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia machache sana. Kwanza katika bajeti hii niseme tu kwamba wengi tuliokuwemo humu tunaipongeza tu, lakini katika kupongeza huko kuna mambo ambayo wamejipangia ni lazima tuipongeze serikali kuona wakati umefika mapato ni uhai wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2018-2019 bajeti hii imekadiria mambo mengi mazuri na ya ufanisi katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Ni mambo ambayo tunategemea kwamba mapato haya yakikusanywa vizuri basi uimara wa mapato yetu katika nchi yatakuwa. Kwa mfano, ukurasa wa 51 mimi nakuja kwenye mapato yatakayokusanywa Mwenyezi Mungu akitujaalia na *inshaallah* yatapatikana. Kifungu cha 92 kwa ruhusa yako naomba nikisome.

> "Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018-2019. Wizara imepangiwa kukusanya TZS 1.28 trilioni ikijumuisha mapato yatakayokusanywa na taasisi zifuatazo:
>
> i. Mapato yatakayokusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar ni TZS 405.36 bilioni;
> ii. Mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Tawi la Zanzibar ni TZS 301.10 bilioni;
> iii. Mapato yatokanayo na kodi ya mishahara ya wafanyakazi wa Taasisi za Muungano wanaofanya kazi Zanzibar ni TZS 21.00 bilioni;
> iv. Ruzuku na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 467.00 bilioni na
> v. Mikopo itakayochukuliwa katika soko la fedha la ndani ni TZS 40.0 bilioni".

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana wizara kwa malengo yake ambayo wamejiwekea na nasema kwamba ili kupatikana mambo haya *ZRB*, *TRA* wazidishe juhudi katika kukusanya mapato hayo ili tufikie malengo. Kubwa ninaloliomba mimi vyombo hivi bado vitoe taaluma kwani wananchi wengi hawaelewi umuhimu wa kupokea risiti na wauza biashara kutoa risiti. Hili ni kero na tatizo ambalo bado tuko nyuma sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunashuhudia baadhi ya maeneo zinauzwa biashara holela sana, unaweza kwenda kununua kama hujui, mimi sikubali, lakini kama mtu hajui si makosa yake anaweza kununua vitu hata milioni 5 au milioni 6 risiti haidai. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana kwa hili serikali inakosa mapato kwa baadhi ya maeneo kwa kutokujua wananchi wetu umuhimu wa kutoa risiti, bila ya kupokea risiti mapato hayapatikani. Naiomba sana wizara na kwa taasisi zetu ambazo zinakusanya mapato taaluma itolewe itasaidia sana wananchi wetu kudai risiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimeamini kwamba ukitembea katika nchi za wenzetu popote utakapokwenda kama umenunua kalamu basi utapewa risiti, kibiriti utapewa risiti, sindano ya kushonea utapewa risiti ina umuhimu wake. Kwa hivyo, bado ningemuomba sana Mhe. Waziri kupitia taasisi zetu watu wakapewa taaluma ili pato la nchi yetu liweze kuongezeka. Lakini nawapongeza *ZRB*, nawapongeza *TRA* na taasisi nyengine kwa juhudi zao wanazoendelea nazo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna mashirika yetu ya bima, Shirika la Bima nalipongeza kwa dhati kabisa. Leo Mhe. Waziri ametutolea kauli nzuri sana asubuhi katika swali ambalo liliulizwa akasema nitaleta kwa maandishi. Ametwambia tu kwamba faida iliyopatikana kwa mwaka uliopita Shirika la Bima limethubutu kufikia bilioni 900 kama sikosei. Kwa hivyo, hiyo ni hatua kubwa na hatua ambayo ya kuigwa, hivyo tuwaambie tu wananchi au watu mbali mbali watumie Shirika letu la Bima ili kuhakikisha kwamba pato linalopatikana faida yake inaingia nchini. Kwa hivyo, mimi nawapongeza wenzetu hawa kwa juhudi yao na matangazo yao.

Kwa bahati nzuri kwenye redio, televisheni wenzetu *PBZ*, wenzetu wa Bima wanaendesha vipindi vizuri na watu wanavipenda. Utamsikia huyu sijui Kigoma nina kijumba changu nitafanya nini, anaambiwa wewe nenda *PBZ* utapata hili, hiyo ndio kutangaza biashara. Kwa hivyo, biashara yoyote inayotanganzwa ndiyo inayotoka, biashara iliyokuwa haina matangazo haitoki.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimeona katika mwelekeo ambao wizara imejipangia kwa makusudi ni kuongeza utalii katika nchi yetu. Kutangaza nchi za nje Asia na kwengineko, hii ni njia moja wapo ambayo itatusaidia utalii tunautegemea kwa hali na mali, na utalii utangazwe ili uje. Kwa hivyo, naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuona hili limepangwa vizuri kuhakikisha kwamba pato la nchi yetu linaongezeka kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nitalisema natoa ushauri au naiomba serikali. Mheshimiwa tulipitisha mswada hapa namuomba sana Mhe. Waziri hili anisikilize. Wazee wetu ambao wanamaliza muda wao wa kazi katika serikali, Mfuko wao wa Hifadhi ya Jamii wameomba sana sheria ile itizamwe upya. Wananchi wetu wanalalamika kwa wingi sana na kama alivyosema Mhe. Rais sisi ndio watumishi wa wananchi wetu wa Zanzibar (Unguja na Pemba). Wananchi wanasema kile walichowekewa bora wapewe wenyewe kwa sababu ukisema unamkata hivyo unakuja kumpa hivi mtu mwengine haelewi. Tunajua kufa ni siku yoyote hata sasa hivi nimesimama hapa Shihata inaweza ikawa ndio mwisho wa kauli yangu, Mwenyezi Mungu anajua yeye na daftari analo yeye. Lakini anasema mfanyakazi akishamaliza muda wake bora apewe chake.

Kwa hivyo, mimi ningeishauri serikali kwa kuwa sheria si msahafu turudi tena tuiangalie upya kwa kuwa kilio hiki waheshimiwa wengi wamepewa malalamiko hayo, wanasema wazee wakishamaliza muda wao wa kufanya kazi fedha zao wakabidhiwe wenyewe kuliko kuekewa wanalipwa kwa mpango ambao umepangwa. Bahati nzuri limepagwa na mpango ni matumizi mimi ningeiomba sana serikali hili likaangaliwa akija Mhe. Waziri labda atupe maelezo tu kwamba linawezekana au lifanyiwe utaratibu gani. Lakini kilio cha wafanyakazi wetu wanasema mtu kafanya kazi miaka 40 au miaka mingapi akimaliza anapata kiinua chake mgongo milioni zake 15 kwa mfano. Sasa katika shilingi 15,000,000 zile hazipati zote wanasema bora sheria ile irudishwe ya zamani si vibaya kwa sababu kudai mema ni moja wapo ya maendeleo, ukidai maovu ndio yatakukuta mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme tu kwamba sina mengi kwa sababu nilitamka mapema kwamba nimeikubali hotuba hii sina matatizo nayo na taasisi zote na mifuko yote naiunga mkono. Ninaloomba mimi serikali kupitia taasisi zetu wafanye bidii ya kukusanya mapato kwa manufaa ya wananchi wetu. Baada ya hayo machache mheshimiwa kwa heshima kabisa nasema tu kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango kwa asilimia mia moja, mimi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali. Naona Mhe. Omar Seif Abeid simuoni hapa kwa hivyo nafasi yake atachukua Mhe. Suleiman Sarahan Said akifuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango. Mheshimiwa mimi awali ya yote kwanza nimshukuru sana Dkt. Ali Mohamed Shein katika juhudi zake za kuiendeleza Zanzibar hasa pahala alipotutoa katika mambo ya utegemezi mpaka sasa tukawa tunajitegemea wenyewe kwenye sekta hii ya fedha. Namshukuru sana katika mipango yake akisaidiwa na msaidizi wake Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kitabu chake ambacho amekifafanua kwa hali ya juu sana.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichangie tu kwamba nimeona humu katika kitabu kuna sehemu ya uondoshaji wa mali za umma. Mhe. Mwenyekiti, kama nakifahamu vizuri ni kwamba uondoshaji wa mali mimi naona labda utaratibu wake haujakaa vizuri sana. Ni kwamba mali za serikali takriban mpaka nyengine haziko tena zinabakisha kama *frame* kama ni gari, kama ni kifaa chochote hatuna utaratibu wa kuondoa na tunajua gari zetu za serikali tunatumia miaka mitano, miaka kumi au vitu gani tunatumia muda gani baadae vitu vichakavu tuviondoe. Tunasubiri mpaka kamati gani ikae, vitu gani vikae kitu kile kinaondoka pale kikiwa na fedha nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ni shahidi tu Waziri wa Fedha na Mipango ameona utaratibu alionao sasa hivi kidogo akiziwahi gari katika muda ambao zinakamatika, basi gari inaweza kuuzika vizuri. Lakini gari nyengine zinapatikana hamna gari, gari ya milioni 50 linakuja kuuzwa shilingi milioni 150, haya ni kwa sababu gari hazina mwelekeo wa kutosha. Kwa hivyo, ningeomba uondoshaji huu Mhe. Waziri akaufanyia tena marekebisho ili tukajua kama gari ya serikali hata kama inakwenda, lakini ikifika muda wa miaka 10 basi gari hii iondoke ili iwekwe nyengine ambayo itakuwa haiharibu pesa ya serikali kwa matengenezo ya kila mara.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba bado Chake Chake kuna ofisi ya *insurance* ambayo haijajengwa, jengo lile watu wake wamemalizwa kulipwa lakini bado

kuna mtu mmoja mle ndani anadai. Mhe. Waziri ningekusihi sana hili suala ukaliingia wewe, kwa sababu inaonekana watu wa *insurance* hawajafanya utafiti wa kutosha kuna mmoja pale hakupata haki yake. Inaweza ikatuletea bughudha, ikatuletea pia matatizo ambayo hata kwa Mwenyezi Mungu sio mazuri mtu amekaa mle zaidi ya miaka 30 au na kuendelea halafu hakupata haki yake. Ningekuomba waziri suala hili ukalitafutia ufumbuzi, nafikiri hata tukikaa mimi na wewe pamoja na Mkuu wa *Insurance* tunaweza tukalitatua pesa ni ndogo lakini lisiharibu jina letu vizuri sana. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri suala hili ukaliingia mwenyewe ukalitatua bado kijana huyu wala si kijana tena ni mzee ana watoto zaidi ya miaka 35 lakini tunamwita kijana.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme kuhusu habari ya kupunguza umaskini. Mheshimiwa suala la kupunguza umaskini linakuja katika njia nyingi sana, serikali inajitahidi kwa hali moja au nyengine. Lakini pia kuna utaratibu mwengine umaskini huwa hauondoki nimeona kwenye kitabu.

Mheshimiwa wawekezaji hawa wakati mwengine wanakuja kwetu wanakuwa sio wawekezaji ambao wana sura nzuri za kibinaadamu, wengine wanakuja huku kuja kututafutia sisi mashaka na baadhi ya wafanyabiashara pia kuanguka kwa sababu zao. Kuna watu wengi wanadai katika mahoteli huko pesa nyingi wawekezaji wapo lakini kuwalipa hawawalipi na hakuna sheria ya kuwahangaikia hawa wanakuwa ni watu wenye tabu sana. Kwa hivyo, tunajaribu na yeye ajaribu tupunguze umaskini, lakini unakuta mtu ana biashara kachukua kwa watu wengine na watu hawa wa mahoteli na maeneo mengine hawalipwi vitu vyao au watu wanaokuja kwenye *contract* na mambo mengine hawawalipi wazawa na sheria haiwabani vya kutosha. Mtu akiondoka hapa ana madeni, ana benki, badala ya kuwa alikuwa ajinasue katika hali hii matokeo yake anakwama anauziwa vitu vyake kwa sababu ambazo mtu huyu hapatikani kisheria au kwa kumfuatilia yeye mwenyewe inakuwa ngumu, mtu yule tayari ameshatumia mali za wananchi ambazo hakulipa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana hawa wawekezaji watakapokuja Mhe. Waziri akawa na sheria ya ununuzi wa vitu vya ndani ambavyo wanasaidiwa na wananchi wa hapa, iwe kuna sheria ya kuwabana au kuwe na kamati maalum ya kuwakamata kabla ya kwenda zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna washirika wa maendeleo, nimeona wamejitahidi sana katika jumla ya mambo yetu ya miradi inayoendelea lakini pia bado tuna tegemezi za mashirika ya maendeleo. Namshauri Mhe. Waziri kwamba washirika wa maendeleo tuwatie katika hesabu wapo washirika wengine ni wazuri sana wanatusaidia kwa nia moja ama nyengine. Washirika wengine wanakuja kama vile na wao waunge mkono lakini hawana nia njema na pakitokea purukushani ndogo inakuwa anatuhukumu kwa ile sehemu ambayo tunafanya au anakuja hapa akiwa na lengo fulani. Ningemshauri sana kama yeye ni kiongozi wetu kwa mambo ya fedha na mipango watu hawa tukawajua kwamba wanaotusaidia kwa nia safi ni wepi, hawa wanatusaidia kwa mguu majanini, mguu njiani ili tukaweza kwenda na bajeti yetu vizuri wasitupunguzie bajeti yetu na kutuweka pahala pabaya.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na tatizo jengine ni kwamba bado suala letu la ujenzi wa nyumba zetu mpya zina mashaka sana. Bado majengo yetu yanavuja ambayo yanagharimu pesa nyingi halafu baadhi ya wakandarasi wengine bado hawajawa wazuri. Kwa sababu Mhe. Waziri nikikwambia mpaka sasa hivi lile jengo langu la Chake Chake la Manispaa linavuja ambalo limefunguliwa juzi kwenye Sherehe za Mapinduzi basi linanitia huruma. Ningeliomba kama taarifa hana akaweza kulikagua akajua kitu gani ambacho kinasababisha kuvuja. Mvua za juzi

zimeingia ndani linaweza likaharibu vitu vingi, ningeomba na hilo likafuatiliwa ili tukaangalia nia njema ya kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niangalie kuhusu habari ya ulipaji wa fidia katika mambo ya barabara. Mheshimiwa sijui tunatumia sheria gani ambayo fidia sasa imekuwa ni *issue* katika mambo ya mipango ya kibiashara. Watu wote wanajua wana *plan* kuliko serikali, wanajua pahala gani patapita njia mtu anakwenda kujenga na utakuja kuikuta *plan* ile inajengwa katikati ya ile nyumba sijui hata watu hawa wanapata *plan* kutoka wapi. Ningeshauri sana Mheshimiwa mipango hii ya serikali ikaweza kuangalia hili suala la barabara linafikia wapi.

Vile vile nataka niulize kwamba hii barabara ya Wete - Chake Chake mwisho wake ni wapi. Inaanza Wete mpaka Maili Tano, inaanza Wete mpaka Chake Chake/Machomane au mpaka mjini. Nataka nijue kwa sababu naona kulikuwa na maelekezo tofauti wengine wanasema labda mwisho Maili Tano lakini watu waliposikia mengine wanajenga kutoka Maili Tano kuja Chake Chake Mjini wanajenga kwenye barabara makusudi kwa sababu walipwe fidia. Kwa hivyo, ningemshauri Mhe. Waziri akatoa maamuzi kwamba watu waliokwishalipwa hao ndio basi.

Pia nije kwenye suala la kukua kwa uchumi. Mheshimiwa kukua kwa uchumi kuna mambo mawili katika dunia, lakini katika nchi kuna mambo ya nchi ambayo inapata miradi mikubwa mikubwa, lakini pia pato la mwananchi la siku moja au la kila siku. Bado nimeona katika kitabu kuna wananchi maskini hasa katika Wilaya ya Mkoani, Micheweni huko, lakini mambo mengi ambayo yanaturudisha nyuma sana pia na serikali kukaa sana na fedha za wananchi ambao maisha yao yaliwategemea. Ningeiomba serikali katika jumla ya kujinasua na kupunguza umaskini ni kuhakikisha serikali haidaiwi na wananchi wake, hili litasaidia sana na mtu mwengine utakuta anafanya kazi miaka yote unamuahidi kwamba atapata kiinua mgongo matokeo yake anakaa mpaka anakufa bila ya kiinua mgongo chake kukipata. *(Makofi)*

Wengine pia wanakuwa na maradhi tunamjua hata kuachishwa kwake kazi ni maradhi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri basi mambo haya ya kiinua mgongo yakaondoka haraka na tuna takwimu nzuri *before*, kabla hata mtu hajakuwa tayari basi kiinua mgongo chake kikae tayari haina haja ya kumsubiri halafu akaja akakitafuta wakati mtu yule kufa kwake anaizulia serikali kwamba sikupata pesa yangu ningekwenda India wakati hata ungempa angeila hapo hapo lakini sababu yote anaitupia serikali. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali ikafanya mambo yake kwamba wale watu wa viinua mgongo na wenye matatizo na hawa ambao wanaovunjiwa nyumba basi ikafanya kila jitihada zake za kuwaweka katika maelekezo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimeona humu katika uwasilishaji wa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji amekuja na *style* mpya juzi ya kutaja kwamba Uwanja wa Ndege ni *Terminal III*. Sasa na humu kwenye kitabu nimeonaUwanja wa Ndege mpya huu ni *Terminal III.* Sasa huu ni *Terminal II* au *Terminal III.* Kama ni *Terminal III, Terminal I* ni ipi, *Terminal II* ni ipi na *Terminal III.* Hebu atakapokuja Mhe. Waziri atupe ufafanuzi wa suala hili maana naona sasa hatujui tuutaje uwanja gani, *Terminal III, Terminal II, Terminal I* hatujui. Kwa hivyo, naona hili suala akatusaidia pia tukajua kwamba uwanja huu utakuwa *Terminal* gani.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie kwamba Wizara ya Fedha na Mipango yeye ndie mwenye mipango yote kila mmoja akitaka kuajiri watu, kutoa ajira kwa vijana na kutoa nafasi nyingi sana. Mheshimiwa hapa sasa hivi hatuna utaratibu maalum wa vijana wetu kupata kazi lakini hasa katika mashirika yanayoletwa, katika mahoteli yanayojengwa na maeneo mengine utaratibu bado watu kutoka nje wana nafasi kubwa kuliko vijana wetu. Tuna maeneo tunawasomesha,

tuna vigezo tumewapatia, lakini kwa nini bado tuna taratibu za kwamba vijana wetu sisi wenyewe hatujachoka au hatujakamilika katika ajira, bado tumeshaanza kutoa ajira kwa watu kwenye nchi kubwa ambazo zina mamlaka hizi. Kwa hivyo, ningeomba kukawa na udhibiti maalum kwa vijana wetu kwanza kupata ajira labda iwe sekta ile hayupo mtu kama yule.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili linalotupunguzia fedha sana na matatizo mengi ni mipango miji. Mipango miji bado haijakamilika, mtu huyu wa mipango miji bado kazi zake hazijakamilika. Lakini tukitazama fedha ambazo tungempa akatutayarishia mipango miji na fedha ambazo zinatoka kwa mipango miji ni fedha nyingi sana zinapotea kwa mipango miji. Watu wanajijengea ovyo, mipango inakuwa ovyo, baadae serikali inarudi kuja kulipa fidia ambazo kwa kweli bora tungekaza roho tukameza fupa tukaweza kupanga mipango miji hata kama hatuna uwezo wa kujenga, lakini tunajua hapa hatuwezi kuingiliwa tena tukaweza kuangalia matatizo yetu.

Pia Mheshimiwa nitoe pongezi sana kwa ofisi zake alizojenga Pemba na nilimshauri katika maelekezo na mimi akanishauri vizuri sana. Mheshimiwa napenda sana ardhi ni mali ya serikali sitegemei tena mpaka kufika mwaka 2020 kwamba bado kutakuwa na ofisi za serikali ziko katika majumba ya kukodi, Mheshimiwa inatupotezea pesa nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika benki ya *PBZ*. Benki hii imeshakuwa benki ya muda mrefu sana ina miaka zaidi ya umri wangu, sasa benki hii inakwenda katika *speed* kubwa sana katika mambo mengi. Lakini ningeshauri tena serikali ipo haja ya kutafuta benki nyengine ya serikali ya maendeleo ili kuipunguzia mzigo *PBZ*. *PBZ* Mheshimiwa ukitaka kufanya biashara zako siku nzima wewe unatafuta. Sasa sisi tunatafuta kodi, tunatafuta pesa ya serikali, lakini kwenda kulipa pesa zako mwenyewe serikalini unachukua siku nzima. Ningeomba sana akaongeza kutaka kufanya maendeleo pamoja na mambo mengi ya ukuzaji uchumi, basi mimi nashauri kwamba ipo haja ya kufunguliwa benki nyengine ya serikali ya maendeleo kuisaidia *PBZ*.

Kwa sababu benki hii ilishafungwa benki nyingi, benki za Konde, Kengeja, Mkoani nazo zilifungwa, leo tayari msongamano umerudi pale pale na benki zimefika mpaka Makunduchi na kwengine. Kwa hivyo, ningeomba kama uwezo wake mdogo ichukuliwe benki nyengine ya maendeleo ya serikali iweze kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena serikali sasa hivi imejikita sana katika gari za serikali katika ukataji wa *insurance* ili serikali kusaidia matatizo yao. Lakini ningeomba tuongoke tena kwenye vikosi, magari ya kijeshi haya ya vikosi vyetu vya JKU basi nazo zikakatiwa *insurance*. Magari haya wakati mwengine yanapata ajali gari za bei kubwa lakini hazikatiwi *insurance* baadae inakuwa ni mzigo wa serikali. Ningeomba pakawa na utaratibu magari haya nayo yakakatiwa *insurance* tena ile *full insurance* ili nayo yakaweza kuwa na bima na zikipata ajali zikaweza kulipwa ili kuisaidia serikali kuondokana na mzigo kama huo.

Pia magari haya nayo yakawa na muda wake wa kuuzwa au kuondoshwa. Mheshimiwa muda mwingi gari hizi zinakuwa mbovu ringi majanini, mguu njiani *brake* zenyewe mashaka. Kwa hivyo, ningeomba sana zikapatiwa *insurance* na vile vile zikatizamwa muda wa kuondoshwa tutakuwa na gari nzuri na gari ambazo zitakuwa na uhakika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mheshimiwa. Pia katika hoja zetu ningeomba tena bado tatizo la usafiri tunalo kubwa sana. Ningeomba kama Zanzibar bado kuna haja ya kuweza kuanzisha shirika letu la ndani la ndege au maboti yetu kama shirika la meli ili kupata mwendo zaidi wa mashirika haya tukafanya vitu kama tulivyofanya huu mradi wa mambo ya TEHAMA, mambo ya Mkonga. Sisi tuna *share* basi tukatafuta mashirika Mheshimiwa tukafanya *share* ya ndege, tukafanya *share* ya boti za kazi ili tukaweza, serikali nayo ikaweza kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia na mimi nitoe rai kwa Mhe. Waziri akatafuta mipango mizuri sana ya kurahisisha zaidi kuliko hapa tulipo katika ulipaji wa ukusanyaji wa kodi ukawa rahisi zaidi watu wakaweza kutoa pesa kwa urahisi, lakini pia ukusanyaji pesa yake mtu ya kulipa kodi isimsumbue.
Mhe. Mwenyekiti, pesa ni kitu kigumu ukimhangaisha mtu tu anasema leo silipi, maana yake anatoa sababu zilizokuwa za msingi. Ningemuomba Mhe. Waziri ana wataalamu wengi akarahisisha sana ulipaji wa pesa ili zikaweza kulipwa kwa urahisi ilimradi isitupe muda. Mheshimiwa muda ni mali sana siku nzima mtu anaipoteza katika mazingira ya kulipa pesa, mazingira ya kutafuta vibali, tungerahisisha sana tukaweza kuangalia vitu ambavyo vitakuwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimuunge mkono sana Mhe. Waziri katika jitihada zake ametuboresha sana tuko katika trilioni 1.28, nafikiri tumepiga hatua kubwa sana lakini bado kunahitajika pesa. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohamed Said na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na nichukue fursa hii pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu huu katika hotuba yetu hii ya Waziri wa Fedha na Mipango. Pia niipongeze Ripoti ya Kamati iliyosomwa na Mjumbe wa Kamati kwa maelezo mazuri. Niseme tu kwamba maelezo yaliyokuwemo katika ripoti hii au hotuba ambayo ameisoma Mhe. Waziri imejitosheleza ina maelezo ya kina na ni utaratibu na sisi pia lazima tuichangie. Kwa hivyo, mimi sitakuwa na maneno mengi lakini naamini yale nitakayoyasema yataweza kumsaidia Mhe. Waziri katika majumuisho yake pamoja na taasisi zake husika.

Kwanza, nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa mahusiano mazuri pamoja na wasaidizi wake wote ambapo mimi mwenyewe binafsi nimekuwa nikifarajika sana, lakini pia na wananchi wa Jimbo la Tunguu jimbo ambalo mara nyingi nikisema jimbo langu au letu maana yake inakuwa kama ni langu peke yangu, mimi naona kama niseme jimbo letu inakuwa ni pamoja. Kwamba wananchi hawa ambao mimi nawawakilisha hapa wanafaidika na mimi kuwepo hapa na kuwa ni msemaji wao.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa jambo moja ambalo anastahiki kupewa. Moja ni kwamba yeye ni waziri ambaye ana mikutano mingi, ana kazi nyingi na anahitajika mara nyingi na mara huzidiwa kuwa yupo ndani mara yuko nje, lakini nithubutu kusema kwamba Mhe. Waziri ni mmoja katika waziri ambaye Barazani mara nyingi unakuwa humkosi na anakuwepo hapa. Tunafurahia sana mimi na Mhe. Suleiman Sarahan Said na ndugu yangu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwamba bado sisi kwa upande wetu tunajiita kuwa siasa ni busara upande huu bado tunaongoza kwamba mawaziri wengi ni wajumbe tunashiriki katika vikao. Kaskazi

watazungumza wao wenyewe hivyo tunafurahi sana kwamba bado kwa upande wetu siasa ni busara tunaendelea kuwepo kuchapa kazi na kuungana na mawaziri wetu bila ya kumsahau Mhe. Mwanasheria Mkuu huku akinitupia macho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nitoe masikitiko yangu. Kwanza, nilizungumza suala la semina nikauliza kwa mfano, ukiangalia katika ripoti kuna maeneo basi Wajumbe wa Baraza hili wanahitaji kupata elimu zaidi, lakini sijui kitu gani kimefanyika katika hii miaka mitatu na Baraza lililokuwepo. Tulikuwa tunasikia zamani tukisoma katika magazeti Wajumbe wa Baraza wanakwenda katika semina wakirudi hivyo wanavyozungumza unaona tofauti yao. Lakini Baraza hili unalikuta wakati mwengine tunahitaji nguvu, inawezekana tunaelewa ndio maana inafika pahala hata watendaji ndani ya wizara kama hii au wizara nyengine unafika kwamba Wajumbe wa Baraza hawajui kitu, ni kweli kama hatujui kwa sababu hatuelewi nini ambacho wakati mwengine tunakijua. Kwa hivyo, watumishi ambao wakati mwengine ni *seniors* ndani ya serikali wanafika pahala kutwambia sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatujui kitu, lakini mimi siwalaumu mambo mengine yanayozungumzwa tunakuwa hatuyajui.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nilikuwa naangalia katika hiki kitabu kuhusu Mfuko wa Barabara, nataka niuchangie lakini Mfuko wa Barabara hata siujui unaanzia wapi, lakini najua kuna fedha ambazo katika kila lita ya mafuta ambayo tunaichangia sisi katika kununua zinakwenda katika barabara zetu. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja atatueleza katika fedha kila lita moja mgawanyiko ni kiasi gani kinaingia serikalini katika hizo shilingi 2,300 ambazo mwananchi anatumia. Kwa mnasaba huo huo, nasema kabisa nazuia mafungu ya PF0101, PF0104 nikiamini wasaidizi wananisikia. Halikadhalika nitahitaji maelezo katika suala hili la semina Mhe. Waziri na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, hapo Nairobi nakusikia tu sijawahi kufika sijui huo mfumo wa bajeti kuweza kuwashauri wananchi na serikali hii, hata hapo Rwanda unaposikia wao wako mbele kamati hii haijawahi kusafiri. Kamati ya Bajeti imefika Dodoma kwa siku mbili kuonana na Mhe. Andrew Chenge tukabadilishana mawazo. Sasa hebu tufikirie tunataka mawazo wenzetu tujifunze. Kwa hivyo, Mhe. Waziri pale anapokuwa na ziada asione tabu kuungana na Kamati zake za Baraza zikamsaidia ili waweze kuwasaidia, tunapopata ile elimu tunaweza kuwasaidia na wengine hatima yake kuweza kuishauri serikali kwa mujibu wa katiba. Hayo ni maombi sio maelekezo Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la biashara na malengo yaliyokuwepo. Nilizungumzia mwaka jana na nitaendelea kuzungumza juu ya *finance bill* na *issue* ya asilimia 18 ya *VAT,* ambayo Wazanzibari au wafanyabiashara wanatakiwa kulipwa wanapofanya manunuzi kwa upande wa Tanzania Bara. Hili kwa kweli ni kero sana na bado tunategemea na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakaposoma *finance bill* yake au Bajeti Kuu tutapata kujua je, itakuwaje. Kwa sababu sasa hivi mtu anafanya manunuzi Tanzania Bara anakuja Zanzibar *ZRB* anamsubiri, 18 na 18 inakuwa 36; anapokwenda kupeleka *claim* zake kule *ZRB* 18 itakuwa imeshapotea mwisho anayeumia ni mlaji.

Sisi kama kisiwa sasa hivi ukiangalia hata katika manunuzi na biashara ambayo Zanzibar tulikuwa tunauza kwa upande wa Tanzania Bara tumeshuka sana. Hata kwa upande wa Tanzania Bara sisi tulikuwa tunafanya manunuzi kuna mabadiliko. Sasa hivi sisi tumekuwa tunanunua lakini leo tunazungumza. Juzi nimewasikia Waheshimiwa wakilalamika kwa sauti kubwa mtu akifika na televisheni tu sasa hivi pale Tanzania Bara imekuwa ni balaa, watu wanaandika mpaka kwenye mitandao ndio maana nikashauri katika biashara hii mnasaba huu. Kwa sababu

tunataka tuongeze mapato yetu, tunataka tukuze biashara, basi kwa yale mambo ambayo tunahisi watu wakifanya biashara na ndugu zetu kutoka Kenya hasa Mombasa tuangalie twende, maana hakuna njia. Sisi ni kisiwa tunataka tufanye manunuzi tuzungumze na Mzee Said Salum Bakhresa meli yake apeleke Mombasa, yuko tayari kujenga bandari kule basi serikali isimamie suala hilo. Mimi niombe Mhe. Waziri kwamba hizo taarifa tayari zipo na mwenyewe Mzee Said Salum Bakhresa yuko *interested* kujenga bandari yake Mombasa na tukijenga bandari kule biashara itachangamka kwa zile bidhaa ambazo zitatengenezwa ndani ya *East Africa Community* wala huwezi kufanya manunuzi hayo Dar es Salam au Morogoro. Kwa sababu Kenya tunajua wao wako mbele basi haina haja mtu akatoka anakwenda zake safari Dubai na wapi. Kwa hiyo, mimi naamini Wizara ya Fedha na Mipango kwa kupitia Tume ya Mipango ambayo ukisoma katika taarifa yao ukurasa wa F02 unasema:

> "Majukumu ya Tume ya Mipango ni kutoa ushauri wa kisheria kwa Mhe. Rais na kwa serikali kwa ujumla katika maeneo yote ya maendeleo ya kitaifa kwa ujumla".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, hii Tume ya Mipango inashindwa kuwasaidia wafanyabiashara na kufunga safari kwenda Tanzania Bara kumwambia Mhe. Dkt. Philip Mpango unaumiza upande wa pili wa Muungano. Sasa tukisubiri *finance bill* leo mtu ananunua biashara vitu vidogo. Kwa hiyo, mimi niwaombe wahusika wa Tume ya Mipango watafute njia ya kushusha hasa kunyanyua biashara Zanzibar lakini kuboresha hizi huduma.

Lakini pia kuangalia katika bidhaa ambazo zinanunuliwa kila siku hizi ndizo ambazo Wazanzibari watafaidikia. Sisemi kama hawafanyi kazi vizuri waongeze juhudi. Mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, ukisoma mstari huu ambao kwenye buku hili Waziri wa Fedha na Mipango ameleta, basi hii Tume ya Mipango baada hiyo tarehe 10/06/2018, baada ya miezi sita Hoteli ya Bwawani kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu na Waziri hapa, kwamba kwa mujibu wa hilo tangazo ambalo litakwisha tarehe 10/07/2018 juu ya Hoteli ya Bwawani, ikiwa mwekezaji atashindwa, basi mradi huu wote ausimamie mwenyewe anayehusika na Tume na Mipango, asipewe mtu yeyote.

Kwa sababu inaelekea Hoteli ya Bwawani ilikuwa na mkono wa wanasiasa ambao wao pia sio ma-*economist* wala hawana uwezo wa kuweza kuyafanya yale ambayo watu wanayajua ndio maana tumefikia hapa leo. Leo tuangalie sijui mimi kazi yangu nimechaguliwa na wananchi kusema, kwa hiyo kazi yangu hapa ni kusema. Kwa hiyo, inasemekana kulikuwa na mfanyabishara mwengine akitaka ile Bwawani tuchukulie nimeota alikuwa Mzee Said Salum Bakhresa, kwa hiyo naendelea kuota Mzee Bakhresa leo ameshamaliza kujenga Mtoni, Hoteli ya Bwawani bado ipo inatuzomea. Ni hatari tumekosea, kwa nini tunakosea mambo kama haya wakati tuna Tume na tuna watu ambao wana nguvu wana uelewa wao.

Kwa hiyo, mimi nashauri sana wanasiasa wafanye kazi zao na wale ambao wana uwezo wayasimamie haya chini ya Waziri wa Fedha na Mipango. Nikuombe sana Mhe. Waziri Hoteli ya Bwawani ikifika mwezi Julai uikamate mwenyewe na watu wako iwe chini yako asiguse mtu yeyote, uje kwetu sisi hapa tukushauri uende zako kwenye *cabinet* tuamue mambo mbele. Lakini hayo yaliyofanyika huku nyuma yasitokezee tena.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *ZRB* niwapongeze kwa kazi nzuri, nichukue nafasi hii pia kumpongeza rafiki yangu, kaka yangu, ndugu yangu Joseph Meza ni mzoefu amepitia katika sekta nyingi za serikali naamini ataweza kusaidia. Lakini pia nimuombe aendelee kujenga

ukaribu na wafanyabiashara ili kuweza kuishauri serikali katika maeneo hasa masuala ya kodi ambayo ni kazi yake kubwa kabisa. Eneo moja nimshauri Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uliokuwepo sasa hivi watu wanatozwa katika mahoteli *rate* ya dola mia hasa zile ambazo kama unataka uingie katika mfumo wa *VAT*.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba hakuna hoteli hata moja itakayokuwa na *rate* au zitakazoweka zile zile katika mwaka mzima. Kwa sababu mwaka tumeona kama juzi kipindi cha mvua hakuna maeneo unaweza kwenda kwa sababu hapavutii hata wageni wanaokuja unaona hata ndege zinasitisha. Lakini ukiangalia bado kodi iko vile vile lakini katika kodi hii tunaambiwa tunaitarajia sisi kuipata Zanzibar asilimia 18 hata hawa wafanyabiashara pia wanatoa kamisheni zao kuna *booking outcome* anaweza kufuta asilimia 15 - 20 hawa kwenye mitandao na wamekamata. Nimesema hili kwa sababu neno la Zanzibar hatunalo sisi wenyewe watu wanalitumia tu huko na linakwenda linafanyakazi kwenye mitandao.

Sasa mtu anapofanya *booking* anataka kuja Zanzibar anaangalia analipa kwa *credit card* atalipia atakapofika hapa lakini asilimia hamsini mtoaji lazima achukue ile kamisheni yake. Sasa lazima tuangalie haya hizi fedha ambazo wanazozipeleka katika *return* zao za *VAT* ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Naomba uniongeze nyengine mbili nimalizie Mhe. Mwenyekiti.

Lakini halikadhalika naomba hilo nimalizie naona Mhe. Mwenyekiti, atakuwa ameshalisikia Mhe. Waziri. Lakini pia nataka niseme kwa suala la Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, niishauri *ZIPA* kwa kushirikiana na Serikali na Tume ya Mipango nikiamini kwamba wao ndio wana uwezo kwamba kodi ambazo tuna-*charge* Pemba, mazingira ya biashara ambayo tumewawekea watu kutoka Pemba haitaweza kuendelea, ili tufanye tuanze kutoa *incentive* kwa ajili ya Pemba kama kodi za *tax holiday* kwenye viwanda hasa maeneo ya Micheweni tuweze kuendeleza Pemba. *Airport* yetu leo bado haijasimama lakini pia Pemba kama unataka miradi mikubwa pia ya kilimo iweze kulisha Zanzibar, kwa hiyo tuangalie mpango maalum duniani kote kumefanyika hayo. Hata katika masuala ya ulipaji ya mishahara huwezi kulipa kodi Pemba ambayo mtu anayelipa Pemba akalipa yule ambaye aliyekuwepo Unguja, hata katika mishahara huwezi kumlipa mtu katika sekta binafsi shilingi laki tatu akalipe *ZSSF* akalipe na kodi nyengine zote, mtu wa Pemba anafanyabiashara na mtu wa Unguja mazingira ni tofauti.

Halikadhalika Mhe. Waziri utakapokuja utatwambia kuhusu suala la deni la taifa naona limeongezeka na najua umekuwa unashiriki katika vikao vya kama *observer* katika *IDB* ambayo ni sehemu ya *OIC* kwa hiyo utatueleza zaidi. Lakini pia katika ukurasa wa 31 umezungumza katika miradi ya *PPP* utatoza miradi ya aina gani.

Lakini pia kwenye *issue* naungana na Waheshimiwa walizungumzia kuhusu suala la *ATM* na mimi nikuombe tu kwenye *ATM* kwenye jimbo langu Dunga na maeneo ya jirani na jimbo la Mhe. Mihayo Juma N'hunga ututafutie mpango na sisi ili tuweze kufaidika na *ATM* ya chuo cha *SUZA* ndani ni mbovu inavuja na muda mrefu inawezekana ikaja kuanguka iko hatarini.

Nimalizie tu kwa kusema kwamba kwenye suala la uhakiki wa mali za serikali tunahitaji mafunzo zaidi ili tuweze kuishauri serikali. Kwa mfano, mimi mwenyewe Mhe. Waziri naona

haya lakini inabidi nikuombe pale *Victoria Garden* kuna nguzo za taa ambazo zimewekwa muda mrefu lakini mimi nahisi naweza kuwasaidia wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu. Kwa hiyo, naomba uyapokee maombi yao rasmi hii mara ya pili nazungumza najua zile mali zinasimamiwa chini ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Mhe. Haji Omar Kheri, basi kwa unyonge kabisa na lugha ya unyenyekevu mnaweza mkanisaidia mkanipa utaratibu ili niweze kufaidika kwa ajili ya wananchi.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana taasisi zote, niwapongeze taasisi kama *ZIC* kwa kazi nzuri wanayoifanya na waendelee kutoa sadaka zao bila ya mtu kujua kwenye mwezi mtukufu hiyo ndio *Tawhid* yenyewe. Niwapongeze pia *ZSSF* pamoja na *PBZ* kwa kazi nzuri mpaka hapo nawashukuru. *(Makofi)*

Mimi niseme naunga mkono hoja kwa matarajio kwamba Mhe. Waziri atakapokuja aweze kueleza yale ambayo nimeyakusudia ambayo nimeyaeleza na kuchangia, sina lengo la kupiga buti nitaunga mkono kwa kutegemea Mhe. Waziri atanipa maelezo mazuri.

Baada ya hapo nachukua nafasi ya kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi ambaye atakuwa ni mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo. Mhe. Rashid Makame Shamsi karibu sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya dakika kumi zilizobaki ili niweze kuichangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango iliyo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kutoa shukrani na pongezi sana kwa Mhe. Waziri, lakini vile vile kwa Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa taasisi hii kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niipongeze Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa uwasilishaji wao na nimpongeze Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni ambaye ni Mwenyekiti wa Kamti pamoja na muwasilishaji. Niwapongeze pia wenzangu walionitangulia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika michango yangu. Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii kama nilivyoisifu ni moja kati ya hotuba nzuri sana na kitabu chake ni maalum kuliko vitabu ambavyo vimetangulia, unaiona hasa kwamba hii ni hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango imepangika vyema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuipitia hotuba hii nilipata tabu kidogo katika mipangilio ya yaliyomo kutoka sehemu (a) mpaka sehemu (e) yaliyomo yameendana sawa na nambari za kurasa, lakini kutoka sehemu (e) hadi sehemu (t) yaliyomo hayaendani sawa na nambari za kurasa. Naomba watendaji waipitie na hii inawezekana ni uharaka, inawezekana ni sababu za kibinaadamu. Kwa hiyo, nilipata tabu kidogo kwa sababu ukiangalia haiendani na kurasa. Niwaombe sana wakala wa uchapajii kuwa makini katika kupangilia yaliyomo na nambari za kurasa ni binaadamu inawezekana wamekosea.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa kwenye majukumu ya wizara, nimeyasoma vizuri zile *statement* za majukumu zimekaa vizuri na niliweza kulinganisha *statement* za mwaka jana za majukumu ya

wizara na *statement* za mwaka huu. *Statement* za mwaka huu kama vijana wanasema zimekwenda shule, zimeongezeka kutoka tano zimekuja saba na kuna *statement* inasema "Jukumu la kusimamia uchumi". Hili ni jukumu kweli na hili ni jukumu mama wa Wizara ya Fedha na Mipango ambalo sikuliona katika *statement* ya mwaka jana.

Lakini kuna *statement* ya majukumu inasema "Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi". Hii ni *statement* muhimu na ni jukumu mama kwa Wizara hii ya Fedha na Mipango. Ukweli haya ni majukumu ya msingi ya wizara na nina hakika tulikuwa sijui tunaendaje hapo awali ukiacha majukumu haya kutokuwemo katika *statement* ya mwaka jana. Nipongeze sana Mhe. Waziri kwa kuweza kuyaona majukumu haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukusanyaji wa mapato, kwanza nitoe pongezi kwa waziri na watendaji wote wanaokusanya mapato ya serikali kupitia vianzio mbali mbali vya taasisi za wizara hii wamejitahidi sana. Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa kwamba kuna ongezeko la asilimia 52.6 za makusanyo ukilinganisha na za mwaka 2017-18. Hii ni hatua kubwa sana ya serikali iliyopiga tunapaswa tuwapongeze sana wakusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado ninaamini kwamba wizara ina uwezo wa kukusanya zaidi kuliko hizi kama watendaji watakuwa waadilifu, nina hakika kwamba mapato yataongezeka, kuna baadhi ya watendaji bado si waadilifu lakini wakiwa wote waadilifu mapato yataongezeka bado kuna mianya ambayo inavujisha mapato. Tukiweza kuiziba hii mapato Zanzibar yataongezeka. Lakini vile vile njia za kisasa za ukusanyaji wa mapato lazima twende sasa katika *electronic*. Vile vile wananchi wakihamasishwa na wakihamasika tuna uwezo wa kukusanya mapato. *(Makofi)*

Lakini jengine makadirio yaendane na vile vianzio vya mapato katika kila taasisi. Hivi sasa kuna hali ambayo kuna viashiria kwamba yale makadirio hayaendani na vile vianzo vya mapato. Kwa hiyo, kama tutakwenda hivyo basi tutafika. Lakini vile vile elimu kwa wakaguzi wetu wa ndani na wale wanaokusanya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika usimamizi na uwekezaji wa mali ya umma ukurasa wa 17. Mhe. Mwenyekiti, katika propgramu hii kwanza niipongeze kwa kuweza kuanzisha mamlaka maalum ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Kwa kweli, tumepiga hatua kubwa, tulipokuwa hatuna chombo hichi kwa kweli kulikuwa na mapungufuu mengi. Lakini kwenye uwekezaji nichukue fursa hii nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuhamasisha mabalozi wetu wa nje kuitangaza diplomasia ile ya uchumi ambayo itawakaribisha sana wawekezaji kuja kwetu.

Mhe. Mwenyekiti suala hili kuhusiana na mali za umma lina kasoro lina mapungufu kidogo, kuna ubadhirifu wa mali za umma kuna kukosekana kwa *asset register* katika baadhi ya taasisi. Lakini vile vile baadhi ya *asset register* katika taasisi haziko kamili zina mapungufu mengi, na vile vile kumekosekana na mfumo wa aina moja wa daftari ya kumbukumbu za mali lakini vile vile, baadhi ya taasisi kumekosekana hata hati miliki za mali zetu. Lakini uondoshwaji wa mali vile vile wakati mwengine baadhi ya taasisi hauendi kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Lakini nimegundua vile vile, hata taratibu nyengine, taratibu za kukabidhiana mali katika taasisi wakati mwengine zinakiukwa na pale ndio mali nyingi zinapotea.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili hatuko vizuri sana, hatuna sera madhubuti ya uchumi na sera

za kodi kwa muda mrefu. Sera ndio inayotoa *direction* na muongozo, bila ya sera maana yake ni sawa sawa na ngalawa ambayo imekata nanga itakuwa inaelea tu. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuweza sasa kuamua kuichungulia sera inayoshughulikia na kodi pamoja na uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika jimbo langu kuna programu hii ya ujenzi wa misingi ya maji machafu ya mvua. Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii, kwanza niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kufikiria mradi huu ambao jimbo langu litakuwa linafaidika na mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ndani ya jimbo langu la Magomeni umezihusisha Shehia za Magomeni na Shehia ya Meya. Hivi sasa ni muda mrefu na mradi ule ulichelewa kwa sababu kutokana na kuchelewa kwa kulipa fidia. Wananchi wangu wa Magomeni Mhe. Mwenyekiti, wanataka kusikia Kauli ya Waziri atakapokuja kwamba mradi huu kwa Shehia ya Meya na Magomeni watarajie mafanikio lini. Lakini vile vile kwa shehia za kwa Mtumwajeni na Sogea vile vile wanaulizia lile bonde la Mwantenga na bonde la Sogea Sebleni kwamba ule mradi utaingia katika *phase* ipi, ili tuweze kuona kwamba na wao wanaweza kufaidika katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie dakika moja kwa kuzungumzia Programu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi. Mhe. Mwenyekiti, tuna utaratibu wa mipango ya kitaifa na kupunguza umaskini, Zanzibar ina mpango wa MKUZA na hivi sana tuko MKUZA III. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina dira 2020, tunatarajia 2020 Zanzibar ifikie uchumi wa kati. Nimuulize Mhe. Waziri, wenzetu Tanzania Bara dira yao ni 2025 wanatarajia 2025 uchumi wao utakuwa ni wa kati uchumi wa viwanda. Lakini mimi naona hii *trend* yetu ya uchumi inaendelea taratibu. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja atuhakikishie je, tutakapofika 2020 Zanzibar itakuwa na uchumi wa kati hii *trend* ambayo tunakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo najua muda wako unakaribia nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kufunga dimba katika siku hii ya leo. Naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Niwaombee waislamu wote sikukuu njema ya Idd el Fitri, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa mashirikiano na michango ambayo mmeweza kumsaidia Mhe. Waziri na hadi hapa naomba niakhirishe kikao hichi cha Baraza kwa siku ya leo hadi siku ya kesho mnamo saa 3:00 asubuhi.

(Saa 8:58 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 13/06/2018 saa 3:00 asubuhi)